ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Piliwa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma naUtawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri waMiundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.

14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Kiembesamaki
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani

30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
32.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasiza Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais
51.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
52.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake

53.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
54.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
55.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani
56.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Jimbo la Mpendae
57.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Nafasi za Wanawake
58.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
59. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
60.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
61.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
62.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
63.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
64.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
65.Mhe. Rashid Seif Suleiman	Jimbo la Ziwani
66.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
67.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
68.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
69.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
70.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
71.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
72.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
75.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Jimbo la Dole

76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake
Ndugu Yahya Khamis Hamad	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Ishirini na Saba – Tarehe 23 Julai, 2012

(Kikao Kilianza saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kwanza karibuni sana kama tulivyokuwa tumepanga kuendelea nazo leo.

Waheshimiwa Wajumbe Taarifa ya Spika ambayo ninapenda nitoe leo ni kwamba katika shughuli zenu au katika shughuli zetu ambazo tumefanya katika Mkutano wa Nane wa Baraza la Nane la Wawakilishi ulioanza tarehe 13 Juni, 2012, Baraza lilipitisha Mswada mmoja wa sheria ambao ni kama ifuatavyo.

Mswada wa Sheria ya Kutozwa kodi na kubadilisha baadhi ya sheria za fedha na kodi kuhusiana na ukusanyaji na udhibiti wa mapato ya serikali na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Kama inavyotakiwa chini ya Kifungu 90 (3) cha Kanuni za Baraza la Wawakilishi toleo la mwaka 2012, ninaomba kutoa taarifa kwenu Waheshimiwa Wajumbe kwamba Mswada huo sasa umekuwa ni sheria kamili baada ya kupata saini ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. (Makofi).

Hiyo ndio Taarifa ya Spika ambayo inatokana na kazi nzuri muliyoifanya wakati wa mjadala wa bajeti ya serikali

Waheshimiwa Wajumbe kama kawaida na leo tuna wageni ambao wamefika katika ukumbi wetu wapo juu pale, na wageni hawa ni Chuo cha Utawala wa Umma cha Zanzibar, jumla yao ni wanafunzi 23 pamoja na walimu wawili. Naomba wageni wetu hao wasimame kuwasalimu Waheshimiwa Wajumbe.

Wageni wetu karibuni sana na Waheshimiwa Wajumbe ahsanteni sana.

Waheshimiwa Wajumbe kuna taarifa ya rambirambi ambayo Ubalozi wa Norway kupitia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ametuma, na pia Rais wa Zanzibar ametuma ili wananchi waweze kujua kwamba ubalozi huo wanaungana na wananchi wa Tanzania na Zanzibar katika msiba mkubwa uliotokea hivi karibuni.

Naomba taarifa hiyo pia niisome. Waheshimiwa Wajumbe mutaniwia radhi sitoweza kutoa tafsiri kwa sababu ipo katika lugha ya Kiingereza lakini ninaelewa kuwa mutaipata vizuri.

ROYAL NORWEGIAN EMBASSY

Plot No. 55/2012

The Royal Norwegian Embassy presents its complements to the Ministry of Foreign Affairs and International Cooperation of the United Republic of Tanzania and has the honour to request the latter to transmit a condolence message from the Government of the Kingdom of Noway to the President of The United Republic of Tanzania H.E Jakaya Mrisho Kikwete and the President of The Revoluntionary Government of Zanzibar Dr. Ali Mohamed Shein.

It is with great sadness and profound sorrow that we have learned about the ferry disaster that happened in Zanzibar on 18th July, 2012.

In the wake of this terrible tragedy, involving the ferry MV Skagit, the Government of Norway would like to express heartfelt sympathies and deepest condolences to the President of the United Republic of Tanzania, the President of the Revolutionary Government of Zanzibar, the people of Tanzania as well as the families of the deceased.

The Royal Norwegian Embassy avails itself of this opportunity to renew to the Ministry of Foreign Affairs and International Cooperation of the United Republic of Tanzania the assurances of its highest considerations

Hii imetumwa Dar es Salaam tarehe 19 mwezi huu wa Julai 2012 Waheshimiwa Wajumbe ninaomba mupokee kuitia kwa Marais wetu taarifa hiyo ya wenzetu Ubalozi wa Norway kuungana na wananchi wa Tanzania pamoja na wananchi wa Zanzibar kwa msiba uliotufika hivi karibuni.

Waheshimiwa Wajumbe ninakushukuruni na ahsanteni sana.

Waheshimiwa Wajumbe kabla hatujaendelea na shughuli zetu na kutokana na msiba uliotufika hivi karibuni shughuli zetu kidogo zimetetereka lakini ilikuwa ni halali kabisa kutetereka kutokana na msiba huo mkubwa, tulilazimika kufanya hivyo kiasi cha kwamba tupo nyuma sana ya ratiba.

Lakini isitoshe zaidi ya hivyo kabla ya hapo ilikuwa tupo nyuma siku juu ya ratiba yetu, kutokana na shughuli zetu kiasi gani zimepanuka. Lakini pia kwa kuwa huu ni mwezi wa Ramadhani na kwa mujibu wa Ibara ya 23 (4) ambayo tumejiwekea utaratibu kuwa mwezi wa Ramadhani shughuli zetu za Baraza. Naomba sasa niiosome hiyo Kanuni ili baadae tuone mambo mengine baada ya hapo tunafanya vipi.

Kanuni ya 23(4) “nyakati zilizotajwa katika fasili za 1, 2 na 3 ya Kanuni hii zitatumika katika siku zote za kazi isipokuwa siku ya Ijumaa na mwezi wa Ramadhani ambapo kwa siku ya Ijumaa kikao cha asubuhi kitaanza saa 3.00 asubuhi mpaka saa 6.00 mchana, na kikao cha jioni kitaanza saa 11.00 jioni na kumalizika saa 1.45 usiku, na kwa mwezi wa Ramadhani kikao kitaanza 3.00 asubuhi mpaka saa 8.00 mchana na hakutakuwepo na kikao cha jioni”.

Hivyo ndivyo kanuni ilivyojipanga kwa mwezi huu wa Ramadhani. Sasa kutokana na kanuni yetu, hii inabidi kuanzia leo tuende mpaka saa 8.00 mchana. Lakini kwa mujibu wa ratiba yetu tupo nyuma kwa muda wa siku kama tatu ambapo shughuli zetu zingetegemewa zimalizike tarehe 3 Agosti.

Sasa kwa vyovyote itakavyokuwa hatutomaliza katika kipindi hicho na hasa hasa kwa kuwa huu mwezi wa Ramadhani tumepunguza muda, utakuta kwamba kuna muda wa saa moja na dakika arobaini na tano tumepunguza kwa kila siku, hii itafanya wasaa wa kumaliza shughuli uwe mgumu zaidi, lakini zaidi tayari tupo nyuma kwa kiasi ya muda wa siku tatu.

Sasa ili tuweze kumudu angalau kufikia pahala pazuri lakini ninaamini pia hatutoweza kumaliza. Ningeomba Baraza hili baada ya Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kutoa hoja ya kutenga kando kanuni hii ya 23(4) angalau tuongeze muda wa dakika 30 kutoka zile saa 8.00 ili tupate mwanya kidogo wa shughuli zetu kuendelea, lakini hatimaye huko mbele ninafikiri itabidi tuje tuongeze muda vile vile kwa mujibu wa kanuni, lakini pia ninaelewa kwamba mwezi huu wa Ramadhani kila Mheshimiwa Mjumbe huwa anataka kuungana na familia kwa ajili ya mfungo wa mwezi wa Ramadhani.

Kwa hivyo baada ya kupiga mahesabu tumeona kwamba itasaidia kiasi kwa kuongeza nusu saa kutoka pale saa 8 ambayo imo kwa mujibu wa Kanuni ya 23(4).

Nimuombe basi Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais ili aombe ruhusa kwenu Waheshimwa Wajumbe twende kwa utaratibu huo ili tuweze angalau kufikia pahala pazuri, pamoja na kwamba baadae itabidi tuongeze muda, kwa sababu pia itakuwa hautotutosheleza kwa kuwa siku tatu tayari tulikuwa tupo nyuma ya ratiba.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa kuwa ratiba yetu ya shughuli za Baraza ipo nyuma, na kwa kuwa huu ni mwezi Mtukufu wa Ramadhani, na kwa mujibu wa Kanuni ya 23 (4) Baraza lako hili linatakiwa kumaliza shughuli zake saa 8 ili kuweza kumudu kumaliza shughuli zilizo mbele yetu za Baraza, naliomba Baraza lako tukufu liridhie muda ili tuongeze muda kwa nusu saa, kwa kuanzia saa tatu asubuhi mpaka saa nane na nusu mchana ili tuweze kumudu kufanya shughuli zilizo mbele yetu.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naafiki**.**

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha Hati mezani juu ya Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa mwaka 2012/2013. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Asha Bakari Makame (Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari: Mhe. Spika, kabla ya yote nichukue nafasi hii ya kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha kufika siku ya leo katika hali ya afya njema na mwezi Mtukufu wa Ramadhani, pia nichukue nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi hii ya kuwasilisha Hati mezani ya Hotuba ya bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo.

Naomba kuwasilisha.

Na. 51

Bustani ya Forodhani

Mhe. Ismail Jussa Ladhu – Aliuliza:

Miaka mitatu iliyopita bustani ya Forodhani ilifanyiwa matengenezo makubwa kupitia Taasisi ya Aga Khan yaliyopelekea kurudishwa kwa haiba na mandhari yake iliyokuwa imepotea, na mara baada ya matengenezo hayo na kufunguliwa rasmi na aliyekuwa Rais wa Zanzibar wa Awamu ya sita , Mhe. Dk. Amani Karume, kulikuwa na usimamizi madhubuti wa kanuni za matumizi ya bustani hiyo na huduma zinazotolewa. Hivi sasa hakuonekani tena umadhubuti ule katika kusimamia kanuni zilizowekwa, na kidogo kidogo mandhari na haiba yake imeanza kuharibika.

a) Serikali inachukua hatua gari kurudisha usimamizi wa kanuni za matumizi ya bustani hiyo ili fedha nyingi zilizotumika kuifanyia matengenezo zisiwe zimepotea bure.
b) Kutokana na yenyewe kushindwa kusimamia eneo hilo, kwa nini serikali isirejeshe usimamizi wa bustani hiyo kwa uongozi wa Taasisi ya Aga Khan ambao ulionekana kuimudu vyema kazi hiyo katika kipindi ilipokuwa chini yake.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Alijibu:

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 51 lenye vifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo.

a) Mhe. Spika, naomba kwanza kumfahamisha Mhe. Mwakilishi kwamba ipo bodi maalum iliyoundwa kusimamia bustani ya Forodhani, bodi hiyo inajumuisha Baraza la Manispaa, Mamlaka ya Hifadhi ya Mji Mkongwe na Uwakilishi wa Aga Khan uliopo Zanzibar.

Bodi maalum ya Bustani itachukua juhudi za makusudi na za ziada kuhakikisha kwamba taratibu zilizowekwa zinafuatwa, ili mandhari ya bustani hiyo izidi kuimarika.

b) Mhe. Spika, usimamizi wa bustani hiyo haujawahi kusimamiwa na Taasisi ya Aga Khan isipokuwa Bodi ilikuwa ikipata msaada wa kifedha kutoka katika Taasisi ya Aga Khan ambao ulikuwa ukitumika kuhudumia bustani hiyo katika kipindi cha kuanzishwa kwake, ndio maana ikaonekana wakati ule ilikuwa iking'ara zaidi. Muda wa mkataba wa msaada wa kifedha umemalizika. Kwa hivyo bustani ya Forodhani inaendelea kusimamiwa na Bodi maalum hivi sasa.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante sana Mhe. Spika, na ninamshukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mafupi yanayojielekeza katika swali. Naomba kumuuliza swali moja tu la nyongeza Mhe. Spika.

Kwa sababu amesema tangu imekuwa ikiendeshwa na Bodi ya pamoja, na kwamba Taasisi ya Aga Khan ilikuwa ikitoa msaada wa kifedha tu. Lakini mwenyewe katika majibu ya hoja mbali mbali wakati wa bajeti ya afisi yake hapa alikiri kwamba kuna fedha si haba zilizokusanywa kutokana na shughuli zinazofanyika pale.

Sasa ni kipi kinachofanya viwango vya usimamizi vinateremka kwa mambo madogo madogo tu. Kwa mfano uvaaji wa sare kwa wale wanaotoa huduma kama ilivyokuwa mwanzo, kutandika makapeti sehemu za chini zinazotumika ili kutoharibu mandhari yake, kutoruhusu uingiaji wa baiskeli katika maeneo yale ya Forodhani, taa zake kuharibika, viguzo kuanguka na pia ukataji wa wananchi katika maeneo yenye bustani hasa za majani kwamba zote zikawa hazisimamiwi,

Kwa nini bodi hii imeshindwa kufanya kazi zake ambazo ilikuwa tangu mwanzo ilipaswa kuzifanya.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, naomba kwanza kabla sijamjibu naomba kutoa maelezo yafuatayo ninaamini yatasaidia sana kujibu swali lake la nyongeza.

Bustani ile ilipozinduliwa tarehe 2 Agosti, 2009 na Mhe. Rais Mstaafu, Mhe. Dk. Amani Karume kwa wakati ule Aga Khan Foundation kama nilivyosema walitoa pesa ambazo ziliruhusu kuwaajiri wafanyakazi watano, nao wafanyakazi watano ni kama *permanent staff* pale katika ile Bodi.

Halafu pili walisaidia kufanya *total allowance* ya *thirty percent* juu ya wafanyakazi wa Manispaa 17 ambao wanahudumia pale. Pia walikuwa wanasaidia kuchangia mafuta ya jenereta. Vile vile kulikuwa na kampuni ya ulinzi KK-Security pale, walikuwa wakisaidia kazi hiyo, na pia walikuwa wakisaidia katika ununuzi wa vitendea kazi.

Sasa mkataba huo ulikuwa ni wa mwaka mmoja. Sasa baada ya kumalizika mwaka mmoja Aga Khan wamejiondosha. Sasa wameikabidhi Bodi. Sasa Bodi kuziendeleza shughuli hizi inategemea yale mapato wanayoyapata ndio inabidi sasa wapate fedha za kuiendesha ile bustani.

Sasa tatizo liliopo kidogo mapato waliyonayo ni machache, lakini pili naomba nikiri kwamba mengine wala hayahitaji fedha kama vile alivyosema kuvaa sare, kusimamia, hayo ni matatizo ya usimamizi tu. Kwa hivyo Mhe. Spika, hilo tunalichukua, tutakaa na Bodi tuone kwamba suala la usimamizi pale hasa la ufuatiliaji linafanyika ipasavyo. Hilo ninachukua *observation* yake Mhe. Spika, ahsante sana.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kuwa Aga Khan alikuwa ajenge pamoja na uzio ule lakini kutokana na mambo yaliyojitokeza Zanzibar akaamua kukatisha miradi yake. Jee ni lini uzio ule utajengwa ili kusije kutokea ajali kama zile zilizotokea ikiwemo kwa wapita njia na gari kutumbukia baharini. Lini serikali itakuwa makini kujenga uzio ule.

Pili kuna taarifa kuwa pesa zinazokusanywa pale kama alivyosema Mhe Jussa kama milioni arobaini kwa mwezi zinapatikana. Kweli milioni arobaini zinashindwa kuweka bustani ile safi Mhe. Waziri.

Mhe. Spika: Swali la mwisho uliza tena Mhe. Jaku.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kuna taarifa Mhe. Spika, pesa zinazokusanywa pale kwenye bustani ya Forodhani karibu ni milioni arobaini kwa mwezi, leo bustani ile ikashindwe kuwekwa safi kwa milioni arobaini.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwanza Mhe. Spika, suala la uzio nimeshalieleza mara nyingi tu, na katika majumuisho na hata swali kwamba tayari mipango hivi sasa inakamilishwa na World Bank, *infact* hata Mhe. Waziri wa Ardhi, Majenzi, Makaazi na Nishati alizungumza kwamba taratibu ameshakamilisha za kumpata *contractor* wa kazi za uzio ili ziendelee. Kwa hivyo hiyo kazi inaendelea na imeshafika mahali pazuri sana.

Kuhusu ukusanyaji wa pesa shilingi milioni arobaini lakini bustani haiendi vizuri, kama nilivyosema ni kweli mimi ninakiri yapo matatizo ya kiutendaji yanahitaji kusimamiwa vizuri, tuone kwamba yale mambo ambayo yanafanywa pale inabidi yafanywe.

Lakini kubwa zaidi ni watu wetu kutofuata taratibu, mfano anaambiwa mtu asiyakanyage majani, lakini kwa jinsi *crowd* inavyokuwa kubwa na watu wanakwenda kupumzika jioni inakuwa vigumu kidogo kuwadhibiti. Sasa hiyo nikiri nayo pia tutajitahidi wao wenyewe waliajiri kampuni ya KK-Security.

Sasa baada ya kuondosha ule ufadhili wao na wale nao wameacha. Sasa tutajitahidi upande wetu serikali kulichukua kwa kushirikiana na Bodi, tuone kwamba hili suala linafanikiwa. Hizo fedha kweli zipo kwenye akaunti ya pamoja na ndizo zinazoendesha hivi sasa. Ahsante.

Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa ya kuuliza swali la mwisho la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri mimi labda nimuulize tu, pamoja na kwamba bustani ya Forodhani inashughulikiwa na Bodi ambayo ipo inashughulika na bustani hiyo. Jee kwa mwaka wa fedha uliopita 2011/2012, Bodi hii imekaa mara ngapi katika harakati za kuhakikisha kwamba bustani ile inakwenda sawa.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Bod hii ambayo kwa kweli inajumuisha watu wa Mji Mkongwe, *Municipal* pamoja na Aga Khan, kwa kweli sina uhakika hasa kwa kipindi kilichopita wamekaa muda gani. Hilo naomba nilichukue nikalifanyie kazi na nitawajuulisha rasmi.

Na. 80

Watumishi wa Muungano Kulipa Kodi ya Mapato Zanzibar

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:

Mhe. Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa fursa hii kuweza kuuliza swali Na. 80 lakini kabla kujibiwa swali hilo naomba kifungu (a) niliondoshe kutokana na jawabu imeshajibiwa katika kipindi cha bajeti, hivyo ibaki kifungu (b) na (c).

Katika mwaka wa fedha 2011/2012 Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo alisema watumishi wa Muungano wataanza kulipa kodi ya mapato Zanzibar badala ya kuingiza katika mfuko wa Serikali ya Muungano.

a) Jee ni kiwango gani kimekusanywa hadi sasa kuanzia Julai mwaka jana.
b) Jee ni watumishi wangapi wa Taasisi za Muungano na Mashirika ya Umma ya Muungano ambao wanafanya kazi Zanzibar.
c) Kwa kuwa kodi anayolipa mfanyakazi lengo lake kubwa ni kuboresha upatikanaji wa huduma. Jee, serikali imejitayarisha vipi na utoaji wa huduma za uhakika kama za afya, maji, na umeme.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo jibu swali (b) na (c), (a) liache kwa sababu ulikwishatoa majibu huko nyuma.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo – Alijibu:

Mhe. Spika, kabla sijajibu swali la Mwakilishi makini Mhe. Jaku Hashim Ayoub, naomba na mimi kwa idhini yako na kwa ruhusa yako niwatakie Ramadhani njema Waislamu wote wa Zanzibar na duniani, na niwaombe basi tuheshimu mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani ili Mwenyezi Mungu aweze kutupatia fadhila za Ramadhani.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo, sasa naomba kabla ya kujibu swali la Mhe. Jaku Hashim Ayoub lenye kifungu (b) na (c), naomba nitoe maelezo mafupi yafuatayo.

Katika kikao cha Mawaziri wa Serikali ya Muungano na wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kilichofanyika Dar es Salaam tarehe 19 Machi, 2011 ambacho kilijadili kero za muungano, kikao hicho kiliagiza pamoja na mambo mengine kurekebisha sheria ya kodi ya mapato ili kuruhusu kodi ya mapato yatokanayo na ajira ya *payee* iweze kuhamishwa na kutumika pale walipo wafanyakazi husika.

Kikao hicho kilielekeza kwamba marekebisho hayo yafanyike na kuingizwa kwenye Mswada wa Fedha wa mwaka 2011/2012. Hatua za marekebisho za sheria hiyo haikuweza kukamilika kama ilivyotarajiwa. Baada ya maelezo hayo naomba sasa kujibu swali la Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo.

(b) Zoezi la kuwatambua watumishi hawa kwa ukamilifu lipo kwenye hatua za mwisho chini ya Mamlaka ya Mapato Tanzania. Zoezi hili litahusisha pia taasisi binafsi ambazo zina matawi Zanzibar, ambazo kodi za mapato za watumishi hao zinabaki Tanzania Bara.

c) Mhe. Spika, utoaji wa huduma za uhakika kwa upande wa afya, maji na umeme unahitaji fedha nyingi. Upatikanaji wa fedha zinazotokana na kodi ya mapato utasaidia sana katika mipango yetu ya kujiendeleza kwenye upatikanaji wa dawa, kuongeza kiwango cha upatikanaji wa maji safi na salama pamoja na kuimarisha utoaji wa huduma za umeme hasa katika maeneo ya vijijini. Hata hivyo serikali imepanga kuongeza bajeti kila mwaka kwa ajili ya upatikanaji wa huduma mbali mbali kwa uhakika kama vile huduma za elimu, afya na maji safi na salama.

Mhe Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, ninakushukuru kunipa fursa nyengine, na kabla ya kuuliza swali langu dogo naomba nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu mazuri lakini pia kwa kule kuamua kuwajumuisha hata wafanyakazi wa sekta binafsi ambao wanafanya kazi Zanzibar, lakini wanalipa kodi ya mapato kwa upande wa Tanzania Bara.

Swali langu la nyongeza Mhe. Spika, linahusu zaidi kifungu (c) ambacho muuliza swali alihusisha suala la ulipaji kodi na upatikanaji wa huduma. Swali langu kwa Mhe. Waziri ni kwamba katika kupitisha bajeti za Wizara mbali mbali tangu tumeanza kikao hiki hapa, imeonekana kwamba kuna maswali mengi yasiyo na majibu kuhusu vifungu mbali mbali vya bajeti vya wizara mbali mbali, ambavyo vinaonesha matumizi yasiyo mazuri au upangaji wa matumizi yasiyo mazuri ya fedha za walipa kodi.

Je, Mhe. Waziri anatuhakikishia vipi kwamba baada ya kazi kubwa iliyofanywa na wawakilishi ya kuvitambua vifungu hivyo, kwamba Wizara yake itachukua hatua ya kufuatilia matumizi yake, ili yale matumizi ambayo hayana tija yaondolewe na baadae yaende kuimarisha huduma muhimu kwa wananchi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwanza nataka niseme tu kwamba ofisi yangu itahakikisha vifungu ambavyo Waheshimiwa Wajumbe wamevitilia shaka, tutahakikisha matumizi yake yaendane au yaende kama ilivyotarajiwa.

Vile vile nataka nikuhakikishie tu Mhe. Mwakilishi kwamba katika kipindi kifupi baadhi ya vifungu hivi ambavyo tunaona kwamba vinaweza vikatumika vizuri zaidi kwengine zaidi, basi tunazihamisha fedha zake ili zitumike katika maeneo mengine ambayo ni muhimu zaidi.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii. Kwa kuwa ukusanyaji wa kodi unaendana sawa na upatikanaji wa huduma muhimu. Namuuliza Mhe. Waziri je, Serikali inawajibika vipi kwa umoja, kuhusiana na suala zima la usafi wa miji yetu, kwa kuwa inawaingiza hata watalii wanaokuja, wananchi wenyewe na afya za watu kwa jumla.

Je, Serikali inawajibika vipi kwa pamoja kuhusu suala la usafi, linaachiwa Baraza la Manispaa tu au ni suala ambalo linachukuliwa kipaumbele. Ni nini Serikali wajibu wake katika suala zima la usafi, baada ya wananchi kulipa kodi zao.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Kwanza nataka nikubaliane naye kwamba Serikali *is a collective responsibility*. Shughuli yoyote inayoendeshwa na Wizara yoyote na taasisi yoyote ilioko ndani ya serikali, inatakiwa ifanye kazi kwa pamoja kwa umoja wetu. Kwa hivyo, suala la usafi ni suala letu sote, ni suala la serikali nzima. Lakini katika kugawana majukumu tumewaachia Baraza la Manispaa pamoja na Halmashauri.

Lakini hivyo hivyo Mhe. Spika, nataka niseme tu kwamba sasa hivi ni lazima tuondoke na vile ambavyo tulivyozowea, kufanyakazi kwa mazowea. Tufanyekazi kwa kuangalia *value for money*, ile thamani ya pesa inayotolewa kwenda katika manispaa na mabaraza ya miji, basi tuangalie na kazi vile vile wanazozifanya.

Mimi nitamuomba tu Mhe. Waziri mwenzangu twendelee kushirikiana kwa upande wake, kama kunahitajika *resources* zaidi, basi tuendelee vile vile kuambizana ili tuweze kutoa *resources* zaidi, lakini wananchi ambao wanalipa kodi waweze kuona matunda yake. *The value for money*.

Nam. 13

Tatizo la Uuzaji wa Vyuma Chakavu Zanzibar

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: (Kny: Mhe. Ali Salum Haji) – Aliuliza:-

Mhe. Spika, hivi karibuni kumekuwa na tabia ya baadhi ya watu kuharibu miundombinu mbali mbali kwa lengo la kuuza shaba na vyuma chakavu.

(a) Je, Wizara ina mpango gani wa kupambana na biashara hii ya vyuma chakavu.
(b) Je, wauza vyuma chakavu wote wa Zanzibar wanatambulika kisheria.
(c) Kama wanatambulika kuna ukaguzi gani unaofanyika kukagua biashara zao.

Mhe. Naibu Waziri wa Bishara, Viwanda na Masoko – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake nambari 13 lenye vifungu (a), (b) na (c) linalohusiana na biashara ya chuma chakavu kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, biashara ya chuma chakavu imekuwa ni bishara kubwa kwa wananchi wengi katika visiwa vyetu, hasa baada ya kuumbuliwa teknolojia ya kusarifu vyuma vinavyotokana na vyombo au mitambo iliyokwisha kutumika na vyuma hivyo hutumiwa tena kama mali ghafi ya kuzalisha bidhaa mpya.

Kwa Zanzibar chuma chakavu kinapatikana kutokana na mitambo mibovu, magari mabovu, mabaki ya vyuma yanayotokana na matengenezo ya viwanja kama vya mpira na bandari, pamoja na vifaa mbali mbali ambavyo vilitengenezwa kwa vyuma na baadae kuchakaa na kushindwa kufanyakazi iliyokusudiwa.

Biashara hii mbali na kuongeza ajira na kipato, pia imesaidia usafi wa mazingira hasa katika kupunguza makachara yanayotokana na bidhaa za mitumba, yaani *used* zinazoingizwa kwa wingi kutoka nje. Tabaan Mhe. Spika, katika shughuli za aina hii changamoto huwa hazikosikani. Hivyo, nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kwamba wapo baadhi ya wananchi ambao wanatumia njia hii kwa kuharibu miundombinu kwa ajili ya kupata chuma chakavu kwa ajili ya kufanyia biashara hiyo.

(a) Kutokana na sababu nilizozitaja hapo juu Mhe. Spika, na hasa zile za kimazingira. Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko haikuona haja ya kupambana na biashara hiyo, bali imeona itakuwa ni jambo la busara zaidi kuweka utaratibu ufuatao, ambao ni pamoja na kupatiwa hati ya usajili, yaani *registration certificate* kwa wafanyabiashara wa aina hiyo, kupatiwa kibali cha usafirishaji yaani *export permit* kwa mfanyabiashara husika, kufanyiwa ukaguzi wa mzigo kabla na baada ya kufungwa kwenye makontena, kupiga marufuku usafirishaji wa shaba, nyaya za umeme, paipu, mifuniko ya makaro, vifaa vya transfoma na aina nyengine ya vitu vinavyopelekea uharibifu wa miundombinu.

(b) Ndio Mhe. Spika, wauza vyuma chakavu wa Zanzibar wanatambulika, kwani wizara imewasajili mpaka sasa wasafirishaji wa vyuma chakavu 11, chini ya sheria ya biashara nambari 4 ya mwaka 1989 na kanuni zake za usafirishaji bidhaa za mwaka 2011 kifungu 3(2).

(c) Wizara kwa kushirikiana na vikosi vya ulinzi kama vile KMKM, polisi na usalama kufanya ukaguzi kabla ya kufunganisha bidhaa hizo. Pia na wakati wa usafirishaji hapo bandarini kwa lengo la kuzuwia vitu ambavyo haviruhusiwi kusafirishwa.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kumuuliza swali moja dogo la nyongeza. Je, ni tani ngapi za vyuma chakavu na dhamani yake ni kiasi gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Bishara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, mpaka sasa tani za vyuma chakavu ambazo tumeweza kuzitolea vibali ili kusafirishwa ni 1,201, na tani hizo Mhe. Spika, zina thamani zaidi ya milioni 517,000,000.

Mhe. Shadya Mohamed Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kuweza kunipatia nafasi hii ya kuweza kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Je, Mhe. Naibu Waziri ni wafanyakazi wangapi wanaofanya biashara hii ya vyuma chakavu? na vyuma hivyo chakavu na vyuma hivyo chakavu vinasafirishwa nchi zipi?

Mhe. Naibu Waziri wa Bishara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, ni wafanyabiashara 11 ambao Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko imewasajili rasmi kwa biashara hii ya kupeleka nje ya nchi vyuma chakavu. Nchi ambazo mpaka sasa tumetoa vibali kusafirishwa vyuma hivyo ni Tanzania Bara, Kenya na Dubai.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Spika. Mhe. Spika, naomba kumuuliza swali moja la nyongeza Mhe. Naibu Waziri kwamba ukizingatia idadi au ukubwa au wingi wa tani ambazo amezitaja hapa kwa vyuma chakavu zinavyonunuliwa na thamani yake, haionekana kwamba ni biashara kubwa kiasi hicho ambayo inachangia kodi kubwa kiasi hicho kwa Serikali yetu. Lakini pengine hasara ya biashara hii kuruhusiwa ni kubwa kwa sababu watu wengi wanashajihika kwenda kuchukua vyuma hata katika maeneo ambayo yanatoa huduma. Kwa mfano kama maeneo hayo ambayo muuliza swali ameuliza.

Kwa hivyo, nilikuwa nataka kumuuliza Mhe. Naibu Waziri, hivi serikali haioni kwamba kuna haja ya kupiga marufuku biashara hii kwa hapa Zanzibar, ili kutowapa ushajihishaji wale wanaokwenda kuharibu miundombinu na mambo mengine ambayo yanagharimu huduma muhimu kwa wananchi na badala yake kunusuru huduma hizi kwa wananchi?

Mhe. Naibu Waziri wa Bishara, Viwanda na Masoko: Ahsante Mhe. Spika. Mhe. Spika, swali alilouliza Mhe. Ismail Jussa tayari nimelijibu katika jibu (a), kwamba baada ya kuzingatia umuhimu wa kupatikana kwa ajira kwa wananchi wetu, lakini pia sababu kubwa ya kwamba wanasaidia katika usafishaji wa mazingira kwa kuhamisha hayo makachara ya vyuma chakavu, basi wizara imeona ni vyema kuweka taratibu ambazo nimezieleza Mhe. Spika, wakati najibu swali hili. Pia utaratibu wa kufuatilia vyuma hivyo chakavu vinavyosafirishwa, kwa maana ya kwamba kuzuwia uharibifu wa miundombinu. Kwa hivyo, utaratibu mzuri tu umewekwa wa kufuatilia hili mpaka bandarini wakati makontena yale yanaondoka Mhe. Spika.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka 2012/2013

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, naomba nichukuwe nafasi hii kukushukuruni kwa michango ambayo mliitoa kwa makadirio ya bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, na tayari wanaonisaidia walikwisha waomba radhi wale ambao hawakupata nafasi kwa kuwepo wengi. Mimi niungane nao wasaidizi wangu hao kuwaomba radhi kwamba basi tayari itakuwa wamepeleka maoni yao kwa maandishi wale waliohitaji, kwa hivyo leo tumalize wizara hii kwa kufanya majumuisho.

Lakini kabla ya kumuomba Mhe. Naibu Waziri ili aanze na hatimaye waziri amalizie, niomba kwamba tujitahidi kubana muda, maelezo ya wazi ili hatimaye tumalize shughuli hii na Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika apate kuwasilisha baada ya hapo tuone mambo yanavyokwenda.

Kwa hivyo, nichukuwe nafasi hii sasa kumkaribisha Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, karibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia katika hotuba hii ya bajeti ya Wizara yetu, iliyowasilishwa hapa Barazani siku ya Jumatano tarehe 18/07/2012.

Mhe. Spika, kabla ya kuchangia na kumsaidia Mhe. Waziri wangu kutoa ufafanuzi katika michango na masuala mbali mbali yaliyoulizwa, naomba kuungana na Waheshimiwa Wawakilishi, kutoa mkono wa pole kwa Wazanzibari na Watanzania wote waliopoteza ndugu na jamaa zao, wazazi wao na marafiki zao katika ajali ya kuzama kwa meli, iliyotokea siku ya Alkhamis siku ya tarehe 19/07/2012. Mwenyezi Mungu awajaalie wenzetu ambao wametangulia mbele ya haki, awapeleke mahala pema peponi, amin. Wale ambao bado hali zao hazijawa nzuri kutokana na ajali hiyo, basi Mwenyezi Mungu awajaalie awape taafifu mapema, amin.

Mhe. Spika, naomba nianze kutoa ufafanuzi kumsaidia Mhe. Waziri wangu kwa baadhi ya masuala ambayo waliuliza Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu. Naomba nianze na Idara ya Maandalizi na Msingi Zanzibar. Katika idara hii Mhe. Mohamed Haji Khalid wa Jimbo la Mtambile, yeye amekuwa na wasi wasi kuhusu mtaala wa elimu ya maandalizi na msingi juu ya ufundishwaji wa ngazi za maandalizi.

Mhe. Spika, wizara ilitoa maelekezo kwa walimu wakuu, kwa wanafunzi wanaotoka maandalizi, wawatenganishe na wale wanaotoka mitaani ambao hawakupita katika skuli za maandalizi. Hii inawapa nafasi walimu waweze kuwapatia watoto programu maalum pamoja na kufundisha kwa mujibu wa uwezo wa watoto kwa hatua zao ambazo wamefikia. Walimu wetu wa darasa la kwanza walipatiwa mafunzo na jinsi ya kuwafundisha watoto hao.

Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak, yeye alitaka kujua skuli za msingi kufungua skuli za maandalizi imekuwa ni tatizo kubwa katika skuli zetu. Ni kweli Mhe. Spika, lakini sera yetu ya elimu ya Zanzibar ya mwaka 2006, imeeleza kuwa elimu ya maandalizi ni sehemu ya elimu ya lazima kwa watoto wote wa nchi hii. Katika kutekeleza hili Serikali imetoa fursa kubwa ya kuwahamasisha jamii, pamoja na watu binafsi kuanzisha skuli za maandalizi. Kwa upande wetu Serikali pia inaendelea kutoa elimu hiyo katika skuli zetu 30 za kujitegemea na kwa upande wa madarasa ya maandalizi yaliomo katika skuli za msingi, madarasa haya huanzishwa zaidi katika yale maeneo ambayo hayana aina yoyote ya skuli za maandalizi, ziwe za Serikali au za jamii au za watu binafsi. Skuli hizi huwa ni zile ambazo zina uwezo wa nafasi ya kuanzisha madarasa hayo, bila ya kuathiri usomeshaji wa wanafunzi wa madarasa ya msingi.

Mhe. Spika, Mhe. Fatma Said Mbarouk wa Amani, yeye alitaka kupata idadi ya madarasa, vyuo vya Quran vya Zanzibar kwa mpangilio wa Unguja na Pemba. Mhe. Spika, kwa sababu hivi vyuo ni vingi na madarasa ambayo tunayo ni mengi, nimeleta hii idadi ya vyuo na madarasa ambayo tunayo, naomba watendaji wako wasaidie kuwapa Waheshimiwa Wawakilishi, ili wayajuwe, asakheri wanaweza wakapata misaada labda ya misahafu, vijuzuu wakaweza kusaidia madarasa hayo na ikawa amesaidia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa jumla.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu wa Jimbo la Mji Mkongwe, yeye alisikitishwa sana kuwa kulikuwa na mradi ambao ulipangiwa kwa Skuli ya Kajificheni, lakini Wizara iliuhamisha mradi huo na kuupeleka katika Skuli ya Kisiwandui.

Mhe. Spika, wizara ililifuatilia suala hili na kugundua kuwa katika mwaka 2007/2008, Skuli ya Kajificheni ilitembelewa na Bibi Anne kutoka *British Tanzania Social*, ambaye akifanyakazi *TAP* kwa wakati huo. Katika ziara yake alitembelea Skuli ya Kajificheni ambapo alivutiwa sana na jinsi wanafunzi hao walivyoandaliwa na kupata hamu kubwa ya kusaidia. Kwa hivyo, aliahidi kusaidia Skuli ya Kajificheni na skuli moja ya mjini Zanzibar kwa kuzipatia maktaba.

Mhe. Spika, mwalimu huyu alionana na Mkurugenzi wetu Maalim Vuai na akamueleza namna ambavyo alivutika na namna ambavyo Skuli ya Kajificheni wanavyosomesha, na akataka kutusaidia. Lakini akasema kuwa basi tuandike *proposal*, lakini isiwe moja, tuandike kama mbili au tatu kwa skuli za mjini. Kwa hivyo, Wizara ikachekecha ikaona ipeleke na watu, ikapeleka Skuli ya Kisiwandui. Kwa bahati nzuri au niseme mbaya kwa Skuli ya Kajificheni, ilichelewa kupeleka *proposal* ile na Skuli ya Kisiwandui ikapeleka kwa haraka. Kwa hivyo, msaada ule ukaja moja kwa moja kwa Skuli ya Kisiwandui.

Hata hivyo, wafadhili hawa walipofanya ziara ya kufuatilia mradi huo katika Skuli ya Kisiwandui mwaka 2011 Juni, waliahidi pia kuishughulikia Skuli ya Kajificheni na kuwapa msaada huo wa maktaba. Hata hivyo, naomba kumueleza Mhe. Mwakilishi kwamba hilo sio suala kuwa wizara ilihamisha mradi huo kutoka Skuli ya Kajificheni na kwenda Skuli ya Kisiwandui, bali Skuli ya Kajificheni ilichelewa kuwasilisha makisio yao kwa mfadhili na hatimaye Skuli ya Kisiwandui waliwahi kusaidiwa kwa wakati huo.

Mhe. Shadya Mohamed Suleiman wa viti maalum, yeye alitoa mchango wake kwa maandishi na aliomba wizara kupunguza wimbi la watoto katika madarasa ya maandalizi. Mhe. Spika, ni kweli kuwa baadhi ya skuli zetu hasa za msingi, zina mrundiko mkubwa wa wanafunzi na husababisha usumbufu kwa walimu na watoto wetu. Hata hivyo, Mhe. Spika, ombi hilo tumelipokea, lakini pia Wizara inatoa shukrani kwa wananchi kwa jitihada zao na kuona hilo na kuendelea kujitolea kuanzisha ujenzi wa miradi ya madarasa kwa nguvu zao katika majimbo mbali mbali.

Aidha, Wizara itaendelea kushirikiana na wananchi pamoja na washirika wetu wa maendeleo katika kuziondoa changamoto hizo. Nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi, na viongozi wote wa shehia, wadi na majimbo kushirikiana zaidi na kuwaandalia watoto wetu mazingira bora ya kujifunzia ili wapate kupata elimu bora.

Mhe. Spika, Mhe. Rufai Said Rufai Mwakilishi wa Jimbo la Tumbe, yeye alizungumzia skuli ya Tumbe haina umeme. Mhe. Spika, kwa sasa wizara yangu haijajipanga kutoa huduma hii kwa skuli zake. Kamati za skuli zinaanzisha na kupeleka huduma hii katika maeneo ya skuli na wizara yangu husaidia kila pale hali inaporuhusu. Pia Mhe. Rufai Said Rufai alieleza skuli ya Mazizini igaiwe.

Mhe. Spika, wizara imeanza kwa utaratibu wa kuzigawa skuli toka mwaka 1980, lakini kabla ya kuzigawa huwa kuna vigezo vingi vya kuangalia. Hii ni pamoja na idadi ya vyumba vya kusomea, idadi ya wanafunzi, idadi ya walimu pamoja na sifa nyengine.

Mhe. Spika, kwa upande wa Skuli ya Sizini kwa sasa tunashauri ibaki kama ilivyo. Kwanza idadi ya vyumba vya kusomea ni 11 tu mbali ya yale madarasa matatu ambayo tunaanzisha. Pia idadi ya wanafunzi sio wengi ni wanafunzi 878 tu. Kwa hivyo, tunamuomba Mhe. Rufai Said skuli hii ibakie kama ilivyo na baadae tutatizama uwezekano wa kuweza kuigawa.

Mhe. Salma Mohamed wa viti maalum pia na yeye alituchangia kwa maandishi na yeye alizungumzia tatizo la walimu wa sayansi, limekuwa sugu na baadhi ya skuli kama vile ya Vikunguni hakuna hata mwalimu mmoja. Mhe. Spika, tatizo la walimu wa sayansi ni tatizo la kitaifa na sio skuli ya Vikunguni peke yake. Kama tulivyokwishaeleza kuwa Wizara yangu inafanya kila jitihada ili kupunguza kama sio kuondoa tatizo hili la walimu wa sayansi. Hata hivyo, Skuli ya Vikunguni ni skuli inayosomesha masomo ya *art* tu na sio ya sayansi na kuna wanafunzi 35 ambao wanatarajiwa kufanya mitihani yao ya kidato cha nne mwaka 2012 kwa masomo ya *art* tu.

Mhe. Hassan Hamad Omar, Mwakilishi wa Jimbo la Kojani, yeye alisema kuwa skuli za mashamba hazipati michipuo hasa ile ya Kojani na Chwale. Mhe. Spika, katika matokeo ya mitihani inategemea zaidi mazingira ya skuli ikiwa ni pamoja na umahiri wa walimu katika kufundisha, wazazi na wanafunzi wenyewe. Kutokupasisha wanafunzi wa michipuo sio kwa skuli hizo tu, zipo skuli nyingi za Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, kwa upande wa Skuli ya Chwale kwa mwaka 2011 umeanza kujikomboa, umepasisha wanafunzi watatu kuingia michipuo mbali mbali. Kwa hilo naomba mashirikiano zaidi kwa jamii, uongozi wa skuli, Waheshimiwa Wawakilishi na Wabunge kuchangia zaidi ili kuweza wanafunzi wa skuli zetu kutoka kwa wingi katika michipuo.

Mhe. Mohamed Haji Khalid, Mwakilishi wa Jimbo la Mtambile, Skuli ya Sekondari Kengeja inakabiliwa na tatizo la ukosefu wa umeme na kupelekea wanafunzi kulala kizani. Mhe. Spika, Skuli ya Sekondari ya Ufundi Kengeja kwa muda mrefu ilikuwa ikikabiliwa na deni la umeme, sasa skuli hiyo inatumia umeme wa LUKU, kwa hivyo wakati inaponunua umeme huo kutoka katika Shirika la Umeme, asilimia kubwa ya fedha hizo hufidiwa deni la nyuma. Hata hivyo, tutajitahidi kuona mara zote umeme haukosekani labda kwa bahati mbaya.

Mhe. Mohamed Haji Khalid pia alitaka kujua Skuli hiyo ya Kengeja ya Ufundi inakabiliwa na tatizo la walimu wa somo la umeme na akasema kwamba tuliwaambia kuna walimu kutoka Unguja, je mwalimu huyo mpaka leo hajafika. Mhe. Spika, mwalimu wa somo la umeme kutoka Unguja kwenda Pemba alifika mwishoni mwa mwaka 2011. Katika mwezi wa Februari, 2012 aliacha kazi na kurudi Unguja. Pamoja na hayo katika jitihada ambazo imechukua ni kuwasiliana na tume ya utumishi serikalini, ili kufahamu kuwa kuna vijana ambao tayari wamesomea masomo ya ufundi katika ngazi ya shahada, ili wapewe fursa ya kufundisha katika skuli ya ufundi Kengeja na masomo ya kompyuta sayansi ya biashara katika Skuli ya Utaani.

Mhe. Spika, Mhe. Fatma Said Mbarouk, pia alitaka kujua ni utafiti gani umefanywa ili kujua wanavijiji wangapi wamefaidika katika kisomo cha watu wazima kupitia vyombo vya habari. Mhe. Spika, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kwa kupitia idara ya elimu mbadala na watu wazima inatoa elimu kwa wana kisomo na jamii kwa jumla, kwa kupitia njia mbali mbali

ikiwemo vyombo vya habari. Lengo la kutumia vyombo vya habari ni pamoja na kuelewesha jamii juu ya programu mbali mbali zinazoendeshwa na idara na kupata ushiriki wao, ili kujua wananchi na wanakisomo wanafaidika kwa kiwango gani. Idara kwa kuwatumia waratibu wake wa wilaya, imekusanya na kuweka kumbukumbu sahihi ongezeko la kimasomo katika kila wilaya, shehia na kwa kila mwezi.

Idara pia katika kufanikisha zoezi hili, hivi sasa inaendelea na matayarisho ya kufanya utafiti na kutaka kujua hali ya kisomo ilivyo katika visiwa vya Unguja na Pemba. Madodoso kwa ajili ya utafiti huo tayari yametayarishwa na kujaribiwa. Hivi sasa yanapitiwa na kufanyiwa marekebisho kabla ya kufanyika kwa utafiti wenyewe. Katika masuala ambayo yamo katika madodoso hayo ni pamoja na hali ya matumizi ya vyombo vya habari kwa wanakisomo vikiwemo redio, TV na magazeti. Mhe. Spika, ni mategemeo yangu kwamba matokeo ya utafiti huo yataweza kutoa picha halisi ya hali ya kisomo pamoja na kiwango cha matumizi ya vyombo vya habari kwa jamii hasa vijijini.

Mhe. Spika, Mhe. Ismail Jussa Ladhu, alizungumzia kadhia ya Mwalimu Ameir Makame Ameir wa Skuli ya Uzini Unguja. Mhe. Spika, mwalimu huyu alituhumiwa kubaka mwanafunzi wa kike wa darasa la sita wa Skuli ya Unguja Ukuu mwaka 1999, jina lake Mhe. Spika, tunalihifadhi. Kesi hii iliripotiwa kwa ofisi ya upelelezi Mkoa wa Kusini Unguja kwa hatua zaidi. Mtuhumiwa huyu alifikishwa mahakamani na baadae kuachiwa huru kwa sababu ya kukosekana ushahidi.

Lakini Mhe. Spika, ninalotaka kumfahamisha Mhe. Ismail Jussa Ladhu, pamoja na wajumbe wa Baraza lako tukufu kuwa huyu Mwalimu Ameir Makame wa Skuli ya Uzini, hii kesi ya ubakaji Mhe. Spika, sio kesi ya kwanza. Hii ni kesi ya tatu na kama wizara tumekuwa tukichukua hatua mbali mbali. Naamini Mhe. Ismail Jussa kama anajua kuwa mwalimu huyu hii ni kesi ya tatu, basi asingesimama na kumtetea, kwa sababu siku zote Baraza lako tukufu Mhe. Spika, tumekuwa tukizungumza na tukionesha vilio vyetu na hisia kali, juu ya watoto wetu ambao wanabakwa, wengine wanapata mimba za utotoni, lakini mahakama inamuachia mtuhumiwa na kusema hana ushahidi.

Mhe. Spika, tuchukulie hii kesi ya tatu kama ambavyo nimezungumza. Mwalimu huyu alishtumiwa kubaka mwanafunzi wa kike wa Skuli ya Mtende mwenye umri wa miaka 14 katika mwaka 2001, hiyo ni kesi ya pili. Kesi nyengine iliripotiwa katika Ofisi ya Mkuu wa Upelelezi wa Mkoa wa Kusini Unguja na hatua za baadae kufikishwa mahakama ya Vuga, mwishowe ilionekana kuwa hakuna ushahidi wa kutosha na mwalimu huyu aliachiwa huru.

Kesi ya tatu mwalimu huyu akiwa katika Skuli ya Uzi, alituhumiwa kubaka mwanafunzi wa kike, jina la mwanafunzi tunalihifadhi, mwenye umri wa miaka 13 mwaka 2009. Kesi hiyo ilipelekwa katika mahakama Mwera, pia aliachiwa huru kwa sababu hakuna ushahidi. Katika kesi zote hizo mtuhumiwa huyu, kwa vipindi tofauti wizara imekuwa ikimsimamisha kazi kwa tuhuma hizi na kutoa nafasi kwa vyombo vya upelelezi kufanya kazi yake.

Mhe. Spika, mfanyakazi huyu tumemrudisha kazini, lakini kwa ushauri wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na ushauri wa sisi viongozi wa Wizara, tumeona sio vizuri kumrudisha skuli tena kucheza na watoto, kwa sababu atatumalizia watoto na ushahidi haupatikani. Kwa hivyo, tutampeleka katika ofisi zetu nyengine kuendelea na kazi, lakini nilitaka kuonesha Baraza la

Wawakilishi juu ya matatizo ya mwalimu huyu, na nimeambatanisha na kesi zote, ushahidi wote pamoja na barua zote ambazo tulikuwa tukizitoa kabla ya kesi hii. Mhe. Spika, naomba hii halafu nimkabidhi Mhe. Ismail Jussa Ladhu.

Baraza la Upimaji na Tathmini ya Elimu, hoja hii ilizungumzwa na Mhe. Mohammed Haji Khalid na Mhe. Saleh Nassor Juma kuhusu usahihishaji kutoka Pemba. Mhe. Spika, ni kweli kuwa idadi ya wasahihishaji, watayarishaji matokeo ni kama ilivyotajwa na Mhe. Mjumbe, kwamba wasahihishaji wa Kidato cha Pili ni 15 na wasahihishaji wa Darasa la Saba ni 7.

Hali hii inatokana na ufinyu wa bajeti, pia naomba kufahamisha kuwa kila msahihishaji mmoja kutoka Pemba anapokuja Unguja, anatakiwa alipwe posho la kujikimu, malipo ya kazi husika pamoja na nauli ya kwenda na kurudi. Hivyo, bajeti yetu haikidhi kuchukua walimu wengi kutokana na gharama hizo, ikiwa bajeti itaruhusu basi tutaongeza idadi kwa walimu kutoka Pemba. *(Makofi)*

Vile vile Mhe. Mohammed Haji Khalid alizungumza kuhusu matokeo ya Kidato cha *IV* na *VI* kuwa matokeo haya hayaridhishi. Mhe. Spika, ni kweli kwa mujibu wa matokeo ambayo tunayo bado hatujafikia pale Wizara ambapo tunataka tufike.

Hata hivyo, kwa wanafunzi wa Kidato cha *IV* wale wanaopata *Division Four* wapo na wanaendelea Kidato cha *V* Chuo cha Kilimo, Chuo cha Uongozi wa Fedha Chwaka, Chuo cha Afya na kadhalika na wala si sahihi kusema kwamba *Division Four* kuwa wamefeli.

Kwa hivyo, wizara inachukua hatua, ili kuhakikisha kama tunapasisha wanafunzi wengi wa *Form IV* na *VI*. Mhe. Spika, hatua tunazochukua ni kama vile ujenzi wa Skuli zetu hizi mpya za kisasa za Unguja na Pemba, kuongeza vifaa vya kufundishia na kujifunza pamoja na kuajiri walimu wapya.

Mhe. Salmin Awadh Salmin na Mhe. Hija Hassan Hija walitaka kujua kuhusu jina la Baraza la Upimaji na Tathmini ya Elimu. Mhe. Spika, sisi hatuna tatizo na jina la Baraza la Mitihani la Zanzibar na kama Waheshimiwa Wawakilishi wamechangia katika mswada wetu huu, Mhe. Waziri wetu aliyekuwepo kwa wakati ule alikubaliana kabisa na madai pamoja na matakwa ya Waheshimiwa Wawakilishi, kwamba sasa tuite Baraza la Mitihani la Zanzibar. Lakini Mhe. Spika, sheria hii ilipotoka kwa Mwanasheria Mkuu ililetwa kama Baraza la Upimaji na Tathmini ya Elimu. *(Makofi)*

Aidha Mhe. Salmin Awadh Salmin alitaka kujua umri wa wanafunzi wanaojiunga na Kidato cha V na kufanya Mtihani kwa *School Candidate* kwa Mitihani ya Kidato cha VI. Jibu mwanafunzi anatakiwa afikapo Kidato cha VI asizidi umri wa miaka 24. Agizo hilo lilitolewa na Baraza la Mitihani la Tanzania *NECTA* tarehe 02/04/2012 kwa barua yenye kumbukubu No. MT/E/16/19/V0L8/177.

Baraza la Upimaji na Tathmini ya Elimu, lililofanya ni kukumbusha agizo hilo kwa barua ya tarehe 08/05/2012 yenye kumbukumbu No. BTKE/MT/69/16. Agizo hilo tayari limeshapelekwa kwa Walimu Wakuu wote wa skuli zetu husika. Mhe. Spika, naomba kufahamisha kuwa kisheria

mwanafunzi anatakiwa kuanza Darasa la Kwanza akiwa na umri wa miaka 7, hivyo akitimia umri wa miaka 20 anatakiwa awe ameshamaliza Kidato cha VI.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, sauti zisipae, ili tuweze kumsikia Mhe. Naibu Waziri vizuri, kwa faida ya Wajumbe walioulizia hoja mbali mbali pamoja na Baraza kwa jumla. Mhe. Naibu Waziri endelea.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, nakushukuru. Akiwa miaka 24 na 25 anatakiwa tayari awe amemaliza Chuo Kikuu.

Vile vile Mhe. Mjumbe alitaka kujua kuhusu walimu waliotuhumiwa katika udanganyifu wa Mtihani wa *form* IV mwaka 2011 na wizara imechukua hatua gani? Mhe. Spika, Wizara imechukua hatua zifuatazo:-

1. Wasimamizi wote waliotuhumiwa wametakiwa kujieleza kwa barua, ambao ni 140 na hivi sasa tayari 95 wameshajieleza kama walivyotakiwa.
2. Walimu Wakuu wawili waliohusika na kadhia hii tayari wameshushwa vyeo na kuwa walimu wa kawaida.
3. Jeshi la Polisi limetakiwa kufanya uchunguzi wa kina kuhusu tatizo hili.
4. Hatua nyengine zitafuata baada ya uchambuzi kukamilika.
5. Katika mazungumzo yetu Wizara na *NECTA*, tumeamua kuanzia mwaka 2012/2013 mitihani yote kutoka Baraza la Mitihani *NECTA* itaratibiwa kwa karibu na Baraza la Upimaji na Tathmini ya Elimu Zanzibar.

Mhe. Fatma Mbarouk Said alikuwa na wasi wasi kuhusu uchakachuaji wa Mitihani ya Taifa kwa *Private Schools*. Mhe. Spika, ili kuepusha udanganyifu huu Wizara inachukua hatua zifuatazo. Kuhakikisha kuwa Walimu wa *Private* hawasimamii *Private Schools* nyengine, na wale wenye dhamana ya kusimamia mitihani hiyo, huzitembelea *Private Schools* mara kwa mara, ili kuona usahihi wa ufanyaji wa mitihani hiyo.

Mhe. Abdalla Moh'd Ali aliuliza kuhusu vipawa vya juu. Mhe. Spika, vipawa vya juu ni wale wenye uwezo mkubwa katika masomo yao na hawa hupatikana kwa kuangaliwa uwezo wao katika kujibu mitihani. Vile vile ni kweli kuwa wanafunzi wengi hutoka katika skuli moja, lakini zipo skuli hutoa kati ya wanafunzi 10 hadi 40, hii inatokana na matayarisho yao pamoja na juhudi zao binafsi.

Kwa mfano, Skuli ya Kisiwandui Unguja jumla ya wanafunzi walikuwa 259, waliofaulu ni 12 sawa na asilimia 4.6. Skuli ya Chumbuni wanafunzi walikuwa 244, waliopasi ni 33 sawa na asilimia 13.5. Skuli ya Mtopepo wanafunzi walikuwa ni 274, waliopasi ni 26 sawa na asilimia 9.5. Skuli ya Bububu A wanafunzi wote walikuwa 273, waliopasi ni 32 sawa na asilimia 11.7. *(Makofi)*

Kwa upande wa Pemba Skuli ya Jadida jumla ya wanafunzi walikuwa ni 244, waliofaulu ni 34 sawa na asilimia 13.9. Skuli ya Kizimbani wanafunzi walikuwa ni 156, waliofaulu ni 30 sawa na asilimia 19.2. Skuli ya Mitiulaya wanafunzi walikuwa ni 184, waliofaulu ni 44 sawa na asilimia

23.4. Skuli ya Ng'ombeni 'A' wanafunzi walikuwa ni 124, waliopasi ni 14 sawa na asilimia 11.3. *(Makofi)*

Mhe. Hassan Hamad Omar, alitaka kujua kwamba *NECTA* kuna watendaji wangapi kutoka Zanzibar. Mhe. Spika, kuna mtendaji mmoja kutoka Zanzibar na Baraza la *NECTA* lina wajumbe wanne.

Mhe. Spika, Kitengo cha Urajisi wa Elimu Pemba, Mhe. Abdalla Ali Moh'd alisema kwamba kitengo kiimarishwe. Kwa kweli hali ya ofisi sio mbaya sana isipokuwa inahitaji matengenezo madogo madogo. Ofisi ina watendaji wawili wanaume na mwanamke, na hata hivyo wizara imejipanga kuongeza wafanyakazi wakiwemo Mwanasheria pamoja na vifaa vya kutendea kazi.

Vile vile Mhe. Mjumbe alitaka kujua kuhusu mwalimu wa Skuli ya Tumbe aliyetuhumiwa kumpa mwanafunzi ujauzito na baadaye mwalimu huyo kurejeshwa kazini. Mhe. Spika, kesi hii iliripotiwa Wizara ya Elimu, hata hivyo, tumepata barua kutoka kwa mlalamikaji, kwamba baada ya kufanya uchunguzi mlalamikaji aligundua kuwa dai lake halikuwa sahihi na kwamba mwalimu aliyetajwa alikuwa hahusiki.

Kwa kuwa kesi hii imeripotiwa kwa Mkuu wa Kituo cha Polisi Konde, basi Wizara inaamini kwamba kosa likithibitika sheria zitachukuliwa, barua ya tarehe 16/06/2011 ya mlalamikaji ilieleza. Kwa upande wa mwanafunzi Wizara itatoa fursa ya mwanafunzi kurudi baada ya kujifungua, ili aendelee na masomo.

Mhe. Spika, ninano *copy* ya mlalamikaji ambaye ni mama mzazi, kesi hii kuipeleka katika Kituo cha Polisi cha Konde, Mhe. Mjumbe akiihitaji basi nitampatia ili aweze kupata maelezo zaidi kuhusiana na hili.

Mhe. Fatma Mbarouk Said, alitaka kujua juu ya ufuatiliaji wa *Private Schools* kuhusu hali ya ufanisi. Mhe. Spika, hali ya ufanisi katika *Private Schools* ni ya kuridhisha, kama vile idadi ya *private schools* inaongezeka hadi kufikia mwaka 2012 kiasi cha skuli 352 zimesajiliwa. Aidha *private schools* zimeweza kusaidia Wizara ya Elimu kwa kuchukua wanafunzi wengi. Pia zipo baadhi ya skuli ambazo hufanya vizuri katika mitihani yao ya Kidato cha IV na VI.

Kwa upande wa ufuatiliaji, Wizara imetunga Kanuni ya Usajili wa Skuli Zisizo za Kiserikali ya mwaka 1998, ambapo utaratibu wake umeelezwa katika kanuni hizo. Vile vile Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Wizara hufanya ukaguzi.

Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak, alitaka kujua kwa nini wanafunzi wanaofunga ndoa wanafukuzwa skuli, lakini waliopata ujauzito wanaendelea na masomo. Mhe. Spika, utaratibu huu ni kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Nam. 6 ya mwaka 1982 kifungu cha 20(3) ambacho kinamtaka mwanafunzi asioe wala asiolewe. Kwa hiyo, kufanya hivyo kunapelekea mwanafunzi huyo kufukuzwa skuli.

Mhe. Spika, Sheria ya Kuwalinda Wari na Watoto wa Mzazi Mmoja Nam. 4 ya mwaka 2005 kifungu cha 4(2) na (3) kinamruhusu mwanafunzi anayebeba ujauzito akiwa hajamaliza elimu

yake ya lazima, basi aendelee na masomo. Lengo na madhumuni makubwa ya sheria hii ni kulinda wari pamoja na kutekeleza Mikataba ya Kimataifa juu ya Haki ya Mtoto.

Vile vile Mhe. Mjumbe aliuliza wakaguzi wanne walioteuliwa na kupewa mafunzo ya ukaguzi, je wakaguzi hao walitoka wapi? Je, wakaguzi hao walikuwa ni wa masomo ya Kiingereza? Mhe. Spika, wakaguzi hao walitoka katika skuli zetu hapa nchini wakiwemo watano kutoka Unguja na watatu kutoka Pemba. Kati ya wakaguzi hao hakukuwa na wa somo la Kiingereza, kwa sababu haikuwepo haja ya wakaguzi wapya wa somo hilo, kwa vile hali iliyokuwepo kwa wakati huo ilikuwa inatosheleza.

Mhe. Spika, Elimu Mjumuisho na hoja hii alizungumza Mhe. Mjumbe pia, na alionesha wasi wasi mkubwa juu ya Elimu Mjumuisho na kwamba haiwezi kuleta manufaa kwa wanafunzi wenye ulemavu katika darasa moja na wanafunzi wengine.

Mhe. Spika, napenda kumhakikishia Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak kuwa mfumo wa Elimu Mjumuisho ndio mfumo pekee unaoweza kukidhi mahitaji ya kila mwanafunzi na kuwezesha kujifunza na kujibu kwa uwezo wake ikiwa pamoja na wanafunzi wenzake katika skuli hiyo.

Skuli iliyo karibu na mahala anapoishi. Kwa kweli mfumo huu umeleta faraja kubwa na kuondoa unyanyasaji, utengaji, unyanyapaa kwa wanafunzi wengine wenye mahitaji maalum, na badala yake unajenga heshima na urafiki miongoni mwa wanafunzi wote.

Mhe. Spika, hapa Zanzibar mfumo huu umelijengea sifa taifa na heshima kubwa, ambapo nchi mbali mbali za Afrika, Ulaya na Marekani zinakuja kujionea wenyewe hali halisi badala ya kusikia tu, mada mbali mbali za utekelezaji wa Elimu Mjumuisho zinazotolewa katika mikutano au kusoma ripoti za utekelezaji wa masomo katika taarifa za mitandao. *(Makofi)*

Wanafunzi wenye mahitaji mbali mbali ya kielimu wakiwemo wenye ulemavu tofauti, wanaendelea kufanya vizuri katika masomo yao. Kwa mfano, mwanafunzi asiyeona anaendelea na masomo yake katika Chuo Kikuu cha Tunguu katika Fani ya Sheria, na wanafunzi wawili viziwi pia wanaendelea na masomo yao katika Chuo cha Tunguu katika Fani ya Sheria na *Public Administration*. *(Makofi)*

Aidha wanafunzi wawili wasioona kutoka Skuli ya Kisiwandui wamefaulu Michipuo mwaka 2011 na kuingia Skuli ya Vikokotoni ambapo wanaendelea kuchukua nafasi ya kwanza na ya pili katika Darasa la Mjumuisho. (*Makofi*)

Mhe. Spika, sasa niende kwa Mhe. Ismail Jussa Ladhu alitaja kujua sababu gani iliyopelekea Wizara ya Elimu kuhamisha walimu Skuli ya Haile-Selassie. Hali hii Mhe. Spika, inatokana na ukaguzi uliofanywa na Maafisa wetu wa Idara, na kuonekana kuwa ziada ya walimu waliokuwepo walikuwa wakisomesha vipindi 8, 10 hadi 12 kinyume na utaratibu wa skuli zetu kiuwiano, ambapo walimu watatu wawe wanasomesha madarasa mawili na idadi ya vipindi angalau 18.

Mhe. Spika, wewe utakuwa ni shahidi hapa, Waheshimiwa Wawakilishi, Mhe. Salmin Awadh Salmin aliwahi kuhoji kuwa skuli nyingi hususan za Ng’ambo hazina walimu, lakini walimu hao

wanarundikana katika skuli za mjini. Mimi nilimjibu Mhe. Salmin Awadh Salmin kuwa suala hilo ni kweli na kama Wizara tumeliona na tunalifanyia kazi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, sio kwa Skuli ya Haile-Sela-ssie na skuli nyengine nyingi tu za mjini tunazifanyia ukaguzi huu, na tutawahamisha na tutaendelea kuwahamisha, kwa sababu tunalo tatizo kubwa la walimu na kwamba hawatoshi, lakini walimu wanarundikana katika skuli moja na wala haileti maslahi.

Vile vile Mhe. Mjumbe, alitaka kujua kuna mwalimu mmoja wa Skuli ya Biashara ambaye amehamishiwa katika Skuli ya Jang'ombe pamoja na walimu wengine kutoka Skuli hiyo ya Biashara na kwenda skuli nyengine kutokana na kuwepo walimu wengi wenye fani hiyo katika Skuli hiyo ya Biashara, ambapo walimu kama nilivyosema hii kesi ya mwanzo, kwamba anasomesha vipindi 8 au 10 tu, wakati mwalimu mmoja anatakiwa asomeshe takriban vipindi 18.

Kwa hivyo, walimu hawa tumewaondoa katika Skuli ya Biashara na kuwapeleka skuli nyengine ambazo tuna upungufu wa walimu, na walimu hao wanasomesha masomo ambayo walikuwa wakisomesha kabla hawajenda kusomea elimu hii ya biashara.

Mhe. Omar Ali Shehe, alitaka kujua kuhusu kutenganisha fedha za vifaa za maabara na fedha za kufundishia. Mhe. Spika, ukweli ni kuwa mwaka huu wa fedha Idara ya Sekondari imetenga jumla ya shilingi milioni 99,000,000/= kifungu 220516. Vifaa vya kusomeshea ambapo matumizi yake ni ununuzi wa vifaa vya maabara kwa skuli zetu za Sekondari za Unguja na Pemba.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis, alizungumzia kuhusu uhamisho wa wanafunzi kutoka Pemba inakuwa ni vigumu. Mhe. Spika, ukweli ni kuwa wanafunzi wote wanaoomba uhamisho, lazima uhamisho huo uombwe kwa wazazi wao na huwa unatolewa.

Ushahidi unaonesha kwamba katika mwaka 2011/2012 wanafunzi 90 wa Skuli za Sekondari wamepatiwa uhamisho kuja kusoma Skuli za Unguja. Mhe. Spika, naomba kumuarifu Mhe. Mjumbe kwamba orodha hiyo ninayo na akiihitaji kwa ajili ya maelezo zaidi, basi nitampatia. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Waheshimiwa Wawakilishi wengi walizungumza kuhusu habari ya *tuition* na walionesha *concern* yao juu ya *tuition* hizi zinavyoendesha vitendo vya utovu wa nidhamu, yaani tunavuna mabaya zaidi kuliko manufaa ambayo yanayopatikana katika *tuition* hizo. (*Makofi*)

Mhe. Spika, *tuition* zipo kisheria na zinasimamiwa na Idara ya Watu Wazima, ambapo zimeandaa taratibu za kusajili idadi ya wanafunzi na muda. Hivyo, wizara kutokana na hali ambayo si ya kuridhisha ya utendaji wa *tuition* hizo, imeamua kusitisha tuition zote katika majengo yetu ya skuli zetu zote hadi hapo utaratibu wa uendeshaji wa *tuition* utakapokuwa tayari na kuweka utaratibu mzuri kama Sheria ya Elimu ilivyoeleza. Kwa sasa kwa zile skuli ambazo zimeanzisha kambi ya masomo katika skuli zao, basi lazima Kamati za Skuli zihusike kuhakikisha kama Kambi hizo zinafanya kazi kwa mujibu wa sheria ambavyo inataka.

Mhe. Spika, Idara ya Uendeshaji na Utumishi, hoja mbali mbali za Waheshimiwa wa Baraza la Wawakilishi ziliulizwa katika idara hii. Mhe. Nassor Ali Salim alitoa ushauri kuhusu skuli na majengo ya serikali kupatiwa Hati Miliki, na kutaka serikali iandae utaratibu maalum wa upatikanaji wa Hati Miliki. Mhe. Spika, ushauri huu tunauchukua na tutaufanyia kazi. *(Makofi)*

Mhe. Ali Salum Haji na Mhe. Omar Ali Shehe, wao hawa walihoji kuhusu kifungu cha safari za ndani na kile cha safari za nje kuwa ni kikubwa ukilinganisha na mwaka jana na kwa nini ikawa hivi?

Mhe. Spika, sababu moja ni kuwa Walimu Wakuu, Walimu wa Kawaida, Wenyeviti wa Kamati za Skuli, Maafisa Elimu wamehamasika kufanya ziara katika skuli mbali mbali za Tanzania Bara kwa ajili ya kwenda kujifunza njia mbali mbali za kukuza elimu. Kwa mfano, mwaka uliopita zaidi ya Walimu Wakuu, Maafisa Elimu na Wenyeviti wa Kamati za Skuli 147 walitembelea Tanzania Bara baada ya kupata wilaya rafiki.

Vile vile baadhi ya skuli tayari zimeanzisha mahusiano ya nje katika Uhusiano unaoitwa Skuli Rafiki. Kwa mfano mwaka wa fedha 2011 walimu 22 kutoka skuli mbali mbali za Unguja na Pemba, Mratibu mmoja wa Kituo cha Walimu Bububu walikwenda nchi za nje kwa ajili ya kujifunza katika ziara maalum.

Pia Maafisa wa Elimu mbali mbali, walimu kutoka Unguja na Pemba, walimu 32 walipata fursa ya kwenda nchini India na China kwa mafunzo mafupi, hawa wote wanagharamiwa kwa posho na *VISA* katika fungu hilo. Kwa hivyo, mwaka huu tunategemea sana kutafanyika safari kwa Walimu Wakuu wengi zaidi.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, alikuwa na hoja tatu. Kwanza alitaka kujua ni kwa nini baadhi ya waajiriwa wapya wa mwezi wa Aprili, 2012 walilipwa nusu mshahara licha ya kujaza Mkataba wa Ajira tarehe za awali ya mwezi. Mhe. Spika, ni kweli baadhi ya waajiriwa wapya walilipwa nusu mshahara baada ya kuripoti vituoni zaidi ya tarehe 16 katika mwezi huo, kwa maana hiyo hawakukamilisha mwezi katika kufanya kazi.

Hata hivyo, Wizara imeliona tatizo hili na kuwasiliana na Wizara ya Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa ushauri zaidi juu ya namna ya kutatua tatizo hilo. Mhe. Spika, ushauri tuliopata ni kuwa waajiriwa hawa walipwe kwa mujibu wa tarehe zao za mikataba. Wizara yangu itatekeleza agizo hili.

Vile vile Mhe. Mjumbe alitaka kujua kwa nini fedha za likizo hazilipwi na alikuwa na hofu kwamba zinalipwa kwa upendeleo. Mhe. Spika, utaratibu wa kwenda likizo ni kuwa kila anayestahiki kwenda likizo aende likizo, kwa sababu likizo ni haki ya mfanyakazi na stahiki kwa anayekwenda likizo hutolewa kila baada ya miaka mitatu.

Kwa mfano, Wizara yangu imeshalipa posho za likizo wafanyakazi 689 sawa na shilingi 68,009,000/= na kubakisha wafanyakazi 2194 ambao wanahitaji jumla ya shilingi 219,400,000/=. Kwa upande wa Unguja na Pemba ni wafanyakazi 105 ndio waliolipwa na wafanyakazi ambao bado hawajalipwa ni 1101. *(Makofi)*

Mhe. Spika, katika mwaka huu wa fedha wizara yangu imetenga jumla ya shilingi milioni 352,000,000/= kwa ajili ya kulipa fedha za likizo kwa wafanyakazi, na tutaanza wale wote wanaostahiki kulipwa kwa mwaka 2011. Kwa hivyo, napenda kumhakikishia Mhe. Mjumbe kwamba fedha za posho hazitolewi kwa upendeleo, isipokuwa namuomba afahamu kuwa idadi ya wafanyakazi wanaohitaji kulipwa ni wengi na hivyo huchukua muda mrefu kulipa.

Vile vile Mhe. Mjumbe alitaka kufahamu ajira kwa wahitimu wa Mafunzo ya Ualimu ngazi ya cheti na kuitaka wizara ifikirie upya kuhusu vijana hawa ili wapate fursa ya kuajiriwa. Mhe. Spika, hoja hii pia ilizungumzwa na Mhe. Abdalla Moh'd Ali, wizara yangu inawahitaji sana wahitimu wa ngazi ya cheti, kwani bado ziko skuli ambazo zinahitaji walimu wa aina hii kwa upande wa msingi. Pia walimu wa aina hii wanahitajika kusomesha katika madarasa ya maandalizi.

Mhe. Spika, hivi sasa tayari wizara yangu imeshawasilisha maombi ya nafasi ya kuajiriwa kwa walimu wa aina hii katika Wizara ya Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mazingatio zaidi. *(Makofi)*

Mhe. Hamza Hassan Hamad, alitaka kujua. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Naibu Waziri, ni Mhe. Hamza Hassan Juma.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, samahani hoja ni nyingi mpaka zinanitia kizunguzungu. *(Makofi)*

Mhe. Hamza Hassan Juma, alitaka kujua kwa nini vijana hao pamoja na walimu wanaojitolea hawaajiriwi. Ni kweli baadhi ya skuli huwa na utaratibu wa kuwa na walimu wanaojitolea baada ya Uongozi wa Kamati ya Skuli kukabiliana na walimu hao, mara nyingi walimu hawa hupata sabuni tu wakati wakisubiri ajira.

Kwa utaratibu wa sasa wale wanaotaka ajira wanatakiwa kupeleka maombi yao ya kazi katika Tume ya Utumishi Serikalini na hatua hufuatwa. Kwa kweli Wizara haina mamlaka ya kutangaza kazi wala kuajiri bila ya kibali kutoka Tume ya Utumishi Serikalini. Kwa hivyo, tunamuomba Mhe. Mjumbe awashauri vijana hawa wanaojitolea kupeleka maombi yao ya kazi katika tume hii, pindipo wakisikia matangazo ya kazi yanatoka.

Mhe. Saleh Nassor Juma, alitaka kujua kwamba vijana wanaotaka kuajiriwa hadi leo bado hawajakamilisha taratibu za ajira, licha ya kuwa Tume ya Utumishi Serikalini imeshatoa kibali cha kuajiriwa. Mhe. Spika, wizara yangu kabla ya kuajiri vijana wapya hufanya uhakiki wa taarifa zao hasa wa vyeti vyao, ili iwe rahisi kuingiza katika *data base* ya wizara.

Kwa hivyo, wizara yangu inafanya uhakiki wa vyeti vya wahitimu, na wahitimu 23 wa ngazi ya shahada waliomba Kazi ya Ualimu, ili kufahamu uhalali wa vyeti vyao kabla ya hatua ya kuajiri, kwa upande wa shahada wote tayari wameshaajiriwa.

Mhe. Spika, naahidi kuwa wale wote ambao vyeti vyao havitakuwa na mashaka, basi wataendelea na taratibu za ajira, na wale ambao vyeti vyao vitagunduliwa kuwa si sahihi na wala sio halali hawataruhusiwa na tutawarudisha Tume ya Utumishi Serikalini kwa hatua zaidi.

Vile vile Mhe. Mjumbe alitaka kujua ni lini wahitimu wa *Program* ya *TAP* watarekebishiwa mishahara yao baada ya wahitimu hawa kuhitimu. Mhe. Spika, Wizara yangu kwa sasa inashughulikia suala hili na hatua iliyofikia ni kuhakiki taarifa za wahitimu hawa na baadaye kupeleka katika Wizara ya Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa hatua zaidi. Kwa hivyo, napenda kumhakikishia Mhe. Mjumbe kwamba suala hili tunalimaliza si muda mrefu.

Mhe. Rashid Seif Suleiman, yeye hakupendezwa hata kidogo na suala la kuchukuliwa walimu wa kujitolea kutoka Nigeria na kutoa rai kuwa, basi ni vyema tukachukua walimu wa *science* na Hesabati walimu ambao wamestaafu. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Mjumbe, akumbuke kwamba miaka ya 1970 na 1980 hapa Zanzibar kulikuwa na walimu kutoka Misri, India, Nepal, Nigeria na wengi walitoka katika Shirika la Kujitolea la Uingereza na Marekani, hawa wote walikuja Zanzibar kwa ajili ya kuja kusomesha vijana wetu, wengi wetu tupo hapa sasa tunafaidika na walimu wa aina hii.

Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Mjumbe, akubaliane na maamuzi haya akizingatia kuwa ni ushauri wa Mhe. Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi la Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein, kwamba tutafute walimu wa *science* na hesabati popote pale duniani. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hoja ya marekebisho ya mishahara ya wafanyakazi hususan walimu kwa nini hawakupewa taarifa ya marekebisho haya, na hii pia ilikuwa ni hoja ya Mhe. Mjumbe. Ni kweli kuwa baadhi ya wafanyakazi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali hasa walimu waliofanyiwa marekebisho tokea kuwepo kwa mabadiliko ya mishahara ya wafanyakazi wote serikalini Oktoba, 2011.

Wizara yangu imekuwa ikichukua hatua mbali mbali, ili walimu wapate taarifa za marekebisho. Kwa mfano, Maafisa wanaohusika na mishahara pamoja na Mkurugenzi wa Uendeshaji na Utumishi, alifanya mikutano na Walimu Wakuu kueleza utaratibu wa marekebisho haya na hatua ambazo mwalimu achukue ikiwa ataona mshahara wake umepungua au kuongezeka.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, tunaanza kutomsikia vizuri Mhe. Naibu Waziri kwa sababu ya ghasia kidogo zinapanda. Kwa hivyo, naomba tuwe watulivu, ili Mhe. Naibu Waziri amalize na baadae tumuombe Mhe. Waziri kwa ajili ya kukamilisha.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, nakaribia kumaliza.

Mhe. Spika, nina imani kuwa taarifa hizi ziliwafikia walimu. Pia walimu wote ambao hawakuridhika na mabadiliko haya walifika katika Vituo vya Elimu kwa ajili ya kuonana na Maafisa husika, ili kujua mshahara wake kamili baada ya wao kuwasilisha vyeti vyao.

Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak, alitaka kujua sababu za walimu wa Skuli ya Potoa kusimamishwa kazi hivi karibuni. Mhe. Spika, ni kweli kuwa walimu watatu wa Skuli ya Potoa walisimamishwa

kazi, wawili ni kutoka Skuli ya Potoa na wengine ni Skuli ya Potoa Msingi. Sababu hasa kusimamishwa kazi walikuwa wakichochea wanafunzi kukataa Muungano wakati wakiwa skuli. Wizara ilipata taarifa hii na kumtuma Afisa wa Elimu Mkoa ili kuchunguza ukweli wa jambo hili na kugundua kuwa walihusika na kadhia hii. Wanafunzi waliwataja walimu hao watatu majina yao tunayo tumeyahifadhi. Hivyo Wizara iliwasimamisha kazi na waliacha kufanya kazi.

Hii ni kinyume na Sheria ya Utumishi Mhe. Spika, ya Nambari 2 ya mwaka 2011 katika kifungu cha 82(i) (a), walimu hawa wamepewa fursa ya kujieleza. Wizara ilipokea maelezo yao na kuthibitisha maamuzi na Wizara iliamua kuwarudisha kazini kwa kuwapa onyo la maandishi. Hivyo kwa sasa walimu hawa tayari wapo kazini. Naomba kutoa wito kwa walimu kutojiingiza katika mambo ambayo yanavunja maadili yetu.

Mhe. Naomba nimalizie kwa hoja ya Mhe. Salmin Awadh, Mhe. Rufai, Mhe. Ismail Jussa, Mhe. Hija Hassan, Mhe. Asha Bakari, Mhe. Salma Mohammed. Waheshimiwa hawa wote wamezungumzia maslahi ya walimu hasa posho kwa walimu wakuu kuwa ni ndogo sana hailingani na dhamana ambazo wamepewa.

Mhe. Spika, nataka nikiri kwamba ni kweli na Wizara yangu imeliona hilo na tayari nimemalizia waraka wa mapendekezo ya kuongezwa kwa posho ya walimu wakuu. Ili kuwasilisha Afisi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa idhini. Wizara yangu kwa hatua ya mwanzo ya Mwaka wa Fedha 2011/2012 Naibu Katibu wangu na watendaji wa Idara ya Utumishi walikutana na Mhe. Waziri wa Afisi ya Utumishi na Utawala Bora na watendaji wake kuona uhalisia wa posho zinazolipwa katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya amali na namna ya kuziboresha ikiwemo posho za walimu wakuu.

Mhe. Spika, nachukua nafasi hii kuwashukuru kwa dhati Mhe. Waziri, Afisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mashirikiano yake anayotupa pamoja na watendaji wake. Naomba Mhe. Waziri punde tu tukimaliza bajeti hii tunaomba kikao kujadili posho za walimu wakuu.
Mhe. Spika, namalizia kwa kuunga mkono hoja na kuwaomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu kuwa waunge mkono Bajeti na watupitishie Bajeti yetu. Wizara yetu ni sikivu, Waziri, watendaji, na mimi Naibu Waziri, naahidi kuyachukua yote yale ambayo wametuonesha wenzetu na hii ni changamoto kwetu Mhe. Spika, kama tulikuwa tukenda, sasa tutakwenda mbio zaidi, kama tulikuwa tukiwatizama watendaji wetu kwa jicho moja sasa tutawatizama kwa macho mawili.

Pia kuhakikisha dhamira ya nchi yetu, dhamira ya Wizara ya Elimu, dhamira ya wananchi wote na wajumbe wa Baraza lako tukufu, wanafunzi wetu kupata elimu bora, elimu ambayo itawasaidia wao na itaendesha maendeleo mbele kwa maslahi ya nchi yetu.

Mhe. Spika, kama walivyozungumza Waheshimiwa wa Baraza lako tukufu bila ya elimu ambayo ni elimu nzuri na elimu madhubuti nchi haiwezi kwenda. Naomba sana Waheshimiwa waipitishe bajeti hii na naunga mkono hoja.

Mhe. Spika: Nakushukuru Mhe. Naibu Waziri na ndivyo hasa utaratibu na nidhamu katika vyombo hivi vya kutunga sheria unafanya *lobbing* ya hali ya juu kama alivyosema Mhe. Naibu

Waziri, hiyo ndio hasa utaratibu. Utaratibu huu maana yake umewathamini sana wajumbe hawa hiyo ndiyo maana yake.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, na mimi nianze kukushukuru binafsi kwa kunipa nafasi hii kuja mbele ya Baraza lako tukufu kutoa majumuisho ya bajeti ambayo tuliisoma juzi.

Mhe. Spika, hata kabla ya kueleza utangulizi wangu nataka nimshukuru sana bila ya kiasi Naibu Waziri wangu kwa kazi nzuri sana aliyoifanya ya kunisaidia. Nina hakika nimefanya hivyo kwamba mimi ni mwanafunzi wake katika Wizara hii. Wizara kubwa, wizara muhimu, wizara ina mambo mengi, mimi bado ni mgeni katika Wizara pamoja na juhudi zote alizozichukua na amefanya hivi kwa kujua hayo. Mhe. Naibu Waziri, nakushukuru sana.

Mhe. Spika, kama alivyowahi kusema Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Majenzi na Nishati alipokuwa anafunga hotuba yake ya bajeti, mimi nataka kutoa tamko hilo wakati nafungua hotuba yangu ya bajeti nalo ni kwamba nawaomba Waheshimiwa wote waiunge mkono bajeti hii. Ili wanipe nafasi sasa baada ya kuipitisha hii bajeti ya kujidhatiti na kutekeleza yale ambayo nimeyaandika ili kuikuza elimu yetu na kuwatunza walimu wetu, walimu wakuu, walimu wasaidizi na walimu wetu wote wengine ili tupate mafanikio.

Mhe. Spika, sasa naomba nikushukuru kwa mara nyengine tena kwa kunipa nafasi kutoa majibu ya Waheshimiwa Wawakilishi waliochangia katika hotuba ya bajeti ya Wizara yangu iliyowasilishwa tarehe 18/07/2012. Kabla yakutoa ufafanuzi katika michango iliyowasilishwa na Waheshimiwa mbali mbali na mimi napenda kama alivyonisahihisha Mhe. Hamza Hassan Juma, kutoa mkono rambi rambi kwa wenzetu waliotangulia mbele ya haki kutokana na kuzama kwa meli. Nawaomba jamaa na marafiki walioachwa nyuma na wahanga hawa Mwenyezi Mungu awape moyo wa subra, uvumilivu na hatimaye kusahau kwa yaliyotokea. Na sisi sasa Serikali tumejidhatiti kuziondosha kasoro hizi kama wananchi wanavyotutaka tufanye.

Nawaomba wananchi wawe na subra *Inshallah* Mwenyezi Mungu atatupa uwezo wa kuyakamilisha Matakwa yao. Na matakwa ya wananchi ni kwa sisi Serikali kununua meli mpya, dhamira tunayo, niya tunayo, tunakosa uwezo na Ishallah mwenyezi Mungu atatujaalia atupe uwezo ili tununue hiyo meli mpya na tusalimike na majanga haya.

Katika chombo hichi kilichozama walikuwemo wanafunzi wetu, vijana wetu 10 ambao walikuwa wanarejea nyumbani kwa mapumziko kutoka Chuo Kikuu cha Kiislamu Morogoro hadi sasa wenzetu hawa bado hatujawaona. Mwenyezi Mungu awape subra wale wote waliopotelewa na ndugu zao na jamaa zao na aziweke roho mahali peme Peponi wenzetu hawa waliotangulia mbele ya haki.

Mhe. Spika, kwa kuanzia napenda niwapongeze wale wote waliochangia hotuba yangu, waliochangia kwa kusema na waliochangia kwa maandishi. Nataka niwahakikishie nimewasikiliza vizuri sana, nimejifunza kutoka kwao mambo mengi sana na *Inshallah* Mwenyezi Mungu atatupa uwezo wa kuyatekeleza wale waliyotushauri na kuendelea kujifunza zaidi ili tukamilishe mambo ambayo tumetumwa tuyafanye.

Mhe. Spika, naomba niwataje ili kuonesha thamani yangu kwao wale waliochangia.

1) Mhe. Nassor Salim Ali
2) Mhe. Ali Salim Haji
3) Mhe. Mohammed Haji Khalid
4) Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
5) Mhe. Seif Suleiman
6) Mhe. Mtumwa Kheri Mbarouk
7) Mhe. Salmin Awadh Salmin
8) Mhe. Fatma Mbarouk Said
9) Mhe. Aballah Mohammed Ali
10) Mhe. Asha Bakari Makame
11) Mhe. Omar Ali Shehe
12) Mhe. Hija Hassan Hija
13) Mhe. Hamad Hassan Omar
14) Mhe. Ismail Jussa Ladhu
15) Mhe. Saleh Nassor Juma
16) Mhe. Rufai Said Rufai
17) Mhe. Suleiman Hemed Khamis
18) Mhe. Hamza Hassan Juma

Mhe. Spika, wajumbe waliochangia hoja hii kwa maandishi ni

1) Mhe. Abdalla Juma Abdalla
2) Mhe. Shadya Mohammed
3) Mhe. Hassan Juma
4) Mhe. Salma Mohammed Ali
5) Mhe. Nassor Juma
6) Mhe. Saleh Nassor Juma

Mhe. Saleh Nassor Juma amechangia tena kwa maandishi na ameniomba sana nipokee maandishi yake aliyoniletea tarehe 20/7/2012 ili wananchi wake wanisikie. Mheshimiwa kwa ruhusa yako nakubali kufanya hivyo.

Baada ya utangulizi huo naomba nitoe maelezo kuhusu. Mhe. Spika, samahani, leo asubuhi nilipata maandishi ya michango ya Waheshimiwa watatu, sina hakika kama hayo yamepita na wakati au bado yanatekelezeka. Mimi kwa ruhusa yako nitayatolea ufafanuzi kwa yale ambayo takwimu zake ninazo. Maana mengine yamekuja na hoja nyingi sana za kitakwimu. Hayo nadhani itabidi wanisamehe nitayatolea ufafanuzi kwa maandishi na maandishi hayo nitayaleta Barazani hapa ili wajumbe wayajue.

Mhe. Nassor Ali Salim, Makamo mwenyekiti wa Kamati hii amepongeza hotuba lakini hatimaye akatoa maoni mawili yake binafsi. Alitushauri skuli na majengo ya serikali kupatiwa hati miliki,

ili kuwe na utaratibu na msimamo kamili wa kisheria. Nakubaliana na hoja hiyo nitashirikiana na Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati, kulitekeleza ombi hilo.

Mhe. Ali Salum na Mhe. Omar Ali Shehe, hawa wote walihoji kuhusu vifungu vya safari za ndani na nje, kwa nini vimekuwa vikubwa n.k. Swali hili Mhe. Naibu Waziri wangu amelijibu, amelitolea ufafanuzi. Lakini pia nikubaliane na hoja aliyoitoa leo asubuhi katika maswali na majibu Mhe. Ismail Jussa. Kwamba kasoro za vifungu vya Bajeti ni nyingi na zimo takriban katika kila Wizara.

Pia alimuomba Waziri wa Nchi, Fedha, Uchumi na Maendeleo kwamba hatimaye avipitie tena hivi vifungu, afanye marekebisho kwa vile ambavyo vimezidi ili hatimaye aweze kutoa ruhusa kwa vifungu ambavyo vinastahiki kutolewa ruhusa. Mimi nakubaliana na hoja ya Mhe. Ismail Jussa, kama mwenyewe Waziri alivyoipokea, hiyo nadhani itanirahisishia kutoa ufafanuzi wa maswali chungumzima yaliyoulizwa. Lakini kama kuna haja ya kutoa ufafanuzi kwa yale ambayo ya ziada nitayatolea ufafanuzi.

Mhe. Ali Salim na Mhe. Omar Ali Shehe, walizungumzia walimu wakuu na walimu wengine kuhusu mishahara yao, maposho yao na kadhalika. Maswali haya Mhe. Naibu Waziri ameyazungumza vya kutosha kwa kuokoa wakati nakubaliana na mawazo aliyotoa Mhe. Naibu Waziri nataka niseme kwamba matatizo ya maposho, matatizo ya mishahara, matatizo ya nyongeza, matatizo ya likizo, fedha za likizo na kadhalika. Fedha za likizo na kadhalika yapo kwa muda mrefu na ni makubwa.

Nataka nitoe ahadi katika bajeti yetu ya mwaka huu, tumetenga fedha sio za kutosha lakini nyingi kidogo. Tumedhamiria wale wote wanaotudai likizo, wanaotudai maposho, wanaotudai mambo mengine na hizi nyongeza nitazungumza na Waziri Afisi ya Rais, muhusika, tukae tuzungumze nyongeza za mishahara za walimu wetu ili hatimaye walimu wapate kujisikia. Ni kweli kabisa walimu wanapata pesa kidogo nyongeza zao zinachelewa. Hilo nataka nitoe ahadi kwamba nitazungumza na mwenzangu ili tulirekebishe.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk nina hakika ameridhika na majibu aliyotoa Naibu Waziri. Naunga mkono majibu yale na naahidi zile kasoro ambazo alizitaja nazo pia tutazizingatia na tutaziondosha. Kwa mfano alitaka kujua kwa nini fedha za likizo hazilipwi kwa wakati. Kama nilivyosema hilo tutalirekebisha ni tatizo la muda mrefu na nikiahidi mieahidi, nitalisimamia mwenyewe kidete kuliondosha.

Wizara yangu tayari imeshawalipa posho la likizo wafanyakazi yaani walimu na wengineo, jumla ya shilingi 69 milioni na kubakisha wafanyakazi 2149 ambao watahitaji jumla ya shilingi elfu mbili mia moja na arubaini na tisa ambao watahitaji jumla ya shilingi mia mbili na kumi na tisa laki nne milioni Unguja na Pemba. Hawa tutawahudumia haraka ipasavyo. Katika mwaka huu wa fedha Wizara yangu imetenga shilingi mia tatu na hamsini na mbili milioni katika fedha za likizo kwa wafanyakazi na tutaanzia kwa wale wote wanaostahiki kulipwa kwa mwaka 2011.

Mhe. Makame Mshimba alitaka kufahamu ajira kwa wahitimu wa mafunzo ya elimu ngazi ya cheti na akakasisitiza kwamba hawa tuwasaidie ili wapate ajira. Nataka niseme hatujawakataa wala hatujawatupa moja kwa moja walimu waliohitimu ngazi ya cheti. Tumeshazungumza na

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Mma na Utawala Bora kwa kulizingatia hilo. Baada ya Bajeti hii huenda tukaajiri walimu wa vyetii. Sitaki nitoe idadi kwa sababu *hansard* iko wazi inaweza ikaninukuu lakini tutaajiri wengi kidogo. Tatizo la kuajiri waliohitimu vyetu itaanza kuondoka pole pole.

Mhe. Saleh Juma ameshapata jibu kutoka kwa Naibu Waziri kwa lile suala lake la awali. Nataka nimjibu swali lake la pili kwa ruhusa yako Mheshimiwa alilolileta kwa maandishi juzi. Mheshimiwa ametaka kujua fidia kwa eneo la Vitongoji, eneo ambalo tumejenga Chuo, Chuo kile tulipojenga tulidhani au ndivyo ilivyo kwamba lile eneo ni letu. Lakini tulipoanza kujenga wakatokea watu kudai kwamba walipwe fidia kwa vipando vilivyokuwemo. Tukatoa watu kwenda kuangalia, tukagundua waliokuwa wanadai walikuwa ni watu 18. Na vipando sio vya kudumu ni vipando ambavyo unaweza ukaviachia vikapea, vikamea wakavichukua na wakavuna wenyewe. Wengine walipanda mivinje. Tukaruhusu wenye mivinje waendelee nayo na tukasema hivi tutalipa fidia.

Mhe. Spika, tatizo likaanza kujitokeza idadi ya wakulima baada ya kusikia watalipwa fidia ikaongezeka mara dufu badala ya kuwa 18 wakawa 26 au 28. Idadi hii pia ikaongeza gharama za fidia. Sisi tulikubali kulipa shilingi 150 milioni kama ni fidia lakini iliyoletwa na Wizara ya Kilimo waliyoifanyia tathmini ikawa kubwa mara 3 au mara 4. Wizara ikakataa kulipa fidia hiyo na ikatoa utafiti mwengine na fidia ikathibiti pale pale 150 milioni. Sisi tukasema tuko tayari kulipa fidia hii na tukaanza kuchukua hatua ya kuanza mchakato wa kulipa angalau milioni 70 za mwanzo. Tukafanya *Re- allocation* tukapeleka Wizara ya Fedha kwa bahati mbaya haikukubalika, tulichelewe kidogo kupeleka. Lakini kwenye bajeti yetu fedha tumeziweka na hiyo fidia ilokuwa sahihi kama wakulima 19 au 18 wataikubali nataka nimthibitishie na nimuhakikishie Mhe. Nassor kwamba tutailipa baada ya kumalizika bajeti yetu.

Mhe. Rashid Seif, nadhani amepata majibu ya kutosha kwa Mhe. Naibu Waziri, nataka kuongezea kwa kumuomba sana. Nakubali maamuzi tuliyoyafikia ya kuwaleta hawa Wanaigeria 15 kwenye masomo ya sayansi na hesabati watusaidie kuondosha upungufu uliopo hawatawaondosha kabisa lakini watusaidie. Hawa ni *Volunteers*, hatuwalipi mishahara katika suala la Mhe. Mtando alitaka kujua habari hii kwamba, tunalipa mshahara, ni kiasi gani, tutawalipa na jumla ya fedha tutakazozitumia. Nasema hawa hatuwalipi mishahara hawa ni *Volunteers*, tutawalipia umeme, nyumba ya kukaa ipo, tutawalipia bili za maji na tutalipia gharama za kuwapeleka kwenye matibabu inapotakikana.

Sasa kama alivyokumbusha Naibu Waziri nataka nikumbushe na mimi pia kuleta *volunteers*. Tulianza zamani sana tokea baada ya Mpinduzi. Nataka nimkumbushe Mhe. Rashid Seif baada ya Mapinduzi walimu wote wa kiingereza na kutoka nje walitukimbia, ikatubidi tuagize au tuombe misaada kutoka Nigeria, Ghana, India nk. Sasa kama suala la Wa-Ghana, na Wa- Nigeria lafdhi yao ya kiingereza ni tofauti na yetu, hata wale walimu waliotusomeshea watoto wetu kutoka India lafdhi yao pia ilikuwa ni tofauti. Lakini waliweza wanafunzi wetu na hatimaye wakafaulu.

Naomba sana kwa sababu ni agizo la Rais tunalifanyia kazi. Rais alituagiza tuombe popote na tunajitahidi kuomba popote. Kwa mfano tumekwenda Balozi ya India amesema yeye sasa hivi hana walimu lakini yuko tayari kutupa nafasi wanafunzi wetu wakasomee masomo ya sayansi ya

hesabu. Tutafanya hivyo, lakini kama anavyosema Mhe. Naibu Waziri, tumeomba Misri, tumeonga Ghana, tumeomba kila pahali na bado tutaendelea kuomba, tutaomba mpaka Marekani, Uingeraza nk. Kwa hiyo naomba sana jibu hili nawajibu wale wengi waliozungumzia kuhusu walimu kutoka Nigeria.

Mhe. Mtumwa Mbarouk masuala yake yamejibiwa sana na Mhe. Naibu Waziri, sina cha kuongeza. Mhe. Awadh Salmin Awadh, Mhe. Ismail Jussa, Mhe. Hija Hassan Hija na Mhe. Asha Bakari Makame maswali yenu waheshimiwa yamejibiwa na Mhe. Naibu Waziri alipokuwa anakaribia kumaliza hotuba yake sina cha kuongeza.

Waheshimiwa wote walizungumzia suala la mishahara midogo ya walimu wakuu walimu wengine, maposho. Nimesema haya tunaanza kuyafanyia kazi, fedha zipo tumeomba na ninamuomba sana Waziri wa Fedha katika mchakato atakaoufanya wa kuondosha yale matumizi yaliyokuwa hayahitajiki matumizi haya atuachie. Kwa sababu asipotuachia tutakwama katika kuwaondoshea matatizo au kujibu kwa vitendo hoja za Waheshimiwa hawa kwamba walimu wetu bado hatujawatunza ipasavyo.

Wizara Elimu mbadala ya watu wazima humu muna suala la Mhe. Fatma Said Mbarouk, Mhe. Naibu Waziri wangu amelijibu vizuri. Elimu ya watu wazima kuna vifungu humu vimehojiwa, ninakubaliana na ushauri wa Mhe. Jussa, Mhe. Hamza Hassan Juma kwa kumuomba Waziri wa Fedha aviangalie tena vifungu vyote vya Wizara zetu zote zilizoleta mabadiliko ya haraka haraka.

Sasa kuna vifungu vyengine tumepunguza pesa sijui navyo hivi vitazingatiwa, halafu pesa tuongezewe sijui, lakini kwa mfano kuna kifungu 211108, kuna kifungu 22030, safari za ndani, malipo ya kujikimu, hizi tumepunguza bajeti. Lakini ninamuachia mwenyewe Waziri atakavyoamua baada ya kuvipitia vyote. Mhe. Mohammed Haji amekuwa na wasiwasi kuhusu mitaala ya elimu ya maandalizi na msingi juu ya ufundishaji wa ngazi za maandalizi, wanafunzi wa maandalizi na msingi kusomeshwa katika darasa moja. Mhe. Naibu Waziri amelijibu hili.

Nasema haya tumefanya kutokana na ukosefu wa madarasa ya kutosha ya maandalizi, ndio maana tumekubaliana kwa mujibu wa utaratibu wetu hawa maandalizi, waliochuchuka kidogo waingizwe pamoja na walimu wa msingi ili waweze kuwa pamoja. Na *observation* inatuonesha kwamba walimu wanaotoka kwenye maandalizi wanakuwa *more competent* kuliko wale wanaotoka nje na kuingia moja kwa moja darasa la kwanza. Lakini mawazo yao ushauri wao tumeusikia, ushauri wa Mhe. Mtumwa tumeusikia na wengi wametoa ushauri kama huo tutaufanyia uchunguzi, lakini wakati huo huo tutaendelea kuwashajiisha wananchi kujenga Skuli za Maandalizi. Wananchi wametusaidia sana katika hili, na sisi tumetenga fedha sio za kutosha lakini tumetenga fedha katika bajeti kuzikarabati na kuziezeka na kuzijenga vizuri Skuli zote za Maandalizi na nyenginezo za msingi zilizojengwa na wananchi ili kukamilisha nguvu zao zithaminike.

Mhe. Ismail Jussa wa Jimbo la Mjimkongwe alisikitika sana kwa mradi ambao wa Kajificheni ukatekwa nyara na Skuli ya Kisiwandui. Hili Mhe. Naibu Waziri amelijibu nadhani Mheshimiwa umetosheka na juhudi tunazifanya, na tumeshawasiliana nao hawa wenye mradi huu ili kuurejesha kwa njia nyengine huu mradi ili na wao waupate ule mradi wao.

Mhe. Spika, Mhe. Shadya wa viti maalum anaomba Wizara kupunguza wimbi kubwa la watoto katika darasa, kwani baadhi ya skuli kuna zaidi ya watoto 100 katika darasa moja. Mhe. Spika, tunakubaliana nae kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri tutaendelea kuhimiza ujenzi wa madarasa mapya, na Serikali itasaidia kuezeka na kufanya ukarabati mwengine ili tuhakikishe pahala pa kusomea panaongezeka, kwa sababu tumeshajiisha vya kutosha wazee na wazazi wapeleke watoto wao skuli, ili ifikapo mwaka 2015 tulitekeleze lile lengo la *millenia* pamoja, na kuwa sasa tumeshalitekeleza kila anayestahiki kwenda kusoma anapelekwa skuli. Lakini bado idadi ya wanaokwenda skuli ni kubwa kuliko uwezo wa madarasa yetu. Hili tumeliona na tunalishughulikia.

Elimu ya mjumuisho Mhe. Naibu Waziri ameizungumza nataka niongezee kusema kwamba kuitekeleza kwa sasa hii ilikuwa kama ni *pilot* au *experiment*, lakini *experiment* hiyo imetupa faraja kuona kwamba hatua hizi tulizozichukua zinafaa badala ya kuwatenga wanafunzi wenye mahitaji makubwa, magumu, kuwatenga mbali peke yao na kuwaacha wasisome pamoja na wenziwao waliokamilika, wenyewe wanasema ni eneo la unyanyasaji. Tumelipokea hilo na kutokana na utafiti wa awali unaonekana kwamba inatusaidia. Kama alivyosema Mhe. Naibu kwamba wapo walimu katika hizo skuli za mjumuisho wanafanya vizuri, wengine wanatokea wa kwanza na wa pili katika skuli za mjumuisho, kwa hivyo bado tutaendelea kulitekeleza suala hili.

Mhe. Rashid Seif, Mhe. Salmin Awadh, walitaka kujua bajeti ya maendeleo ya chuo kikuu cha taifa ipo? Kwani kazi ya kukiendeleza hichi chuo zimeshakamilika? Mhe. Rashid Seif nakuomba nikurejeshe katika kifungu cha 30 ukurasa wa 21 wa kitabu cha bajeti, unazungumzia hoja hiyo kwamba fedha katika bajeti zipo na mradi huu umepatiwa shilingi bilioni 1.7 za SMZ na shilingi bilioni 3.3 za BADEA. Kwa hivyo bado mradi upo unaendelea na bajeti yake ipo.

Mhe. Salmin Awadh alitushauri hatua hii ya kuzichukua taasisi au skuli nyengine kuziweka pamoja na SUZA, hata kama uamuzi huu au ushauri ulitolewa na Rais sisi watekelezaji tuwe *very careful*, tunakubaliana na hoja yake na kwa kweli tuko *extra careful*. Na tumeweza kuziweza kuzichambua kwa haraka zile skuli ambazo zinaweza kujumuishwa na SUZA lakini sio skuli zote tunakwenda pole pole. Na SUZA ni Chuo Kikuu pekee cha Serikali. Wakati huo ilikuwa ni sahihi hawa wengine wajianzishe kidogo kidogo, lakini kama sasa wameshakuwa ni vizuri tukafikiria suala la kuwajumuisha na SUZA ili SUZA wenyewe iweze kukua.

Mhe. Spika, tunakataa kuwa SUZA yenyewe inasuasua, SUZA haisuisui, kuna kila ushahidi SUZA inaendelea na inafanya vizuri. Tuupe nafasi ushauri wa Mhe. Rais na kama mlivyotushauri sisi tutafanya pole pole kwa uangalifu zaidi, ili tusije tukakichukua kwa mfano Chuo cha Afya ambacho kipo na kinafanya vizuri tukakiunganisha na SUZA ili kifanye vizuri zaidi, na badala yake kikaja kikafa. Hilo tutajaribu kama iwezekanavyo kuepukana nalo.

Mhe. Salmin Awadh aliuliza tena kuhusu Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar ni mwanachama wa TCU, SUZA imejitoa kwenye kipengele kimoja tu cha TCU nacho ni kile cha udahili kwa kupitia CAS. Kwa hivyo SUZA bado kinaendelea kushirikiana na TCU ukiacha hicho kipengele walichokitoa.

Mhe. Spika, Mhe. Fatma Said Mbarouk nimeshamjibu na Mhe. Hassan Hamad wa Kojani, yeye anataka kujua katika suala hili la muungano wa elimu ya juu sisi na Tanzania Bara kuna kasma yoyote ya bajeti inayotoka huko? Jibu ni kwamba ni kweli limejiunga na suala la muungano, lakini chuo kina mitaala na program zake wenyewe na kinajitegemea wenyewe kwa kazi nyingi sana. Lakini Chuo cha SMZ na hata kama elimu ya juu ni suala la muungano, SUZA itabaki kuwa Chuo cha Taifa cha Zanzibar. Na kwa hiyo SMZ ndio itakayohusika na kukamilisha bajeti na kuendesha Chuo hicho na hivi sasa inakwenda vizuri.

Mhe. Hamza Hassan Juma, kwanza ninakushukuru kwa michango yako uliyoitoa kwenye bajeti hii, umeitoa kwa upole, umeitoa kwa uangalifu sana, hukutumia ule utaratibu uliouzoea wa kutuhenya, kutushambulia, kutubana na kadhalika umetushauri sana na tunakubali ushauri wako. Umetwambia pamoja na chuo chetu kupata ruzuku kutoka kwenye bajeti ya Serikali, lakini chuo bado ruzuku yake haitoshi, na kama kuna uwezekano wa kuongeza basi tuongeze bajeti ya Chuo Kikuu. Bajeti yetu ya chuo kikuu ni bilioni nne sasa hivi nukta kidogo. Profesa kijana aliyepo sasa hivi anaendesha hichi chuo *Vice Chancellor* ni mkakamavu, ni muelewa, ni hodari sana ana programu nyingi sana nzuri. Sisi tumewahi kutembelea chuo chake kule Tunguu na kila siku ukienda unakikuta kimebadilika. Na punde si punde atahamia katika chuo hichi.

Kwa hivyo kama kutakuwa kuna uwezekano wa kuongeza bajeti yake tuongeze, vyenginevyo mwakani tuonewe huruma, tutakapoleta bajeti ya SUZA iangaliwe kwa jicho la huruma.

Mhe. Hamza Hassan alizungumza suala la malipo, suala la kuchelewesha kulipa malipo ya ada akatuomba tustahmili tusiwe wakali katika kuwadhibiti waliokuwa hawajalipa bado, lakini nataka nimhakikishie Mhe. Hamza pamoja na stahmala hiyo na ukarimu tunafanya kama ulivyotangulia kusema bajeti yetu ni ndogo, pesa nyengine tunazozitegemea ni hizi za ada na kadhalika. Na pesa za mwaka huu ukizingojea mpaka mwaka ujao inapungua thamani, na kwa hivyo tunaendelea kula hasara. Tutaendelea kuwa wapole si wastahmilivu lakini wapole na kuzidai hizi ada pole pole, lakini Mhe. Hamza kuwasamehe itakuwa ni vigumu sana.

Mhe. Mohammed Haji Khalid alitoa hoja kutaka kidato cha nne wanafunzi wetu wanafeli sana, kwa sababu maandalizi ya *secondary* hayafanywi vizuri. Mitihani inayotoka Bara kidato cha nne ni tofauti kabisa na maandalizi tunayoyaandaa sisi kwa wanafunzi wetu hapa Zanzibar. Napenda kujibu hoja hii kama ifuatavyo:-

Katika ngazi ya elimu ya sekondari yaani kuanzia kidato la kwanza hadi kidato cha sita Zanzibar tunatumia mitaala sawa na Tanzania Bara, kwa hivyo suala la kudumaza wanafunzi kwa kuwa tunafanya mitaala yetu hilo halipo.

Halafu Mhe. Mohammed Abdalla Ali Jimbo la Mkoani aliuliza somo la historia linasomeshwa katika skuli za Zanzibar? Jibu lake ni kwamba tunasomesha. Tunasomesha katika darasa la tano hadi la sita, tunasomesha kama *pure* historia, vile vile kidato cha kwanza hadi kidato cha sita. Pia somo la historia linasomeshwa kama ni jina la historia.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu aliuliza kuhusu suala la vitabu vinaandikwa na wazanzibari kwa nini vitabu hivi hatuvitumii na badala yake tunatumia tulivyovikataza vya Macmillan.
Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Jussa kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, uandishi wa vitabu kwa Zanzibar wengi wao vitabu vyao viko katika hatua ya miswada huwa havijakamilika kuwa vitabu. Hata hivyo hivi karibuni Wizara yangu kupitia taasisi ya elimu Zanzibar imefanya tathmini ya vitabu 30 vilivyoandikwa hapa Zanzibar kutoka Baraza la Kiswahili la Zanzibar yaani BAKIZA. Baada ya ripoti ya tathmini ya vitabu hivyo kukamilika vitabainisha namna gani miswada hii inaweza kurekebishwa ili iwe vitabu kamili.

Kuna vitabu vyengine tisa vya Kiswahili vya riwaya, vitabu viwili vya tamthilia, tenzi na shairi vitabu tisa, kamusi vinne, Kiswahili sanifu kimoja, Kiingereza vinne, hesabati kimoja na dini viwili. Vitabu hivi vipo tunaviangalia, tunavitafiti zaidi na hatimae kuvisambaza maskulini.

Mhe. Spika, Mhe. Mohammed Haji Khalid na Mhe. Saleh Nassor, walitaka kujua kuhusu usahihishaji wa mitihani kutoka Pemba na masuala yao ilikuwa kwa nini ni idadi ndogo inayotoka Unguja kwenda Pemba, na idadi inabakia waunguja watupu peke yao akenda mbele zaidi akasema huu sio ubaguzi? Nataka kumthibitishia kwamba hapana sio ubaguzi hatuwezi kumbagua Mpemba na Muunguja. Lakini kutokana na bajeti ya kumleta msahihishaji kutoka Unguja kwenda Pemba ina matumizi makubwa. Sasa tumeliangalia hilo na tumeangalia hii hoja inayoanza kuchimbuka ya kisiasa, na tunafikiria njia mbadala za kutumia walimu kutoka Pemba na walimu kutoka Unguja kadri iwezekanavyo kusahihisha mitihani. Lakini mitihani lazima ibakie katika kituo kimoja tu, na kituo hicho ni hapa Unguja. Kwa hivyo kasoro hii tumeisikia na tutaifanyia kazi na *inshaallah* tutaiondosha katika hali ya kuridhisha.

Mhe. Spika: Mheshimiwa jitahidi muda unakwenda haraka ili tuweze kumaliza shughuli hii.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ninakushukuru na ninakwenda kwa haraka haraka sasa. Mhe. Jussa ameshajibiwa kuhusu yule mwalimu wa biashara mwenye shahada ya fani ya biashara akachukuliwa akapelekwa skuli kwenda kusomesha fani ambayo hakusomea tumelisikia hilo na tunalifanyia kazi kwa haraka sana.

Mhe. Omar Ali Shehe kutengewa fedha za vifaa vya maabara kwa kufundishia, kweli ni kuwa mamlaka fedha hizi ni nyingi na zinahitaji kufanyiwa marekebisho. Jawabu sahihi ni kama tulivyolizungumza kwamba Mheshimiwa atamwachia Mhe. Waziri wa Nchi, Fedha, Uchumi na Maendeleo kuzipitia bajeti zote na kuangalia vipaumbele.

Bodi ya Mikopo imechangiwa na watu wengi. Mhe. Spika, tunakubali kwamba bodi ya mikopo ina matatizo, tunakubali kwamba liko agizo alilitoa Mheshimiwa, nitamkumbuka kutaka anisaidie suala hili la kukusanya mikopo iliyochukuliwa na wananchi hao wasomi mbali mbali. Na akashauri tuitumie kamati ya PAC ili tusaidie, mimi nilikubaliana nae hapo tuitumie kamati ya PAC itusaidie kukusanya mikopo. Na sisi tunayo orodha ya wakopaji wote na wale ambao bado hawajalipa ingawa orodha hii ina kasoro fulani ambapo hatukuonesha kwa ukamilifu wale wote ambao hawajalipa. Nasema kuna idadi ya watu ambao hawajalipa bado wako masomoni hawajamaliza kusoma. Na ile kasoro ya milioni tatu inaonekana inatokana na hawa bado hawajamaliza kusoma, na kwa sababu hawana kazi hawajapata uwezo wa kulipa.

Mhe. Spika, ofisi yangu haijakaa kimya maana hiyo kamati ya PAC sina hakika kama imeshapewa agizo au haijapewa agizo. Na mimi nadhani sina mamlaka ya kuitaka kamati ya

PAC isaidie suala hili. Kwa hivyo sisi wenyewe tunaendelea bado na mchakato wa kutafuta madeni, na sasa tumeshakusanya bilioni nane za madeni na tunaendelea kukusanya. Tumetafuta vipande vyote vya ukaazi kwa wazanzibari na kadhalika. Tumeandikiana na Wizara ya Nchi, ya Mhe. Haji Omar Kheri, kushirikiana pamoja na kupata idadi ya wafanyakazi binafsi ili tuwakusanye tuwajumuishe na tuanze kuwadai.

Kwa hivyo almuradi zoezi la kuwatafuta wadeni bado linaendelea, na miezi sita tulichofanya kazi hii ya kukusanya hivi fedha, sisi tuna hakika hii kazi bado tutaiweza, maana pesa hizi za mikopo ni tokea mwaka 2006 ni za siku nyingi kidogo, lakini kama kuna uundwaji wa kamati hiyo iliyotajwa inaweza kutusaidia kama nilivyosema awali, nasema tena sisi tuko tayari hiyo kamati iundwe na tutashirikiana nayo kadiri iwezekanavyo ili tuweze kushirikiana kuzipata hizi fedha.

Mhe. Spika, fedha zilizoongezwa katika bajeti bilioni nane kati ya hizi ziko fedha nyengine itabidi zitumike kwa madeni na kwa malipo mengine. Fedha itakayobakia kwa kutumia mikopo peke yake itakuwa kama bilioni nne na sio pesa nyingi sana. Kwa hivyo idadi ya fomu zinazokuja sasa maombi ni kubwa inaongezeka kila leo, ingawa sasa tumeshafika tamati kupokea idadi hiyo, kupokea fomu hizo. Lakini nataka nilithibitishie Baraza hili bado hatutakuwa na uwezo wa kutoa mikopo kwa kila atakaetaka kukopeshwa.

Umetoka ushauri hapa kwamba mikopo sasa tuwape wale waliokosa katika kipindi kilichopita, ushauri huo ninauunga mkono asilimia mia moja, na hivyo ndivyo tulivyoelekeza nguvu zetu. Kwanza *priority* ni hawa baadae tutawapa wale ambao wametimiza haja za kukopeshwa.

Mhe. Spika, Mhe. Rashid Seif tumeshamjibu, Mhe. Rifai alitwambia skuli ya Tumbe hakuna umeme tunakubali kwamba skuli ya Tumbe hakuna umeme, na hiyo imeshajibiwa. Lakini sio skuli ya Tumbe tu, ni skuli nyingi sana hazina umeme. Waheshimiwa Wabunge na Wawakilishi tumewaomba na tunaendelea kuwaomba na wanaamua kuzisaidia skuli zao katika majimbo yao, wanafanya kazi nzuri sana na sisi tuna-*appreciate* misaada yao wakeshaanza Wizara inakuja kumaliza pale palipobakia.

Kwa hivyo naomba sana tuendelee Waheshimiwa Wabunge na Wawakilishi nikiwemo na mimi Mwakilishi, tuendelee kuzisaidia skuli zetu kuzipatia umeme ili wanafunzi wetu waweze kusoma mchana na usiku kufanya *revision* zao.

Mhe. Spika: Wakati Mheshimiwa anaendelea na anakaribia kumaliza tuone basi Waheshimiwa walioko nje warudi ukumbini tumalize kazi hii. Watendaji wetu tusaidie kuwapa taarifa Wajumbe walioko nje.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Hoja iliyotolewa na Mhe, Jussa Ladhu ya vifungu hivi vya fedha vilivyorekebishwa hasa kile kifungu cha mipango, uendeshaji na utafiti cha Wizara yangu na nakubaliana nae kama alivyokubali Mhe. Waziri wa Fedha tutaviangalia na hatimae kuvifanyia marekebisho.

Mhe. Spika, Baraza la Mitihani nataka nimalizie kwa kuonesha huu utafiti tulioufanya kwa kushirikiana kati yetu na Tanzania Bara kwa wale waliofutiwa matokeo yao ya mitihani, wale

waliozuiliwa kufanya mitihani mpaka baada ya miaka mitatu jambo ambalo tumeshalimaliza. Taarifa hii inaeleza kwamba kuna kasoro nyingi sana, kuna kasoro za wanafunzi za kughushi, kukopia, kasoro za walimu na walimu wakuu na kadhalika, tumejifunza vya kutosha.

Hatua ambazo tumezijadili na ziko njiani sasa kutekelezwa ni moja iliyotoka katika taarifa hii, lakini pia hatua hiyo tuliyokuwanayo zamani kwamba, kuanzia sasa mitihani isisimamiwe na Kamati za Mikoa au Wilaya wala isisimamiwe na vyombo vya ulinzi. Mitihani sasa itasimamiwa na Wizara yenyewe kuhakikisha tunakuwa madhubuti, mitihani haivuji na kasoro ndogo ndogo zilizotajwa hazitatokea. Na kile kitakachotokea kwa bahati mbaya sisi lazima tutawajibika maana ni letu hili kuliko kumuachia askari Valantia anafanya kazi kukimbia sisi majukumu.

Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu nawashukuruni nyote, nasema ile michango niliyoipata leo asubuhi ambayo ilituuliza mengi ya kitakwimu namuomba radhi Mhe. Mbarouk Wadi Mussa, kama alivyosema kuwa kama sitompa majibu hatoipitisha bajeti. Namuomba sana aipitishe bajeti yangu na mimi naahidi majibu nitayaleta hapa Barazani kwa Mhe. Spika, ili sio yeye tu, lakini na wengine wote wapate kuyaona na wapate kuridhika. Baada ya hayo Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri tunakushukuru na Waheshimiwa Wajumbe tunawashukuru wote mmekuwa watulivu kusikiliza majumuisho kwa muda wote.

Waheshimiwa Wajumbe sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka 2012/2013 wananyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kukubali hoja ya bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kupitisha vifungu vya matumizi ya Wizara yangu. Naomba kutoa hoja.

UTARATIBU

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, kutokana na hoja nyingi ambazo tulizizungumza kuhusiana na vifungu mbali mbali vya matumizi ambavyo tulisema tutavihoji wakati wa kupitisha vifungu, na kwa sababu Waziri mwenyewe katika majumuisho yake amekiri kwamba kuna matatizo ya msingi katika vifungu hivi. Mhe. Spika, naomba tutumie kanuni ya 156 na uruhusu kutenga kanuni kando kuomba ruhusa yako na Baraza lako kwamba kanuni ya 98(3) ambayo naomba niisome.

Kanuni ya 98(3) inasema kwamba:

"Endapo hoja ya kupunguza fungu kwa kupunguza kifungu chake fulani kidogo cha fungu hilo kimekubaliwa au kukataliwa, hoja nyengine si zaidi ya mbili zinaweza kuruhusiwa juu ya kupunguza kifungu hicho".

Mhe. Spika, nilikuwa naomba kwamba utuhoji tutenge kanuni hii kando, ili uturuhusu katika kila kifungu angalau tuweze kusimama mara tano katika fungu. Kwa sababu Mhe. Spika, nina sababu ya msingi, tumevipitia vifungu hivi tumefanya kazi ambayo tumeletewa hapa ambayo ni kuchunga fedha za wananchi walipa kodi, na vifungu vingi vina masuala mengi ambayo yanahitaji kuhojiwa ili tuweze kuidhinisha vifungu hivyo. Kwa hivyo, naomba Mhe. Spika, tutenge kando kanuni ya 98(3) ili uturuhusu badala ya hoja tatu kwa kila fungu, basi angalau hoja tano kwa kila fungu zikubaliwe tuweze kuhakikisha kwamba fedha za walipa kodi zinalindwa na zinafanya kazi ambayo wananchi wenyewe walipa kodi wanaikusudia. Naomba kutoa hoja Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Unajua kifungu hiki cha kutenga kanuni kando ni kifungu ambacho kinatumika kwa sababu ya dharura, inapotokea dharura kwa ajili ya jambo mahususi basi tunatenga kanuni kando, ili kuweza kwa ajili ya jambo hilo mahususi liweze kufanyika vizuri.

Kwa mfano, leo tumetenga kanuni kando kwa sababu kikao hiki tumechelewa mno hiyo ni dharura, dharura ambayo imetokea kwa sababu nyingi, moja ni kwa sababu ya shughuli zetu ambazo zimerefuka tukawa tuko nyuma kwa siku moja, lakini pili ni kwa sababu ya msiba mkubwa uliotokea ikabidi kikao kisiendelee kwa muda wa siku mbili; hizo ni dharura. Sasa muda utakuwa hautoshelezi kumaliza shughuli yote ya bajeti, na kwa sababu huu ni Mwezi wa Ramadhani ambapo kanuni yetu inapunguza muda wa saa moja dakika arubaini na tano kwa kila siku itazidi kurejesha nyuma kufanikisha shughuli zetu.

Kwa hivyo, kwa mwezi huu tutakubaliana sote kwamba hiyo nayo ni dharura kubwa kufanya vikao jioni isingewezekana, ndio maana ikawa tumekubaliana kanuni tubadilishe iwe hadi saa nane, lakini pia tukaitenga kanuni hiyo ili tuongeze angalau dakika 30 iwezeshe shughuli zetu kufanyika.

Sasa tutumie nafasi kwa mujibu wa kanuni yetu ilivyo kama ilivyo chini ya kanuni ya 98(3) tusifumue kanuni hii kwa kila wakati kutenga kanuni kando tukaleta mwanya kwa kufanya masuala mengine. Suala la Mhe. Ismail Jussa ni muhimu lakini bado nataka nisisitize tutumie kanuni iliyopo, na sitapendelea hoja hii tuiamue na tuendelee kwa utaratibu wa kanuni iliyopo.

Maelezo yaliyotolewa kwamba masahihisho yatafanyika basi isaidie, na tayari hayo mafungu tuliyaonesha, ahadi imetoka kwamba marekebisho yatafanyika mimi nadhani isaidie na tuendelee kutumia kanuni iliyopo. Kwa hivyo, tuendelee na shughuli zetu na sasa Kamati ya Matumizi ikae. Waheshimiwa Wajumbe nakushukuruni.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU 23 WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI

Kifungu 0401 – Idara ya Mipango, Sera na Utafiti 22,500,000

Jumla ya Fungu: **22,500,000**

(Kijifungu kilichotajwa hapo juu kimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Fungu 23 Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali

Kifungu 0401 – Idara ya Mipango, Sera na Utafiti

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nishukuru kwa hekima yako uliyoitumia na nimekubali hoja yangu kuiacha kwa sababu ya kukubali hekima zako, haidhuru kanuni inaruhusu kwamba utuhoji moja kwa moja lakini nakiheshimu sana kiti chako.

Mhe. Mwenyekiti, naomba vile vile nimshukuru Mhe. Waziri na Naibu Waziri kwa kujibu hoja mbali mbali, sasa Mhe. Mwenyekiti niende moja kwa moja katika hoja yangu. Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu mimi nilikuwa mmoja wapo wa Wajumbe ambao walihoji baadhi ya vifungu vya matumizi, na nikatoa mfano Idara ya Mipango, Sera na Utafiti lakini nikasema nitavihoji kwa kila Idara kwa sababu muda ulikuwa hauruhusu kwenda kimoja kimoja, lakini nilionesha vifungu hivyo hivyo mpaka nitapokinaishwa kwa maelezo. Sasa Mhe. Mwenyekiti, nimesikiliza maelezo yaliyotolewa, lakini bado naomba maelezo na naomba hoja yangu ifahamike vizuri na Waziri na Mhe. Naibu Waziri tufuatane pamoja.

Hoja yangu Mhe. Mwenyekiti, ilikuwa ni kwamba ukichukua waraka huu tuliopewa ambao umefanya marekebisho ya mahesabu utagundua kwamba *vote* 211100 ambayo iko ukurasa wa nne juu pale, fungu hili awali katika hili buku lilikuwa katika fungu la malipo baada ya saa za kazi 211107, lilikuwa na jumla ya shilingi 115,599,000/-. Utachokigundua hapo Mhe. Mwenyekiti, zimeondolewa *round figure* shilingi milioni mia moja zikabakishwa shilingi 16,599,000; ingelikuwa zimeondolewa hizo ikawa zimepunguzwa ili kuzinusuru fedha za walipa kodi tungekuwa hatuna hoja tena, lakini kwa sababu wewe ulitaka kuhalalishiwa matumizi, zimechukuliwa zikenda zikatupwa katika mafungu mengine zikagawanywa kidogo kidogo. Nataka maelezo katika hilo Mhe. Spika.

Kwa kumkumbusha Mhe. Waziri naomba niyataje kwa uchache tu. Mhe. Mwenyekiti, katika shilingi milioni 100 hizo shilingi 30 milioni zimetupwa katika fungu la 220100 Gharama za vifaa na Huduma za Mawasiliano kwenye *sub vote* ya gharama za vifaa vya uchapaji ilikuwa shilingi milioni 11,900.0000 ikafanywa shilingi milioni 41, 900,000/-. Kwa hivyo thalathini zikawekwa hapo.

Halafu katika fungu la gharama za safari za nje palikuwa na shilingi 4,000,000/- zikawekwa shilingi 24,000,000/- kwa hivyo na shilingi 20,000,000 zikaongezwa hapo hapo jumla 50,000,000/- Mhe. Mwenyekiti. Katika jumla ya fungu la Mafunzo ambapo awali lilikuwa katika fungu 221100 ukurasa wa tano lilikuwa *zero* kama lilivyokuwa mwaka jana lilikuwa *zero* vile vile likawekwa shilingi 30,000,000/-. Sasa Mhe. Mwenyekiti, ukijumuisha hizo pamoja na katika fungu la viburudishaji zikaongezewa pale, jumla ukifanya hesabu unakuta zile shilingi 100 milioni zimechomolewa pale, lakini zikawekwa katika fungu awali lilikuwa lishakadiriwa kwamba lilikuwa na mahitaji halijajitosheleza.

Kwa hivyo, naomba maelezo ya Mhe. Waziri kwa nini tuidhinishe, na kwa nini tusizikate hizi shilingi 100,000,000 ambazo wenyewe katika Idara hii walishaziona kwamba zimezidi hapa juu wakazikata wenyewe katika marekebisho haya, lakini baadae yakaoneshwa matumizi zikawekwa katika vifungu vyengine. Waziri anitosheleze kwa nini Baraza hili Kamati hii ya matumizi isikate shilingi 100,000,000 katika fungu hili la Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Naomba maelezo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Ismail Jussa suali lake linalohusu kupunguza fungu katika bajeti ile au kifungu kile kwa shilingi 100,000,000/- na baadae tukazigawa katika vifungu mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, mwaka huu zaidi ya kazi zake za kawaida, Wizara yangu imepewa majukumu ya utafiti. Kuna tafiti za aina mbili za kimataifa, moja zinahusu nchi 15 na tafiti moja inahusu nchi nne za Afrika Mashariki. Nchi 15 hizi za Afrika ya Mashariki Kati na Kusini zenye nchi 17. Katika bajeti yetu kwa utaratibu wa ile *system* ya utengenezaji wa bajeti ya kisasa lilikuweko fungu moja tu, na fungu hili likachanganywa katika matumizi yote tuliyoyagawa, tulipogundua kwamba tuna jukumu la kutekeleza hizi tafiti za kimataifa, moja inahusiana na kupima namna ya maendeleo ya taaluma inayotolewa katika nchi hizi 17 za Afrika na namna inavyokuwa *effective,* na nyengine ilikuwa inalingana na hilo hilo, lakini hili kwa nchi nne za Afrika Mashariki, ndipo tulipoamua kuzitoa hizi shilingi 100,000,000/- milioni kuzitenga huku na katika utafiti huu.

Katika utafiti huu tulioufanya sisi tunakwenda katika nchi za wenzetu, wao wanakuja, tunakaa pamoja, tunajadili, tunaandika waraka na kadhalika, kuna matumizi makubwa ya safari, malazi, vinywaji na kadhalika na chakula. Kwa mfano, hivi sasa mwenzetu mmoja yuko Afrika ya Kusini na juzi alitoka Nairoibi katika kufuatilia kazi hizo hizo.

Mhe. Mwenyekiti, tunaweza tukalitoa hili fungu sawa, lakini maana yake tunajitoa katika utafiti au katika tafiti hizo za nchi 17 za Afrika Mashariki na Afrika ya Kati, Kusini na hizi nchi nne za Afrika Mashariki, tumejitoa. Kujitoa maana yake nini? Maana yake tunakosa maendeleo, ruzuku, kushiriki na kadhalika. Kwa sababu hiyo narejea tena kusema Mhe. Mwenyekiti, tusiamue kwa haraka hata kama kunaonekana kuna kasoro, hizi kasoro zina maana yake na tumezitolea maelezo. Bila ya sisi kushiriki katika tafiti hizi uwezo wetu wa kitaaluma unapungua sana kama hautotoweka moja kwa moja. Sasa namuomba Mhe. Mwakilishi aizingatie tena hoja yake, pamoja na jukumu tulilopewa sisi sote la kulinda pesa za wananchi wavuja jasho, lakini katika hili sababu za msingi zipo na hatukuzitoa pesa hizi halafu tukazibandika bandika tu kila pahala, tumefanya utafiti na tukajua kwamba fedha hizi tukizeweka katika maeneo haya ya utafiti na shughuli nyengine za maendeleo tutapata manufaa na mafanikio makubwa. Mhe. Mwenyekiti ahsante sana.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, mimi niwaombe sana Waheshimiwa Mawaziri kwa jumla, tunawaomba sana naendelea kusisitiza wasiamini maelezo tu ya jumla jumla wanayopewa na watendaji wao, maelezo aliyonipa Mhe. Waziri namuheshimu sana mzee wangu, hayaendani na huku kulikopelekwa vifungu. Ili nifahamike Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri amenijibu kwamba hii ni kwa sababu ya kuimarisha utafiti ambao unajumuisha mashirikiano ya kimataifa na nchi nyengine. Lakini Mhe. Mwenyekiti, hebu nambie kwa akili ya kawaida tu, hizi

fedha awali katika hili buku ilikuwa zimewekwa katika fungu la malipo baada ya saa za kazi, na ndio yalivyo katika kila kurekebishwa kulikokuweko huku, na ndio tukasema humu ndimo mnamofichwa, ndio vichaka vya watendaji kufanya matumizi yasiokubalika.

Mhe. Mwenyekiti, tunajiuliza Wizara ya Elimu ina walimu wanafanya kazi hawana malipo ya muda wa ziada, na haya mafungu kwa nini yameongezeka. Sasa limehamishwa pale kwenye malipo baada ya saa za kazi limepelekwa wapi. Shilingi 30,000,000/- nimesema zimeongezwa kwenye gharama za vifaa vya uchapaji, zilikuwa shilingi 11,900,000/ imekuwa shilingi 41,900,000/- hebu nambie vifaa vya uchapaji Mhe. Mwenyekiti vinahusiana nini kwenda Kimataifa kwenda kufanya utafiti. Lakini pale pale juu imepunguzwa ile shilingi 100, 0000, 0000 malipo baada ya saa za kazi shilingi 20 milioni ikaingizwa katika malipo ya kujikimu na malazi, ilikuwa shilingi milioni tisa ikafanywa 29 milioni. Hiyo labda unaweza kusema ndio katika kusafiri, lakini halafu viburudishaji Mhe. Mwenyekiti, hapa pana viburudishaji.

Katika gharama za safari kama nilivyosema hili buku wamelitayarisha wao wakaweka shilingi milioni nne kwa safari za nje, imekuwa shilingi milioni ishirini zimewekwa pale, labda hiyo inaendana kidogo na maelezo ya Mhe. Waziri. Lakini Mhe. Mwenyekiti, gharama za mafunzo ya ndani na ya nje, sasa kama mtu anasafiri kwa mafunzo haiwezekani ikawa kuna shilingi milioni ishirini huku, halafu ikawa mtu huyo huyo kuna mafunzo ya nje anaingiziwa katika safari za nje. Kwa hivyo, unakuta hapa kwenye mafunzo pamewekwa mafunzo ya ndani shilingi milioni kumi, na mafunzo ya nje shilingi milioni ishirini jumla thalathini, ilikuwa *zero* Mhe. Mwenyekiti.

Mwaka jana pia hapa palikuwa *zero* katika fungu hili la safari. Sasa ndio nikasema ukichukua shilingi thalathini hizi na thalathini za gharama za uchapaji, ishirini za gharama za safari na ishirini katika malipo ya kujikimu ndio unazipata zile mia, hizo Mhe. Mwenyekiti, haziwiani kabisa na maelezo aliyotupa Mhe. Waziri. Kwa hivyo, nilikuwa namuomba Mhe. Waziri katika hili atukubalie kwa radhi kabisa hizi shilingi milioni mia moja watendaji wake walijua kwamba hazina maelezo ndio maana mwanzo ziliwekwa katika malipo ya baada ya saa za kazi, baada ya kuona Wajumbe wanahoji katika marekebisho haya zikenda zikagaiwa katika mafungu ambayo hayana hata uhusiano Mhe. Mwenyekiti. Kwa hivyo, nasema nimuombe sana Mhe. Waziri nataka kumwambia ajitayarishe kwa sababu mimi takriban nina shilingi karibu milioni mia sita nataka kuzikata hapa za mafungu mbali mbali. Kwa hivyo nasema hizi shilingi milioni mia moja katika idara hii atukubalie tuzikate kwa sababu zinaonekana wazi hazihitajiki.

Mhe. Mwenyekiti yako mafungu yameongezeka katika Idara hii wala hayo sikuyahoji, na naomba ili nifahamike niseme moja tu nipate nikae. Jumla ya bajeti ya Idara hii imepanda kutoka shilingi 271,500,000 milioni mpaka shilingi bilioni moja laki nne arubaini na nne elfu kwa mwaka huu. Na kuna fungu kubwa limeongezeka la ununuzi wa samani hatukulihoji shilingi 987 milioni, kwa hivyo kuna mafungu mengi yameongezeka hatukuyahoji kwa sababu maelezo yake yanawiana, lakini haya ya shilingi milioni mia moja ambazo kuwa juu hazina maelezo zikatawanywa katika mafungu mengine haya Mhe. Waziri atukubalie kuwa maelezo yake waliyomuandalia hayakidhi haja, na hivyo alikubalie Baraza hili kupitia Kamati ya Matumizi inayosimamia fedha za wananchi wa Zanzibar tuziondoshe pesa hizo. Naomba sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kwa maelezo yako. Mwanzo tulizungumza hapa na Waziri wa Fedha akakiri kwamba haya mafungu yana matatizo, lakini sio kama yana matatizo kuwa hayatumiki, yana matatizo kutokana na ule utaratibu wao wa *MTEF* ambapo *system* yake wameweka. Hivi vifungu Mhe. Mwenyekiti, vyote viliwekwa kwenye fungu la malipo baada ya kazi kama Mhe. Ismail Jussa alivyozungumza, baada ya kuona yale ambayo yamewakuta wenzetu, na kwa sababu mafungu haya yote yako katika kifungu hicho ambacho kimewekwa tukaona ni vizuri tulichukue lile fungu tulichambue yale matumizi ambayo tunataka kuyafanya na matumizi tunayotaka kuyafanya ni haya aliyoyazungumza Mhe. Waziri.

Mhe. Ismail tuna tafiti mbili za kimataifa kubwa ambazo tafiti hizo tunalenga kufanya ndani ya mwaka huu, kwenye tafiti hizo Mhe. Mwenyekiti kuna gharama za uchapishaji, kwa sababu kuna madodoso ambayo tutayatawanya kwa walimu wetu kwa wilaya zote za Unguja na Pemba. Hiyo bila shaka inahitaji gharama za uchapishaji na ndio hizi ambazo tumeziweka hapa shilingi thalathini milioni, fedha hizi zitatusaidia kuchapisha hayo madodoso katika skuli zetu zote.

Lakini kuna gharama za safari za nje, Mhe. Ismail kifungu hiki 220300 hiki tunakusudia kwenda katika hizo safari, kwa sababu hii ni mikutano ya kimataifa ambayo inafanyika. Kwa hivyo, hapa tunahitaji nauli za kwendea huko kwa watu wetu, na hizi safari Mheshimiwa zitakuwa nyingi. Kama mmepata taarifa kuwa kuna tunzo ambayo aliipata Mhe. Waziri aliyepita Mhe. Haroun Ali Suleiman ni tunzo ambayo inahusisha vikao hivi na tafiti hizi ambazo zinafanywa. Kama alivyozungumza Mhe. Waziri kuwa tafiti hizi sio kwa Tanzania tu, ni nchi 15 ambazo zinashiriki katika tafiti hizi na ndani ya tafiti hizi Mhe. Mwenyekiti, ndimo ambamo tunapata misaada ya kuweza kutusaidia na sisi kujiendesha, na ndani ya tafiti hizi kuna pesa za serikali lakini pia kuna pesa ambazo wanatupa wenzetu wafadhili ili kuhakikisha kwamba tafiti hizi zinafanikiwa.

Sasa naomba Mhe. Mwenyekiti, na hii aliyoizungumza ya malipo ya kujikimu na malazi shilingi milioni ishirini, bila shaka Mhe. Mjumbe anajua maana ya tafiti zinakusanya watu wengi, kuna wengine watatoka Pemba ambapo tutakuja kufanya majumuisho ya pamoja hawa wanahitaji gharama za kulala na kula. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Mjumbe hili atukubalie na wala hatukuliweka hapa kwa ajili ya kuvungavunga, tumeliweka hapa kama kufafanua kifungu kwa kifungu kwa mujibu kitavyotumika. Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuongeza maelezo ambayo Mhe. Naibu Waziri ameyaeleza vizuri sana. Kuna taasisi inaitwa SACMENT, SACMENT maana yake ni *Southern African* pamoja na *Eastern African Countries, Consortium for Monitoring Quality of Education*. Zanzibar ni miongoni mwa nchi nne za mwanzo zilizojiunga na taasisi hii katika miaka ya 1995. Bahati nzuri tumeendelea kuwa wanachama kama Zanzibar, na tukifika kule Ufaransa wakati ule na mpaka sasa hivi kinakuwepo kibao ambacho kimeandikwa Zanzibar kwa zile nchi nne. Baadae wenzetu Tanzania Bara wakajiunga mwaka 2001 wana kibao chao ambacho kinaandikwa *Tanzania Main land.* Kwa hivyo, hii ni taasisi ambayo imetupa heshima kubwa Zanzibar, na ni taasisi ambayo hayo tunayoyalilia tuyapate hii ni taasisi ambayo tayari tushaipata heshima hiyo Mhe. Mwenyekiti, na tunaendelea.

Mwaka 2009/2011 Zanzibar ilipata heshima ya aliyekuwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali akachaguliwa kuwa ndiye *President* wa Mawaziri wa *Eastern Central* pamoja na *Southern Africa,* kwamba aiendeshe taasisi hiyo kwa tokea mwaka 2009 – 2011. Kwa ninavyojua uendeshaji wa shughuli hii Mhe. Mwenyekiti, hizi pesa zilizowekwa basi ni kidogo na tunahitaji kuwaonea huruma Wizara ya Elimu tuwaongeze pesa hizi.

Mhe. Mwenyekiti, katika utaratibu huu kabla ya kufanyika vikao hivi kunakuwa na *coordinators* inabidi waende wawili, watatu mpaka wanne. Safari ya kutoka hapa mpaka Ufaransa ile tiketi yake ni gharama kubwa haipungui US$ 2000. Mimi namuomba sana Mhe. Ismail Jussa kutokana na hali halisi ya taasisi hii bado tunahitajia kuionea huruma Wizara ya Elimu, na wawaruhusu ili tuweze kuendelea. Kwa sababu pesa nyingi zinahitajika na mambo mengi, na hii ni heshima kwa Zanzibar tukijitoa tunajipunguzia heshima yetu katika taasisi za nje ambazo kila wakati sisi tunalilia tupate heshima hizo. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, maelezo ya Waziri wa Elimu mstaafu anayeipenda Wizara hii nimeyasikia, lakini bado sijaridhika. Nina sababu zangu Mhe. Mwenyekiti, kwanza taarifa nilizonazo kwamba katika Kamati lilipohojiwa hili awali tulitolewa maelezo tofauti na haya yaliyotolewa hapa, kamati husika ya sekta kwamba hapa zimewekwa katika posho kwa sababu hii ni idara inayosimamia miradi tofauti, kwa hivyo inashiriki katika vikao tofauti, kwa hivyo posho zake ikabidi ziwekwe hapa.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, mimi ninasema hoja ya kusema hesabu hizi zimekosewa, mimi ninavyoamini hili buku kabla hatujagaiwa sisi kwa utaratibu wa serikali makini ni lazima kwanza Mawaziri wameridhika, kwa sababu wao ndio wanaopanga watuletee hapa, chini ya *doctrine* ya *collective responsibility* kwamba wameridhika haya mafungu ndio tukaletewa Wawakilishi chombo cha kusimamia serikali.

Mhe. Spika, isitoshe hili buku baada ya kupewa wizara linakwenda katika kamati husika linakwenda katika kutetewa kabla hatujaanza kikao cha bajeti hapa. Sasa kama mapungufu haya yaliyoelezwa leo kuwa Wizara ya Fedha imekosea ikaweka hapa, mbona katika kamati ilipopelekwa hayakufanywa marekebisho haya. Marekebisho haya Mhe. Mwenyekiti, tumeanza kuyapokea baada ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuanza kuhoji vifungu humu ndani na vikaandaliwa vifungu gani ambavyo vinahojiwa Mhe. Mwenyekiti, ukakuta vile ambavyo vinakwenda kupunguzwa au kurekebishwa.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, nimeyasikiliza maelezo lakini bado mimi ninasema ninapata shida sana, ukiniambia kwamba kwa mfano hapa nitoe mfano mmoja tu kumeongezewa milioni thalathini katika gharama za vifaa, uchapaji imekuwa ni milioni arobaini na moja. Mhe. Mwenyekiti, kuna fungu huku la *stationaries* ambalo lipo vile vile na limeongezwa, na katika idara hiyo hiyo na lipo katika kila idara lipo, na kama kuhudumia wizara kuna Idara ya Utumishi na Uendeshaji ambayo pia yana mafungu yake, nayo pia kuna matatizo yake. Kwa hivyo ninasema bado Mhe. Mwenyekiti, nikishikilia maelezo haya hayanipi maelezo ya kunikinaisha hasa nikitizama kule zilikohamishwa zile mia na huku zilizopelekwa hayana mahusiano Mhe. Mwenyekiti.

Kwa hivyo mimi ninaamini kwamba fungu hili lilikuwa halihitajiki na ndio maana likapunguzwa kutoka lilikokuwepo kwenye malipo baada ya saa za kazi kutoka milioni mia moja na kumi na sita hadi zikafanywa kumi na sita. Na niulize Mhe. Mwenyekiti, labda hilo nisaidiwe la mwisho ili nikae kitako tena.

Hivi katika marekebisho Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Fedha inakosea katika hizi *round figure* za mwanzo tu, maana yake huku kwenye nambari kwa mfano ina watoto, ilikuwa ni milioni mia moja na kumi na sita laki tano, tisini na tisa elfu, huku mwisho hakukosewi huku kumi na sita, nambari zinabaki vile vile lakini kwenye haya ma-*round figures* mia, hamsini, thalathini ndiko kunakokatwa. Sasa Wizara ya Fedha hiyo ndio inakosea katika kuweka haya majumla tu, hivi kwenye vitoto vyake vikawa havikosewi. Maelezo hayaridhishi naomba maelezo ya ziada, la si hivyo kama hatuelewani ninafikiri tutafute utaratibu wetu wa kupiga kura wa kuzipunguza, nitaomba wenzangu waniunge mkono tupunguze fungu hili Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Kabla sijawaomba wahusika Mhe. Waziri na Naibu Waziri, mimi ninadhani tungeangalia hoja, moja kwa sababu maelezo yako Mhe. Jussa yana hoja mbili kubwa.

Kwamba matumizi haya kwa mujibu wa matumizi yaliyotoka hapa hayakutawanywa kwenye vile vifungu ambavyo hasa vinavyohusiana na jambo hilo. Hiyo ndio hoja moja wapo.

Lakini hapa tuangalie msingi wa hili jibu lilivyotoka, kwamba ipo haja ya kuendelea kushiriki katika mikutano ambayo Mhe. Waziri na Naibu Waziri na Waziri wa zamani wa Elimu wameyatoa kwa madhumuni ya kuendeleza elimu ikawa ya *quality* zaidi. Hilo ni suala muhimu.

Sasa kama hili, zipo taarifa kwamba hilo jambo sio kweli, hapo sawa na sisi kwenye Kamati hii ni sawa sawa na vile tunavyotunga sheria. Mhe. Jussa ungeweza ukasema hapana hili kwa umuhimu wa hili jambo lenyewe lilivyo, jee fedha ninasema ingewekwa kwenye kifungu kadhaa, ni jambo la kawaida ingewezekana sana hilo. Kama vile unavyosema maandishi ya kifungu fulani ingekuwa tunazungumza mswada, haya mimi naomba tuyarekebishe yasomeke kwa utaratibu kama ufuatavyo.

Mimi Mheshimiwa wangu Jussa ni mtaalamu wa hayo na wakati mwengine huwa unaniletea pale juu, kwamba kifungu hiki kisomeke namna hii. Sasa na hapa kazi ni ile ile badala ya kwamba tunatunga mswada wa sheria, hapa ni mswada wa matumizi.

Kwa hivyo kama hii hoja ya kwamba jambo hili la kuhudhuria mikutano lipo kweli na inavyoonekana lipo, basi haja ya matumizi hayo yapo. Wapi tuweke hilo ni suala jengine. Kama hapa sipo labda tungesema tu wapi palipo sahihi, lakini tukiangalia maelezo yaliyotoka weka fedha kwenye kifungu cha safari sawa, weka fedha kwenye kifungu cha kujikimu sawa, kuweka fedha kuhusu masuala ya uchapaji inaingia akilini na hata viburudishaji kama wageni unapata unafanyaje.

Mimi ninadhani tungekubaliana tu kama kuna tatizo la sehemu ya fedha imekwenda kwenye kifungu sicho, tupendekeze basi kwenye kifungu gani lakini kimatumizi haja ya jambo hili ni muhimu.

Kwa hivyo labda nimemuona Mhe. Mwenyekiti pale atatusaidia.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Mhe. Mwenyekiti, na mimi ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kutoa majibu ya nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, nikiri kwamba Kamati yetu ilikaa na kupitia, lakini pia nikiri katika Baraza hili tulikuwa na wasi wasi kama walivyokuwa na wasi wasi Waheshimiwa Wajumbe wako wa Baraza la Wawakilishi, lakini mwisho wake tuliwafahamu wizara na pia tulijua umuhimu wa kupitisha fungu hili kwa sababu sote tunafahamu kwamba elimu sote tunaihitaji, lakini pia tunahitaji kwamba Wizara ya Elimu misaada mbali mbali kutoka kwa nchi za wenzetu.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa ninataka kuongezea hayo tu, niseme kwamba na sisi Kamati yetu tulikuwa na hofu hiyo kama walivyokuwa na hofu Waheshimiwa wenzangu, lakini mwisho wake tuliwaelewa wenzetu hawa na tulijua ipo haja ya kugaiwa vifungu hivi. Ninakushukuru Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ninadhani Mhe. Jussa sasa tupo pahali pazuri.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, ninasikitika hatupo pahala pazuri kwa sababu nimepekua sana na ninafikiri ninajitahidi sana kusoma sijawahi kuona Kanuni hata siku moja humu kwamba Mwenyekiti wa Kamati naye anajibu hoja za Waziri.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, ninachosema ni kwamba kama nilivyosema mimi ninavyoelewa na kuna siku ilitangazwa hapa, nilitoa hoja yangu kwamba buku hili lilitolewa mwanzo na mimi ni Mjumbe wa kamati yangu vile vile.

Lakini baada ya kuridhika haya ndio yakaletwa hapa, haya marekebisho yamekuja baadae, na tulisikia kwenye tangazo kwamba kamati inaitwa baada ya kuanza kuhoji hapa. Tulipokuwa tukitoa mwanzo hapa kwa sababu kamati inaweza kuwa haijui, lakini wizara inajua iliomba nini, kama Wizara ya Fedha ilikosea, wao wizara kwa sababu katika kupitisha hapa wapo peke yao, watendaji wao wapo juu lakini kwenye kamati wao na watendaji wao wapo pamoja, na wao wote wanaruhusiwa kujibu hoja za Wajumbe Mhe. Mwenyekiti.

Sasa mimi ninasema kama ilikuwa Wizara ya Fedha imekosea humu katika hili buku kubwa Mhe. Mwenyekiti, hivi wao Wizara hawakuyaona hayo makoseo. Kwa nini walipokwenda ku-*defend* bajeti yao katika kamati mara ya mwanzo hayakurekebishwa kwamba Wizara ya Fedha imekosea haya mafungu sio, marekebisho haya yamekuja baada ya Wajumbe kuanza kuhoji mafungu ya wizara nyengine Mhe. Mwenyekiti.

Na hapa Mhe. Mwenyekiti, naomba nitoe angalizo kwamba kuanzia mwakani utoe onyo hapa kwamba marekebisho yote yakafanywe baada ya kumaliza kazi za kamati katika buku hili tuletewe hapa, lakini huu utaratibu kwamba unangoja mwenzako kahojiwa vipi halafu na wewe unaleta marekebisho hapa, kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, unaongeza walakini na masuala kuliko kujibu hoja hapa.

Kwa hivyo nimemsikia Mhe. Mwenyekiti lakini ninachosema na kusikia hayo maelezo yako Mhe. Mwenyekiti, kwamba labda yangehamishiwa pahala pengine. Mhe. Mwenyekiti, ukiniambia hapa hapa labda majibu haya wizara kwa kamati, labda kamati ingesaidia na wanao Wajumbe makini tu wangeweza kuwasaidia wapeleke wapi, lakini hapa kwa hapa kuniambia niyapeleke wapi, mimi nitajiuliza kwa sababu ukiniambia niyapeleke kwenye fungu la safari lilikuwepo fungu la safari, kama kulikuwa na fungu la mafunzo lilikuwepo fungu la mafunzo Mhe. Mwenyekiti, kama malipo ya kujikimu lilikuwepo.

Halafu vile vile hayo malipo ya kujikimu Mhe. Naibu Waziri ananiambia kwamba zimeongezeka kwa sababu ya safari, zile ishirini zikabandikwa pale zikawa ishirini na tisa, lakini huku kwenye safari kuna gharama za hoteli huku, *boarding* and *lodging* na zimeekewa fungu lake vile vile.

Ndio maana mimi ninasema haya mafungu hayawiani Mhe. Mwenyekiti, ni kama vile kwamba yanalazimishwa kubandikwabandikwa mwahala mwengine ku-*justify* matumizi. Sasa Mhe. Mwenyekiti, hizi ni fedha za walipa kodi wa Kizanzibari, hawa maskini Mhe. Mwenyekiti, wanaoteketea katika ajali kwa sababu serikali haina fedha ya kununua meli lakini pesa kutoa za namna kama hii zipo.

Naomba sana Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema hili au labda kwa sababu kwa kuheshimu kiti chako niombe kitu kimoja. Kama tulivyofanya kule kwengine, kwa hili na mengine nitaendelea kuyahoji ndio kazi yangu niliyoletewa hapa Mhe. Mwenyekiti.

Lakini kwa hili tukubaliane kwamba likae *chanisi* kwanza katika Wizara ya Fedha, tulifanya hapa katika wizara moja, tupate Wizara ya Fedha ijiridhishe na wao wapeleke matatizo yao na kamati baadae Wajumbe na sio Mwenyekiti mmoja, ninasema ni Wajumbe wa kamati waridhike kwa niaba yetu kwamba kweli fungu hili linakwenda kufanya kazi ambayo iliyokusudiwa. Tukikubaliana hivyo Mhe. Mwenyekiti, na nitakubali ninaliweka *chanisi*. Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ninakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa na moja tu la kuongezea.

Mhe. Mwenyekiti, ninasema Mhe. Mwenyekiti wa kamati amethibitisha kama haya marekebisho tumeyapeleka katika kamati, na Mhe. Mwenyekiti ni lazima tukiri kama upitishaji wa bajeti wa mara hii, sio kama wa miaka ya nyuma, ni tofauti.

Miaka ya nyuma ilikuwa tukipitisha kifungu kimoja kinakwenda moja kwa moja, lakini mara hii kifungu kinakwenda *item* moja moja. Sasa tulipoona ule mtiririko wa wenzetu ulioanza kama nilivyozungumza hapo awali, tukaona na sisi tujirekebishe ili tusiwape Wajumbe wako wa Baraza la Wawakilishi tatizo.

Sasa anasema haya ambayo tumeyazungumza, hizi *items* ambazo tumezungumza kwamba tutatumia na kwengine zipo ni kweli Mhe. Mwenyekiti, lakini hizi tumesema ni *special* kwa ajili ya utafiti. Kwa hivyo kama kuna maji na vinywaji ipo kweli lakini kwa masuala ya uendeshaji wa kawaida. Hii ambayo inayoonesha hapa ni kwa ajili ya huu utafiti.

Tunamuomba Mhe. Jussa hili halimalizi hapa, linamaliza mpaka ufuatiliaji wa Wajumbe wa kamati. Atuachie tuendelee nalo kwa sababu ni jambo muhimu Mhe. Mwenyekiti, sisi tupo kwenye dunia, hatupo nje ya dunia. Hizi tafiti zinatusaidia kujipima wapi tupo na wapi tunataka kwenda. Hii ni tafiti ya tano Mhe. Mwenyekiti, zile za nyuma zilionesha kama Zanzibar tupo kati kwa kati, hatupo chini wala hatupo juu. Kwa hivyo inatuwezesha kujipanga upya na kwenda kwa *speed* zaidi.

Kwa hivyo ninamuomba Mhe. Jussa hili atuachie, kamati itafanya kazi yake ya kufuatilia, kama ni kweli haya ambayo tumezungumza ni sawa, kama ni uongo atakuja kutukamata hapa hapa kutusuta. Ninakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mimi ninafikiri tukubaliane na mashauri yaliyotoka Kamati isaidie kufuatilia suala hili lakini hili fungu Mhe. Jussa tukubali tuendelee nalo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema sisi kazi yetu hapa na ndio maana tunaita Kamati ya Matumizi ni kusimamia fedha za walipa kodi wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nilitoa maelezo na mwisho wa maelezo yangu nilikuwa nishaisaidia Wizara, nimesema ninakubali kwa sharti moja na tushafanya hivyo kwa wizara zilizopita, kwamba tuliachie lakini tuliweke chini ya dhamana ya wizara, kwa bahati mbaya leo Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo sasa hivi hayupo lakini bahati nzuri yupo, kabadilisha upande tu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa bahati nzuri Mheshimiwa mwenyewe yupo, mimi ninasema ninakubali, labda nilikuwa sijasema ninakubali tuendelee, lakini kama nilivyosema kwamba kwa utaratibu kama tulivyofanya katika wizara ile kwamba hili, kwa sababu hata tukiidhinisha hapa bado wanaotoa fedha ni Wizara ya Fedha, kwa hivyo ninakubali tuliidhinishe lakini baada ya Wizara ya Fedha kuridhika kwamba haya matumizi yaliyotajwa ndio na kamati nayo kuridhika kama mafungu haya yanakwenda kutumika kwa kazi hiyo ya utafiti tukijaaliwa. Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, ninasema tuendelee ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, mimi nimemfahamu sana Mhe. Jussa maelezo yake.

Lakini vile vile pamoja na maelezo mazuri ya Mhe. Waziri pamoja na Naibu Waziri, mimi ninataka nikubaliane na Mhe. Jussa kwamba atuachie tutafanya kazi kwa karibu zaidi na Wizara ya Elimu tuone kwamba hizi fedha zitatumika kwa malengo yaliyokusudiwa ili yasije yakatumika vyenginevyo.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru na mimi nipo kwenye fungu hilo hilo la Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yako hii inafanya kazi muhimu sana, na uzuri kwamba tunafanya kazi kwa uchanganuzi wa kimafungu, fungu kubwa na hivi vifungu vidogo vidogo. Sasa ili tufikie pahala kwa kweli tukubaliane kuipitisha bajeti maana yake ni lazima Baraza hili, Wajumbe tupate maelezo ya kina ili tuwafanyie haki wananchi wetu.

Mimi wakati ninachangia Mhe. Mwenyekiti, kwanza ninaomba muongozo wako kwamba Mhe. Waziri hapa alikiri kuwa vifungu vimekosewa. Sasa ikiwa vifungu vimekosewa, maana yake hata lile fungu kubwa tunalotaka kuja kulikubali katika kila fungu, ina maana litakuwa halina uhalali kwa sababu yeye mwenyewe kakiri.

Sasa ikiwa vifungu vinakosewa na yeye akataka Wizara ya Fedha ivifanyie marekebisho. Sasa hapa tunakuwa tunapitisha mafungu gani. Kamati yako hii ina mamlaka ya kupitisha mafungu yaliyokosewa. Hilo lilikuwa ni moja.

Lakini nitakapojibiwa hilo na mimi niliomba nipatiwe ufafanuzi kwamba kuna vifungu nilivihoji ili nikitegemea kwamba hapa nitapata majibu yake. Kwa mfano kuna fungu la ushauri nasaha mwaka jana walitoka kwenye shilingi milioni sitini na tano hadi milioni mia mbili na ishirini wanazozitaka sasa. Voti hiyo hiyo ya Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.

Milioni sitini na tano ….

Mhe. Mwenyekiti: Kasma yenyewe hebu

Mhe. Omar Ali Shehe: Ni hiyo hiyo 0405 kifungu kidogo cha 272100 ukurasa wa 6.

Mhe. Mwenyekiti: 272100 ndio

Mhe. Omar Ali Shehe: Nilihoji ilikuwaje zitoke ule ushauri nasaha ni ushauri nasaha gani wanaopewa wanafunzi.

Kwa mwaka jana kutumia shilingi milioni sitini na tano hadi mara hii kutaka milioni mia mbili na ishirini. Nilitaka maelezo ili tukubaliane, vyenginevyo kama hakuna maelezo basi tuidhinishe zile za mwaka jana kwa sababu kuidhinisha fedha hizi hizi ni nyingi, na hii hatuioni hasa ile *impact* yake iliopo.

Lakini vile vile nilihoji suala zima la vinywaji ambapo ilitoka kwenye milioni mbili hadi ishirini na tano, hizi ni fedha nyingi sana vinywaji, tunakunywa vinywaji gani huko? Na kwa nini mtu asinywe chai kutoka kwake mpaka akaja akanywa chai ofisini siku hizi.

Sasa hizi hazikubaliki tunahitaji maelezo ili tupate Baraza lako lipitishe. Mhe. Mwenyekiti, ninahitaji maelezo vyenginevyo basi tukubaliane basi ile hoja ya kwanza ni uhalali gani kupitisha vifungu kwenye Kamati hii ambayo vifungu vimekosewa.

Lakini kama si hivyo basi tukubali kwamba hii bajeti kwa kweli tuungane na Mhe. Jussa kwamba tupunguze fungu hili ili twende vizuri, na fungu hili tulipeleke pahala kunakohitajika zaidi.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ninakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kujibu.

Katika majibu ya Waziri na maelezo yangu tulisema kama vifungu vimekosewa lakini sio kukosewa kihesabu. Kilichokosekana ni *heading*, ni majina ndicho ambacho kimekosewa si vifungu vyenyewe.

Hiki kifungu Mhe. Omar kweli alikitolea ufafanuzi lakini hiki kifungu kimeandikwa na kitazameni kwa uzuri, ushauri nasaha/vitengo. Kwa hivyo hii ushauri nasaha inajumuisha na vitengo.

Mhe. Mwenyekiti, tuna vitengo sita ambavyo vinne vipo chini ya Katibu Mkuu, viwili vipo chini ya Kamishna. Katika mgawanyo wa pesa hizi, elimu mjumuisho ni milioni sabini, uhasibu ni milioni thalathini, ukaguzi wa ndani ni milioni thalathini, ununuzi na ugavi ni milioni thalathini, uratibu wa elimu ya juu milioni thalathini, habari, elimu na mawasiliano ni milioni thalathini.

Jumla ya pesa kwa vitengo hivi vyote pamoja na huu ushauri nasaha Mhe. Mwenyekiti, inakuja jumla ya milioni mia mbili na ishirini. Ninakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, mimi sijafahamu hivyo vitengo ni vitengo vya kufanya kazi gani. Hivyo vitengo shughuli yake nini. Maana yake hapa hili fungu la ushauri nasaha kwa wanafunzi *stroke* wa skuli, sasa hili ndio fungu. Sasa sijui hivyo vitengo ndio navyo vinapewa ushauri nasaha.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mjumbe kwamba vitengo ni *division*, ambavyo tumesema vipo chini ya Katibu Mkuu na chini ya Kamishna.

Kwa hivyo hivi vitengo tumeviweka kwenye hili fungu moja la ushauri nasaha/vitengo, na pesa zake ni hizi hapa nimezitamka na tuna vitengo sita. Elimu mjumuisho na stadi za maisha hata kwenye kitabu chetu akitazama kimo, uhasibu upo, ukaguzi wa hesabu za ndani upo, ununuzi na ugavi upo, uratibu wa elimu ya juu kipo, habari, elimu na mawasiliano pia kipo.

Vyote hivi ni milioni thalathini thalathini isipokuwa elimu mjumuisho na stadi za maisha ni milioni sabini. Jumla inakuja hiyo milioni mia mbili na ishirini.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, mimi ninaamini kwamba na hivyo vitengo kwenye bajeti ya mwaka jana vilikuwepo. Hoja yangu ni kwamba kwa nini zikatoka sitini na tano hadi mia mbili na ishirini. Kuna kitu gani kilichokosekana mwaka jana, kilichopelekea mara hii fedha hizi ziongezeke kwa kiwango hicho kikubwa.

Hiyo ndio hoja yangu kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, mimi ninataka nikwambie sisi katika Kamati yetu ya kuchunguza mahesabu, haya mambo haya tunakumbana nayo na ndio ile mara zote tunapopiga kelele kwamba kuna *re-allocation*, ni kwamba fedha zinawekwa pahala hazina matumizi badala yake watu wakazifanyia *re-allocation* wakazipeleka sehemu nyengine.

Hii ndio maana yake. Sasa hapa tunachohitaji ni maelezo vyenginevyo basi tukubaliane tuzirudishe zile zile za sitini na tano za mwaka jana, hizi nyengine zilizozidi tuzipeleke sehemu nyengine.

Mhe. Mwenyekiti: Maelezo ya Mhe. Naibu Waziri yapo wazi kwamba kuna vitengo na kwamba kila kimoja matumizi yake yamesemwa, isipokuwa labda sasa tupate maelezo juu ya hili ambalo Mhe. Omar umeliuliza. Nini kilichokosekana mwaka jana mpaka mwaka huu ikabidi pesa zikawa hizo. Yaani huko mwaka jana ilikuwa kuna nini, labda tupate maelezo juu ya hili.

Mwaka jana ilikuwaje mpaka ikawa milioni sitini na tano, kitu gani kilikuwa hakikufanyika huko.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, mwaka jana fungu lilikuwa ni sitini na tano milioni. Hizi ndizo fedha ambazo tulizozipata lakini Mhe. Mwenyekiti, kwa mahitaji ya ushauri nasaha kwa mwaka huu ni mkubwa. Wewe mwenyewe utakuwa ni shahidi wa hayo.

Waheshimiwa wanavyozungumza namna ya maadili yetu yanavyoporomoka katika skuli zetu, watoto wetu wanabakwa, mimba za utotoni zimekuwa nyingi. Juzi hapa Mhe. Mtumwa katika kuchangia alisema kuna skuli tatu ambazo zina vitendo viovu. Sasa hizi kwa ushauri nasaha kuna walimuu wapo kila skuli, kwa hivyo hawa tunawatayarishia semina.

Hizi pesa mara hii tumeziweka kutokana na hayo matendo yamekuwa makubwa, ule ushauri tu unaotoka ofisini unakuwa hautoshi, sasa tuwafuate katika maskuli kuhakikisha kama ushauri huu tunawapelekea, na wale walimu ambao wapo katika maskuli tunawawezesha basi kuweza kukabiliana na hivi vitendo na haya matendo ambayo yanayotokea.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, katika bajeti hii kuna mafungu ya mafunzo. Tukimaanisha mafunzo ndio hayo semina. Sasa leo tushakuja tena kwamba haya ushauri nasaha ndio mafunzo, sasa tunachukua lipi.

Kwa sababu katika bajeti hii kuna mafungu maalum ya mafunzo, tukimaanisha ndizo hizo semina tunazozikusudia. Sasa mimi bado Mhe. Mwenyekiti, ninahisi bado hili ni fungu kubwa tulikate tubakishe hili la mwaka jana.

Lakini vile vile kuna hoja ya vinywaji tunahitaji maelezo.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na maelezo mazuri yaliyotolewa na Mhe. Naibu Waziri, mimi naomba niongezee maelezo kidogo ya nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, serikali hivi sasa imeweka utaratibu mzuri unajulikana kama bango kitita. Utaratibu huu kila Wizara inatakiwa kupeleka shughuli zake wanazozifanya na matumizi yake kila baada ya miezi mitatu kwa Mhe.Rais.

Kutokana na utaratibu ule wa bango kitita Mhe. Mwenyekiti, umewezesha wizara kuelewa mapungufu yake mbali mbali ambayo huko nyuma yakisababisha sana kuwa na *re-allocation*. Sasa katika kuepuka hilo kila Wizara inafanya tathmini ya kina katika kuhitaji matumizi yake.

Ndio maana ukaona sasa matumizi yetu yanapanda zaidi kwa sababu tunakwenda na uhalisia wa mambo. Utaona mafungu mengine matumizi yanashuka sana kwa sababu mahitaji kule huwa hayahitajiki sana kutokana na uzoefu tulioupata katika suala zima hili la bango kitita.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, Waheshimiwa Wajumbe waelewe kwamba zinapokuja tofauti kubwa si kwamba tume-*inflect* tu lakini nia yetu ni kwa sababu tumefanya tathmini zaidi inayoonesha mahitaji ya fungu hilo, ndio matokeo yake yanakuja namna hiyo.

Kwa hivyo naomba sana watuelewe kwenye hilo na pale ambapo tunapoona pana kasoro huwa tunakubaliana na Wajumbe, lakini kwenye fungu hili suala la ushauri nasaha ni suala mbali na mafunzo ni suala mbali, na kwa hali yetu na kwa matatizo yaliyojitokeza kwenye Wizara hii ya elimu Mhe. Mwenyekiti, mimi ninawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe kwamba tukubaliane tuwape nafasi hii Waheshimiwa wakafanye kazi hii, kwa sababu yanahitajika mambo haya na yametokezea mambo mengi hapa ya kubakwa na kadhalika.

Kwa hivyo Mhe. Naibu Waziri kaeleza vizuri naomba sana Waheshimiwa wenzangu tukubaliane fungu tuendelee, na pale ambapo patakapoonekana pana kasoro za kweli kweli, basi tunakubali kujirekebisha. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, mimi sina matatizo kwamba tusiendelee ninataka sana tuendelee. Tunafanya hivi Mhe. Mwenyekiti, kuwapunguzia wao kazi, kwa sababu Kamati tumeshapita na tushashuhudia kwamba haya tunayoyaidhinisha, tukifika katika ukaguzi huko kufuatia ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ni vitu tofauti kabisa.

Sasa tunaeleza hivi ili kupeana indhari mapema kwamba kesho na kesho kutwa, leo zinaidhinishwa fedha kiwango hiki, kamati zisije zikapita zikaambiwa aah! Fedha fungu fulani zimefanyiwa *reallocation* likenda pahala fulani, ndio maana yetu kwa kweli. Au tukataka matumizi, tupeni matumizi haya, ikawa hakuna ushahidi ni kubabaishana, ndio maana yetu. Sisi kila wizara na idara hizi zikipewa mafungu, sisi ndio tunafurahi vizuri zaidi. Lakini kwa kuwa tunakuwa na indhari, ndio maana kwa kweli tukawa makini katika hili. Kwa hivyo, madam hili tumeshakubaliana mwanzo, kwamba litakuwa chini ya uangalizi wa Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, niungane na hilo, tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, tunaendelea, lakini kuna maelezo kidogo ningeomba niyatowe, ili kusakafia pale ambapo tumefikia. Mnajua kunapokuwa na matumizi ambayo ni mapya sio jambo la ajabu sana, suala muhimu ni kusimamia hayo matumizi, hilo ndio suala muhimu.

Kwa mfano, tungesema turudishe ule mfano wa milioni 65 turudishe hapo, bila shaka kwa thamani yetu ya shilingi hata hizi zitakuwa hazitoshi, *inflation* inazidi kila siku kwa matumizi mbali mbali. Kwa hivyo, mimi nadhani ni kusimamia matumizi, ilimradi serikali imetoa maelezo juu ya matumizi na usahihi wake watakavyotumia. Sasa kazi iliyobaki na ndio kazi yetu ya kamati ni kuja kuona je, yale matumzi ambayo tulihoji kwamba yatatumika kwa ajili ya jambo fulani, yametumika kweli. Ndio hiyo uliyosema sasa hivi kwamba ok, basi tuyafuatilie ili tuone baadae je matumizi haya yamekwenda sawa. Hiyo ndio kazi ya kamati zote kimsingi, hatimaye hata zaidi kamati ambayo wewe Mhe. Omar Ali Shehe unaiongoza.

Kwa hivyo, nadhani hizi hoja zinazojitokeza tokeza, wenyeviti wa kamati na wajumbe wengine tuwe macho tu-*pick* kutoka hapa kwamba kipindi kinachokuja tunakwenda kufuatilia jambo hili. Kama tutafuatilia mafunzo yetu ndio yale tuliyosema kwamba unapokwenda katika kamati kufuatilia utekelezaji, fanyeni utafiti kutokana na *Hansard* zetu hizi.

Mfano, Waziri kaeleza nini juu ya matumizi fulani, ili hatimaye sasa unakwenda kule uwe na hoja ya kutosha. Waziri alisema kwamba pesa hizi zitatumika kwa jambo moja, mbili na tatu. Je, zimetumika kweli na hiyo kazi imefanyika. Hilo ndio suala ambalo litasaidia kuona kwamba matumzi haya yametumika vilivyo na ile kazi ya Baraza yenyewe itakuwa imetimia katika usimamizi wa matumizi haya. Tunashukuru Mhe. Omar Ali Shehe tuendelee. Eeh! Mhe Salmin Awadh hoja ya mwisho.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii na mimi nikajenga hoja katika idara hii ya mipango na sera. Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia hotuba hii ya Mhe. Waziri nilizungumzia juu ya kukerwa na tabia ya wizara hii ya kutoa taarifa juu ya wanafunzi waliokuwa hawastahiki kufanya mtihani wa *school candidate* badala yake kupelekwa kama ni *private candidate* kwa dakika za mwisho wakati tayari wameshafanya usajili kama wao ni watahiniwa wa *school candidate*.

Nashukuru Mhe. Naibu Waziri hapa amenileta waraka huu ambao umetoka Baraza la Mitihani la Tanzania unaoelekeza hivyo. Ni waraka wa kisheria ambapo kwa mara ya kwanza umewasilishwa kwetu tarehe 25/01/2010 ambao unatoa maelekezo hayo. Lakini ukakumbushiwa tena tarehe 02/04/2012.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naona utaratibu huu sio muafaka pamoja na kwamba sheria imepitisha. Lakini hoja yangu ni kwamba kwa nini Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali haitowi taarifa hii mapema na kuwajulisha wanafunzi ambao wanahitaji kufanya usaili wakajua mapema, kwamba mtoto mwenye umri wa zaidi ya miaka 24 haruhusiwi kufanya usaili kwa kutumia hii mitihani ya skuli za kawaida na badala yake anatakiwa aende kufanya usaili kwenye skuli za *private*. Kwa nini wizara imekuwa kimpya mno wakati jambo hili lipo na ni la muda mrefu na limepitishwa kwa mujibu wa sheria, kwa nini mnakua hivyo.

Kwa nini wanafunzi wanafika pahala wanalipa fedha kwa ajili ya usaili kama *school candidate*, baadae wanawaandikia barua dakika za mwisho kwamba watafanya mitihani yao kama *private candidate* na kwa nini kuna baadhi ya wanafunzi wanakuwa ile miaka 24 kwa mujibu wa miezi yao ambayo wamezaliwa, wao wanauchukulia mwaka badala ya kuchukulia ule mwezi na kufika mpaka wakati wa kufanya mtihani wanakuwa hawajatimia miaka 24, lakini wanawaandikia barua kwamba wafanye mitihani ya skuli za *private candidate* kwa nini.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Salmin Awadh Salmin katika kuchangia alilizungumza hilo na mimi katika majumuisho yangu ya kumsaidia Mhe. Waziri kujibu hoja, Mhe. Mjumbe nilimjibu hilo pia.

Mhe. Mwenyekiti, hiyo tarehe 04 ambayo ameisema ya mwezi wa 12, ndio Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ilitowa barua ya kupeleka maskulini kwa ukumbusho. NECTA wenyewe

hiyo walituletea sisi Wizara kwa ukumbusho. Hiyo barua tulitoa sisi baada ya kupokea hiyo barua ya NECTA kwa ukumbusho, kuwakumbusha walimu kama wanafunzi wa miaka 24 kuanzia hapo wanatakiwa wafanye mitihani ya *private*.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, barua ambayo amenipa hapa, ina nembo ya Baraza la Mitihani la Tanzania. Hii barua ambayo anasema wameitoa kwa ukumbusho, lakini ina *letter head* ya Baraza la Mitihani la Tanzania. Sasa sijui kama Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali wanatumia nembo hii kupeleka katika maskuli yao. Ndio maana nikasema kwamba hii barua inaonekana imetoka Baraza la Mitihani la Tanzania, lakini Mhe. Naibu Waziri anasema kwamba ni wao wamewaandikia katika skuli mbali mbali, ili kuwakumbusha.

Sasa mimi Mhe. Mwenyekiti, sina tatizo na hili, lakini hoja yangu ni kwamba kwa nini hawawaelezi wanafunzi mapema, kwa sababu barua hii mimi nasema imetoka kwenye Baraza la Taifa la Mitihani, haikutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kwa sababu ina nembo ya Baraza la Mitihani la Tanzania, kwa nini wanakuwa hawawakumbushi wanafunzi mapema, wakajua kwamba mimi mwaka huu nitafanya mtihani kama *school candidate* au nitafanya mtihani kama *private candidate*. Kwa nini wengine wanawapa barua ya kufanya mitihani ya *private candidate*, wakati umri wao haujatimia.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kama alivyosema Mhe. Salmin Awadh Salmin, barua ambayo nimempa yeye ni ile ambayo imetoka Baraza la Mitihani. Barua ambayo tumeitoa sisi kukumbushia, sikumpa nakala Mhe. Salmin Awadh. Kwa hivyo, hizo barua tumetoa na tumepeleka skuli zote za Unguja na Pemba. Nakala yake Mhe. Salmin Awadh kesho tukijaaliwa hapa nitampa.

Mhe. Mwenyekiti: Mimi nafikiri anachosema Mhe. Salmin Awadh tujitahidi iwe tunatoa taarifa mapema, ili wanafunzi wajijuwe kama wanaweza kufanya mtihani kama *school candidate* au *private candidate*. Hayo ndio maelekezo anayoyatoa. Mhe. Salmin Awadh.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Nina swali la mwisho nasema akinijibu nasema tuendelee. Kwa nini kuna wanafunzi ambao hawajatimia umri wa miaka 24 na wakawapa barua ya kufanya mitihani kama ni *private candidate* na umri huu wa miaka 24 ambao uko kwa mujibu wa sheria, kwa nini wakawapa hivyo. Akinijibu hilo basi nitasema tuendelee.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka moja alifahamu Mhe. Salmin Awadh kwamba sisi sio ambao tunaendesha mitihani hiyo. Sisi inatuhusu kwa sababu sisi ni Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na wanafunzi wetu wanafanya mitihani hii.

Lakini kwa mara hii Mhe. Mwenyekiti, kutokana na yale matatizo ambayo yalijitokeza Baraza la Mitihani tumekubaliana nao na tumekaa pamoja na Waziri wa Elimu wa Bara, kuhakikisha kwamba wanatushirikisha katika mambo yote ya mitihani. Kwa hivyo, hili Mhe. Mwenyekiti, tutalizingatia namuomba Mhe. Salmin Awadh atukubalie hili.

Mhe. Mwenyekiti: Tuambie Mhe. Salmin kwamba tuendelee.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Tuendelee.

Kifungu 0401 Idara ya Mipango Sera na Utafiti 1,444,000,000

Kifungu 0701 Idara ya Utumishi na Uendeshaji

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, na mimi kuweza kusema chochote katika yale niliyokuwa nikichangia. Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia katika kabrasha hili la Mhe. Waziri linasema kwamba hapa chini mwisho katika mabano, "rasimu ya maelezo ya bajeti inayozingatia au inayotumia programu".

Mhe. Mwenyekiti, sikutegemea kama hizi ndio wizara za majaribio ambazo bajeti yake zinaangalia programu, lakini bado katika mafungu hayatoshelezi. Ingawa tulipata maelezo ya Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwamba safari hii wanaangalia hali halisi, lakini kwa kweli hivyo vifungu tulivyokuwa tunaviona vinatuna havilingani na maelezo aliyoyasema. Lakini hilo tuliache kwa kuwa tumeshamuachia kazi Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, pamoja na idara yetu ya utafiti hapa Baraza la Wawakilishi kufuatilia hivi vifungu ambavyo tumevihoji baadae watuletee kwa ajili ya kulifanyia kazi. Nakuja katika suala langu.

Mhe. Mwenyekiti, katika idara hii ya Utumishi na Uendeshaji, nilizungumzia suala la wale wanafunzi ambao walipatiwa vyeti feki ili waweze kupata ajira. Wakati tukizingatia kwamba tunao walimu ambao wanasomea diploma na wengine digrii katika masomo ya sayansi ili waweze ku-*qualify* na waweze kuja kusomesha hayo madarasa ya sayansi. Lakini kwa bahati mbaya Mhe. Waziri pengine kutokana na muda, hakuwahi kueleza na yeye kuguswa na wale ambao wamefanya vitendo hivi na hatua gani za kinidhamu ataweza kuzichukua.

Sasa nilikuwa nahitaji nipate maelezo ili baadae kama yatanitosheleza tutaendelea, lakini kama hayajanitosheleza itabidi sasa Baraza lako hili likawatafute hao waliowatoza pesa walimu kwa ajili ya kuwapa vyeti ili wawe wenye sifa za kusomesha madarasa ya sayansi. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, naomba maelezo halafu baadae nitaangalia, ahsante.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kutoa maelezo ambayo Mhe. Hamza Hassan anayahitaji kuhusu vyeti feki.

Mhe. Mwenyekiti, wizara inakubali kwamba suala hili lipo, tumeliangalia na tumepata taarifa zake na hatimaye tumeweza kupata taarifa ambazo bado hatujaweza kuzithibitisha kwa maana ya kuchukua hatua za kisheria, lakini zinamuelekeo huo wa karibu utaweza kuthibitisha.

Kwa mfano, Mwalimu Mkuu baada ya sisi kusikia hii habari ya vyeti feki. Aah! Samahani ni Mkuu wa Chuo, nimemu-*approach*, akatuambia na yeye ana wasi wasi huo, kwa sababu katika stoo yake vyeti vimepungua. Sasa huo ni ushahidi ambao tumeukamata kwamba angalau kuna tetesi kwamba vyeti vimepungua. Lakini huyo Mwalimu Mkuu alitupa hint kwamba mwalimu fulani na mwalimu fulani ndio wanahusika. Sasa tumeanza kulifuatilia na pia kuna ile saini ya

Katibu Mkuu wetu imeghushiwa pamoja na muhuri wa kupigwa katika hivyo vyeti umeghushiwa, yaani umetengenezwa maalum.

Kwa hivyo, baada ya suala hili kuibuka hapa Barazani na baada ya kusikia hapa Barazani kwamba watu hao wanajulikana na ushahidi kamili upo. Sisi kwa heshima na taadhima, wale wajumbe waliosema wao wakiulizwa watawataja na ushahidi wanao. Basi watusaidie itafika pahala sasa, hawa jamaa kuwapeleka mahakamani, kwa sababu kosa hili la kughushi ni kosa la jinai, sio kosa jengine lolote, hawa moja kwa moja tunawapeleka mahakamani kuwashtaki.

Kwa hivyo, tunakamilisha ushahidi tukishautekeleza na tukisha utimiza pamoja na huo tutakaoupata hapa kwa wenzetu walioko Barazani, kutuambia fulani tumwite atusaidie, basi sisi tuliloliweka ni kuwapeleka hao jamaa mbele ya haki ili tupate maamuzi ya mahakama.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri alisema atawapeleka mbele ya haki, lakini mimi naomba awapeleke mbele ya vyombo vya sheria. Maana yake mbele ya haki mbali sana.

Mhe. Mwenyekiti: Hawatawaua.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, unajua Hansard ina matatizo yake. Anaweza mmoja huko siku ya pili ukamkuta kanyooka hivi. Wakasema Mhe. Waziri alisema atanipeleka mbele ya haki. Kwa hivyo, nadhani baadae Mhe. Waziri atakuja kurekebisha, najua aliteleza ulimi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nashukuru sana na vile vile bado nawashangaa sana watendaji wetu ndani ya Serikali. Yaani pamoja na kelele zote hizi bado wanaendelea kufanya mambo kama haya. Nadhani wanaona Serikali inasema tu haichukuwi hatua ndio maana ikafika pahala kelele zote za Baraza, tunasokotana na maswahib zetu kwa wao, bado wanaendelea kufanya vitendo kama hivi. Hebu naomba Mhe. Makamu wa Pili hayupo. Lakini naomba Serikali ione kwamba hawa watu iko haja sasa hivi, kama kauli aliyoizungumza Mhe. Waziri sasa hivi, ni kauli sahihi kabisa. Wakiwagundua tu wao wenyewe wawapeleke mahakakani.

Sasa kuna ombi nililiomba nilipokuwa nikichangia hoja hii, kwamba Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa kuna upungufu wa walimu wa sayansi na mpaka imefika pahala baada ya kuonekana pengo hilo, watu wakatengenezwa ili wawe walimu wa sayansi, lakini kuna vijana wetu ambao mwezi wa Oktoba keshokutwa wanategemewa wafanye mitihani. Hawa na wengine wameshaanza kuletewa vijibarua, wakimaliza tu kama wamefaulu basi waende wakajiunge na skuli kule Dar es Salaam za *secondary* kwa ajili ya kwenda kusomesha, na hawa wanalalamika kwamba basi angalau wizara ingeka nao angalau ikawapa moyo kwamba atakayefaulu, wataweza kumuajiri ili akasomeshe haya masomo ya sayansi.

Kwa hivyo, nadhani Mhe. Waziri huu ulikuwa ni ushauri wangu, kwa sababu hapa bila shaka kutakuwa kuna mapungufu, waliopata vyeti feki bila shaka watakuwa sio walimu wa sayansi, hawaku–*qualify*. Lakini lile pengo, mimi nadhani kwa kuwa wako hawa ambao wanaandaliwa, mimi nafikiri Mhe. Waziri ungewachukua ili baadae vijana wetu wakaendelea kupata moyo, na wengine wawe na moyo zaidi wa kujiunga na masomo ya sayansi ili kupunguza ile ya kuwaleta

Wanigeria na Wakongo na wengine kwa ajili ya kuja kutusomeshea wanafunzi wetu wa sekondari, ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nimshukuru sana Mhe. Hamza Hassan Juma kwa kuona umuhimu wa kuona vijana wetu wanaotumia gharama za serikali katika kuwasomesha, tunabaki nao ili wasichukuliwe na nchi jirani.

Mhe. Mwenyekiti, ninachoweza kumuhakikishia kwamba vijana hao wa sayansi wenye taaluma ya sayansi ajira zao ziko tayari. Baada tu ya kumaliza masomo tutahakikisha kwamba tunawa-*handle* wasitupenye kwenda kwenye nchi ya jirani hasa Tanzania Bara, ili waweze kusaidia kupunguza tatizo la uhaba wa walimu wa sayansi. Serikali katika mwaka huu wa bajeti imetenga ajira 1,000 kwa ajili ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Ni imani yangu kwamba kati ya hizo, asilimia 95 zitakuwa ni kwa ajili ya walimu na hasa kuzingatia hawa vijana wetu watakaomaliza masomo ya sayansi. Ahsante.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabla sijatoa hii hoja yangu, Mhe. Mwenyekiti, katika michango tunayotoa iko ile ya kuuliza maswali, iko ile ya kisera na iko ile ya vifungu. Sasa naomba Waheshimiwa Mawaziri wayachukulie kwa uzito, kila moja na uzito wake. Katika michango yangu mitano mimi niliyoitoa, limejibiwa moja tu. Lakini katika michango yangu hiyo niliyokua nikichangia kuhusu walimu waliotiwa saini kutoka Nigeria, nasikitika sana Mhe. Mwenyekiti, kwamba Mhe. Naibu Waziri alipojibu, alipotosha na akampotosha majibu ya Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sikuchangia kabisa kwamba walimu hawa wasiajiriwe au waajiriwe, hilo sikusema. Nimekwenda kutafuta *Hansard* hii hapa. Kwa hivyo, Mhe. Waziri ataisoma baadae. Nilichokizungumza katika maelezo yangu ni masikitiko yangu, kwamba nililinganisha mwaka ambao nilikuwa mimi *form five* na *six*, kwamba tukisomeshwa na walimu wa ndani na walimu wa nje. Lakini baada ya miaka 37 kuanzia pale, bado Zanzibar tunaagiza walimu wa sekondari kutoka nje, ndio masikitiko yangu mimi. Sikusema kwamba walimu wa Nigeria wasiajiriwe au waajiriwe na Hansard hii hapa, nimeiagiza Mhe. Mwenyekiti.

Kwa hivyo naomba sana tunapotoa michango yetu watujibu kama tulivyotoa na sio kupotosha. Mimi Mhe. Mwenyekiti, sina tatizo na uajiri wa walimu kutoka popote, ilikuwa ni sentensi moja tu ambayo ili-*include pronunciation* ya walimu kutoka Nigeria, ndio nikasema kwamba wapelekwe taasisi ili kuchekiwa zile *pronunciation* zao basi, lakini masikitiko yangu makubwa ilikuwa, je hali hii tuliyofikia tunaitathmini vipi kwamba baada ya miaka 37 ambayo nilikuwa na kipimo, Zanzibar tunaagiza walimu sasa kutoka nje wa sekondari na sio wa Chuo Kikuu.

Kwa hivyo, kwa hili baada ya Mhe. Waziri kukiri kwamba kapotosha tutaendelea. Pia nilichangia kuhusu walimu wale ambao wameshasomesha kwa muda, na katika uchunguzi wa Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora, waliona kwamba kuna kasoro ya vyeti. Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ikapeleka barua Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kwamba walimu hawa tumewakuta na kasoro katika vyeti vyao, kwa hivyo hawangestahiki kulipwa kiasi fulani. Niliuliza je kwa nini Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali haikuwaandikia barua kwanza wale walimu wao, inaonesha hii

tabia ya kuandika hawana. Kwa hivyo, kwa nini hawakuwaandikia wakenda kugundua kuwa mishahara yao imeshakatwa moja kwa moja. Jibu hili halikupatikana, kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri aniweke sawa hapo kidogo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri jaribu kusawazisha kauli ambayo yeye ameita upotoshaji, lakini labda imekosewa tu, upotoshaji pengine ni neno zito sana. Pia hili suala la kutowaandikia.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru. Wakati nikijibu swali hilo ambalo Mhe. Rashid Seif Suleiman alilizungumza la kuhusu walimu wa Nigeria, alikuwa sio Maalim Rashid tu ambaye alichangia suala hili, wako Waheshimiwa Wajumbe, ambao walichangia katika suala hilo, kwa hisia kali na wengine wakasema kama lafudhi zao na hata Kiingereza chao hawawezi kutamka vizuri. Lakini wengine Mhe. Mwenyekiti, walizungumza maneno ambayo sipendi katika Baraza lako tukufu niyarudie.

Kwa hivyo, nilijumuisha ile michango kwa wale ambao walichangia walimu wa Nigeria. Sasa Mhe. Maalim Rashid limemgusa kwa wale ambao na yeye hakulichangia kwamba hakutaka kwamba waajiriwe, basi namuomba radhi Mhe. Rashid Seif kwa hilo.

Jengine Mhe. Rashid Seif Suleiman, labda alitizama hili la kutaka nimuombe radhi tu, hakutizama lile ambalo nilimjibu la kuwa kama walimu hawa tuliwapa taarifa mapema. Nilizungumza Mhe. Mwenyekiti, kwamba mara tu baada ya marekebisho haya ya mishahara, tuliwatoa watumishi wetu kwenda katika mawilaya yote ya Unguja na Pemba, kukaa na walimu wakuu, kuwaeleza juu ya marekebisho haya ya mishahara na tukawaeleza kuwa mwalimu yeyote yule ambaye atahusika na kadhia hii, kama ni kuongezewa, kama ni kupunguziwa basi aripoti kwanza kwa mwalimu wake mkuu, halafu tutaletewa sisi wizarani. Walimu wengi Mhe. Mwenyekiti, walifuata utaratibu huo na tuna barua nyingi tu ambazo tayari nyengine tumeshazipeleka utumishi na nyengine ambazo tunazifanyia utaratibu wa kuzipeleka utumishi, nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, hili suala alilojibu mwisho mimi sikumfahamu, kwa sababu mimi nilitaka kujua tu kwamba waliwapelekea barua kabla ya kuwapelekea barua kabla ya kukatwa mshahara, kwamba nyinyi kwa mujibu wa uchunguzi uliofanywa na Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora, mmegundulikana kuwa na vyeti ambavyo sivyo ama hivi na hivi. Kwa hivyo, mshahara wako kwa mwezi wa Mei utakuwa kiasi kadhaa, waliwapelekea barua na kwa sababu mwalimu yuko chini ya mwalimu mkuu, kwa sisi tulivyofanyakazi, ukiletewa wewe barua nakala anapewa na mwalimu mkuu, je wizara ilifanya utaratibu huo. Ndio swali lenyewe lilivyo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, swali ni kwamba barua waliandikiwa au hawajaandikiwa.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Mjumbe, kwa swali lake kuhusu kuandikiwa barua au laa. Kwanza nataka niseme kwamba hawa walimu si wachache ni wengi wanafika 1000 na zaidi. Pamoja na hayo, walimu hao tuliwaandikia barua na kila mmoja tulimuandikia barua na kumuelezea hitilafu hizo zilizojitokeza.

Vile vile tuliwaomba kama watagundua ikiwa kuna hitilafu katika malipo yao, basi watujibu kama wameongezewa zaidi au wamepunguziwa. Mhe. Mwenyekiti, wapo wanaotujibu, lakini wengine bado hawaja-*respond* katika maandishi yetu.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, kabla sijamwambia tuendelee, nataka kujua hizi barua zilizoandikwa ilikuwa ni baada ya kukatwa au kabla ya kukatwa, maana hapa maelezo kidogo yalinipita na sikuyasikia vizuri.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, tuliwapelekea barua kabla ya kukatwa, ili wajue kitakachotokezea na waripoti kwetu haraka kama kuna kasoro yoyote kwenye malipo yao na tumefanya hivyo. *(Makofi)*

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, hayo ndiyo niliyokuwa nikieleza kwamba wamewashtukia walimu, wamewa-*frustrate* na baada ya kuona hivyo, ndio ikawa sasa waandike barua baada ya kukatwa. Kwa hivyo, naiomba sana Wizara ya Elimu, kwa sababu ndio nyenzo, malighafi pamoja na viwanda vyao, kwa hiyo barua ni muhimu sana, na chochote kitakachotokea basi ni vyema mwalimu kuandikiwa barua. Mhe. Mwenyekiti, tuendelee. *(Makofi)*

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na naomba nitoe hoja kama nilivyohoji kwenye Idara hii. Lakini kwanza naomba nimkumbushe Mhe. Waziri kwamba yeye ni mwanataaluma, ambaye wazanzibari wanamjua kuwa ni msomi mzuri. Kwa hivyo, wazanzibari wasingetegemea hata siku moja kwa nafasi aliyonayo kuruhusu ajira za walimu ambao wenye vyeti *fake*, na mimi kwa niaba ya kamati nitamsaidia yale majina ambayo tunayo pamoja na vyeti vyao.

Lakini hoja yangu kwangu kwa hapa nilihoji kwamba kuna wafanyakazi wa Mamlaka ya Mafunzo ya Amali, Wizara ya Fedha iliingiza fedha tangu mwaka 2010 Julai kwa maana ya marekebisho ya mshahara. Sasa zilipoingizwa fedha hizo kwa bahati mbaya walimu wale hawakulipwa mishahara yao na badala yake Mamlaka ya Mafunzo ya Amali wakatumia fedha zile kama *Other Charges* (*OC*), jambo ambalo si utaratibu mshahara kutumiwa kama *OC*.

Kwa hivyo, naomba maelezo Mhe. Mwenyekiti, kwa nini wizara yake ikatumia sehemu ya mshahara kama *OC* na kumbe lengo la Wizara ya Fedha ilikuwa ni sehemu ya mshahara, *Scheme of Service* ya Mamlaka ilikuwepo, lakini fedha hawakupewa na wao wakatumia kama ni *OC*.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mhe. Mjumbe kwa hicho cheo alichonipa kwamba mimi ni msomi na wala mimi si msomi isipokuwa ni mtu wa kawaida tu. Lakini alitaka tutoe maelezo kuhusu fedha za mshahara zimetumika kwenye matumizi ya *OC*.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nieleze kwamba Chuo cha Amali kinapata ruzuku na utaratibu wa kuzitumia ruzuku zinafuatana na maagizo ya Bodi ya Wakurugenzi. Ni kweli kabisa fedha za mshahara zilitolewa na wahusika wakalipwa mishahara yao na kukawa kuna bakaa. Kwa bahati mbaya sana fedha za *OC* zilikuwa ni chache na *almost* hazikuwepo. Kwa hivyo, Uongozi wa Chuo ukazungumza na Bodi na kutolewa idhini kwamba fedha hizo mnaweza kuzitumia.

Matumizi yaliyofanywa hata kama unaweza kuyaita si halali kwa maana hakukuwa na *re-allocation*, lakini ni halali kwa maana Bodi ya Wakurugenzi walitoa idhini kwamba zitumike. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, katika matumizi yaliyofanywa na *records* zote zipo, ni pamoja na ununuzi wa vifaa vya kusomeshea, chakula kwa wanafunzi waliopo dakhalia wakati ule.

Baada ya kuona gharama za matumizi ya chakula kwa dakhalia zimekuwa kubwa sana, ndipo tulipoacha shughuli za dakhalia na tukaruhusu kwa mwenye kutaka kukaa dakhalia ajihudumie mwenyewe. Hali hiyo, ipo mpaka leo na tutairudisha pale tutakapohakikisha kwamba tunazo fedha za kutosha za kuiendesha dakhalia, pamoja na ushauri mkubwa uliotoka kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi pamoja na wengine.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nikiri kabisa kwamba hili lilikuwa ni kosa, tena nataka niombe radhi kwa kosa hilo. Lakini laitani kama tungefuata utaratibu pamoja na kwamba tulipata idhini ya Bodi na kufuata utaratibu wa kuandika dokezo la kutaka *re-allocation* na tukapata idhini ya *re-allocation,* nafikiri kungekuwa hakuna hoja kubwa. Mhe. Mwenyekiti, nakubali kwamba kosa hilo lilitendeka na wala sidhani kama litaweza kutendeka tena chini ya uongozi wangu nikiwa hai katika suala hili. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Waziri amekiri kuwa lilikuwa ni kosa. Lakini taarifa ambazo ninazo ni kwamba Bodi ya Mamlaka iliridhia *Scheme of Service* ya Wafanyakazi, kwa maana hiyo ndio Wizara ya Fedha wakaingiza fedha za mshahara. Je, ni nani aliyepinga maamuzi ya Bodi kwamba walipwe fedha za mshahara mpya na badala yake fedha zile zikatumiwa kama *OC*.

Kwa nini fedha zile baada ya kuonekana ni nyingi zisirejeshwe Wizara ya Fedha na badala yake watu wakachukua maamuzi. Je, kuna maamuzi yoyote ya Wizara ya Fedha kwa matumizi yenu? Maana yake kifungu cha mishahara kisingepaswa kutumiwa kama *OC* kimya kimya hasa kwa vile Bodi ilikubali kwamba hawa walipwe mshahara huu.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri atuambie kwamba nani aliyetoa idhini kwamba fedha hizi zitumiwe kama *OC* badala ya kurejeshwa Wizara ya Fedha kama fedha halali ya kifungu hichi cha mshahara.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana. Mhe. Hija Hassan Hija suala hili tulizungumza kwenye kamati, na yeye ni Mjumbe na tulizungumza kwa mapana yake. Lakini Mhe. Mwenyekiti, nataka nimueleze Mhe. Mjumbe pamoja na Baraza lako kwa jumla, kwamba hii mishahara kweli iliidhinishwa na Bodi na Wizara ya Fedha ilitoa fedha hizo kwenye bajeti.

Mhe. Mwenyekiti, wizara kama msimamizi mkuu wa taasisi zake zote zilizomo kwenye wizara, ikaona nyongeza ya mishahara ile haikuwa halali kwa sababu tunavyo Vyuo vingi vya Amali, kama vile Chuo chetu cha Karume. Kwa hivyo, haiwezekani Mhe. Mwenyekiti, waliopo Karume wana *Masters* tuseme na walioko kule inawezekana wana *Masters* wa chini, lakini ikawa mshahara wao mkubwa kuliko wanavyopata Karume.

Kutokana na hali hiyo, tukaona hii ingetuletea matatizo, hivyo kwanza tukaizuia, lakini ilirudi kwa wenyewe mamlaka na wala sio kama tulikuwa nayo sisi wizara mikononi mwetu au mfukoni mwetu.

Mhe. Mwenyekiti, jambo ambalo nataka nilifafanue hapa kwamba hii mishahara ya mamlaka kila ambapo inapoongezeka mishahara ya serikali huongezewa, na wala sio kama wao wanakuwa utaratibu wao uko kinyume na mishahara ya serikali. Kwa hivyo, hilo ndilo ambalo wizara tuliona tukae na wenzetu wa Mamlaka, ili jambo hili tulipatie ufumbuzi zaidi. Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, mimi kweli ni Mjumbe wa Kamati na nilisema kwenye Kamati kwamba hili siliungi mkono, kwa sababu mimi natetea wafanyakazi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri kwamba ilionekana mishahara ya Mamlaka itakuwa mikubwa pengine Karume. Lakini taarifa ambazo nilizonazo mimi tena za uhakika *Scheme of Service* ya Karume ilikubaliwa na waliweza kulipwa, sasa hapo ndipo lilipokuja tatizo kwa nini mtoto A apendelewe na mtoto B azuiliwe. Kwa hiyo, mimi nakubali kwamba mshahara wa Mamlaka wastani wake ni shilingi milioni 1,300,000/= mkubwa kuliko ule wa *SUZA*.

Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu ni kwamba kwa kuwa walijua mshahara huu hauhitajiki kwa nini wakaomba na ulipoingizwa kwa nini wasirejeshe na huyu mwenye mamlaka ya kutumia kifungu cha mishahara ni nani?

Kwa kweli mimi tegemeo langu ni kwamba fedha baada ya kuonekana ni nyingi na mhasibu hilo alikiri kwamba uwezo wao ilikuwa ni shilingi milioni 20,000,000/= ya mshahara, lakini walikuwa wana ongezeko la zaidi ya shilingi milioni 40,000,000/=, kwa nini wasirejeshe Wizara ya Fedha na kusema fungu hili limezidi na badala yake wakatumia kimya kimya?

Mhe. Mwenyekiti, utaratibu ambao wameufanya Mhe. Waziri amekiri kwamba ni kosa, sasa kama ni kosa basi hutolewa adhabu. Kwa hivyo, atuambie kwa nini tuwape fedha wakati walifanya makosa?

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nijibu lile swali nani aliyetoa idhini ya kuzitumia hizi fedha. Nilizungumza wakati nilipokuwa nikizungumza kwamba Bodi ndiyo iliyotoa idhini baada ya taasisi kuishauri Bodi, kwamba tumieni fedha hizi kwa sababu ya shida kadha kadha, na kwa kuwa nyinyi hamkupata fedha zenu za matumizi ya kawaida.

Kwa hivyo, ndio maana nikasema kama ni kosa basi ni hilo la kutekeleza agizo la Bodi baada ya sisi kuiomba Bodi. Sasa kama kuna adhabu ambayo Mhe. Hija Hassan Hija ameiweka ya kuniadhibu mimi niliyesema hivyo, basi sina matatizo. Lakini nilitaka niwe mkweli katika kuyaeleza yale yaliyotokea na kujibu lile swali nani aliyetoa kibali na fedha zilizotumika nilisema zipo zimeandikwa na *record* zake zipo. Sasa sidhani kama ukiwa mkweli maana yake ndio uadhibiwe. Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, nadhani kuna baadhi ya makosa yanatendeka *in good faith* hili ni moja wapo. Kwa kweli kosa linaloweza kutendeka *in good faith*, basi hili kwa kawaida, yaani huoni namna utakavyotoa adhabu, kwa sababu ile haja ya kuchukua hatua ipo na chombo kinachohusika kilitoa idhini na haidhuru hakina madaraka, lakini kimefanya kwa nia nzuri ya kutekeleza jambo na wanasheria wapo. Lakini masuala aina kama haya huyatolewi adhabu, isipokuwa unatoa maelekezo kwamba jambo hili lisiendelee tena. Nafikiri tuendelee.

Kifungu 0701	–	Idara ya Utumishi na Uendeshaji	35,897,747,000/=
Kifungu 0702	–	Baraza la Elimu	30,000,000/=
Kifungu 0703	–	Shirika la Huduma za Maktaba	267,000,000/=
Kifungu 0801	–	Idara ya Elimu ya Msingi na Mandalizi	

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii kuomba ufafanuzi au maelezo zaidi kwa Mhe. Waziri. Wakati nilipokuwa nikichangia hotuba ya Mhe. Waziri nilieleza masikitiko yangu juu ya mishahara ya walimu hasa wa msingi, ambao wamekuja kulalamika kwangu, kwamba mishahara yao haina utulivu wamekuwa wakikatwa, yaani wamekatwa hivi mara vile, pamoja na kwamba kuna maelezo ambayo yametolewa wamekatwa kutokana na kuwa mishahara yao hailingani na taaluma zao.

Sasa hawa wengi walionilalamikia ni wale ambao wamekatwa fedha na taaluma zao zinalingana na sifa zao, lakini wamekatwa mishahara yao. Kwa hivyo, naomba kumuuliza Mhe. Waziri tokea nilipotoa maelezo yale wakati nilipokuwa nikichangia, je wamefanya utafiti ni walimu wangapi ambao wamepata usumbufu huo na kujihakikishia kwamba hao walipata usumbufu kweli walikuwa wanastahili kukatwa fedha zao, ili apate nafasi ya kuja kutoa majibu.

Kwa maana hiyo, walimu waliokatwa mishahara yao ni kadhaa na walikuwa wanastahiki kukatwa hizo fedha, mbali na taarifa ambayo Mhe. Rashid Seif Suleiman kwamba hawakupewa taarifa awali, isipokuwa walikwenda na wamekuta mishahara imeshakatwa. Mhe. Mwenyekiti, naomba maelezo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana. Mhe. Salmin Awadh Salmin ni kweli alichangia hoja hiyo na mimi nilimjibu, lakini sikumjibu kumwambia ni idadi gani ya walimu waliokatwa mishahara yao.

Vile vile kwa hivi sasa hapa niliposimama Mhe. Mwenyekiti sina, lakini ofisini kwangu ninayo, kwa sababu Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora ametuletea idadi hiyo ya walimu.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nimuombe Mhe. Mwakilishi kwamba kosa hili limetendeka na wala hatukupeleka barua kwa mtu mmoja mmoja. Kwa kweli kama tulivyozungumza mwanzo kwamba tulieleza mwanzo kupitia kwa Walimu Wakuu, na walimu wengi tayari wameleta malalamiko yao ofisini kwetu na nusu yao tumeshawapelekea Wizara ya Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Salmin Awadh Salmin na kauli hii iwe kama ni wito kwa walimu wengine ambao wanahisi mishahara yao haijatulia imepungua au imezidi, kwa sababu pia wako ambao wamezidi mishahara yao Mhe. Mwenyekiti, wanakuja na kusema ofisini kwamba mishahara yetu inaonekana sio na kima ambacho tunatakiwa tulipwe.

Kwa maana hiyo, atusaidie hilo na *Inshaallah* tutawarekebishia mishahara yao kwa wale ambao wataonekana hawana tatizo.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, ahsante. Kwa kweli mimi hoja yangu kubwa mbali ya kukatwa najua kwamba watapata haki yao kama inavyostahiki.

Lakini hali hii ya mishahara ya walimu kutokuwa na utulivu hatujui kama tunawasumbua kila wakati, yaani mwezi huu uko hivi na mwezi unaofuata vile, tunakuwa tunawasumbua na kuwa na wasi wasi, basi ule wasi wasi wao unawafanya washindwe hata kuwasomesha watoto wetu vizuri, kwa sababu hajui mwezi huu nitakatwa kiasi gani. Kwa hiyo, hali hii ya kutokuwa na utulivu mishahara ya walimu itakwisha nili?

Kwa maana hiyo, Mhe. Waziri atuhakikishie hapa kwamba utulivu sasa utakuwepo katika mishahara ya walimu, baada ya marekebisho haya ambayo yamefanywa, kwa sababu inaonekana bado hakuna utulivu wa mishahara. Sasa sijui ni wao au Wizara ya Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa nini mishahara ya walimu imekuwa haina utulivu jambo ambalo linawapa usumbufu? *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa nini utulivu wa mishahara ya walimu haupo?

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, mimi nashukuru kwanza kwa taarifa hii ambayo ameitoa Mhe. Mwakilishi, na kwa sababu wafanyakazi ambao wamekwenda kulalamikia ndio hao wamempelekea kuja kutoa taarifa, kwamba mishahara ya walimu haina utulivu.

Kwanza nataka kusema kwamba hakuna ruhusa au utaratibu wowote wa kumkata mtumishi yeyote yule wa serikali au umma licha ya walimu mshahara bila ya utaratibu na bila ya ridhaa yake mwenyewe. Sasa kama hilo lipo Mhe. Mwakilishi nitamshukuru sana kwa kushirikiana na wizara yangu na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, akatupatia taarifa hizo na kwa sababu tayari tumeshazipokea itabidi tuzifuatilie. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba kurejea tena kwamba hakuna sheria au utaratibu wa kumkata mtumishi wa umma mshahara bila ya ridhaa yake mwenyewe, na kama hilo lipo basi ni vizuri tukapata taarifa kamili, ili tukaweza kulifanyia kazi.

Lakini kama ni hili ambalo limekuwa linazungumziwa hata kwenye *budget speech* yangu lilizungumziwa la kukatwa mishahara kwa wale ambao waliweka viwango vya elimu kinyume na uhalisia ulivyo, hawa tunaendelea kuwaangalia. Mhe. Mwenyekiti, nilisema siku ile kama ni hawa hakuna *compromise* ya kuwarejeshea fedha hizi, kwa sababu wamechukua fedha kinyume na hali halisi ilivyo au uwezo wao wa *qualification* walizonazo.

Vile vile katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali alizungumzia Mhe. Saleh Nassor Juma, kwamba kuna walimu ambao wizara iliwapandisha daraja, na walimu hawa tayari wizara iliamua kuwapa viwango vya mishahara.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nilihakikishie Baraza lako Tukufu kwamba hawa tutahakikisha kuwa viwango hivi au daraja hizi zinawekwe katika *Scheme of Service* yao ya Utumishi, baada ya hayo, ina maana mishahara hii wataendelea kuipata.

Lakini kama hawa nao baada ya vile viwango vyao waliamua kuandika vyeti ambavyo hawana, basi nao fagio la chuma litawakumba kama litakavyowakumba wengine na wala hakuna *compromise* katika hili, kwa sababu huo ni utaratibu ambao tumekubaliana na katika suala zima la uwajibikaji tunasema hapa, kwamba watendaji inaonekana wanafanya hivi na vile, hata mtumishi wa kawaida naye ni mtendaji anapoamua kuidanganya serikali maana yake hawajibiki. Kwa hivyo, inapobidi kuchukuliwa hatua, basi atachukuliwa hatua. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa hilo ambalo amelisema Mhe. Salmin Awadh Salmin kama mishahara haitulii, kwa sababu watu wanakatwa mishahara yao kinyume na ridhaa zao na utaratibu, basi hili tutalichukulia hatua nasema kama Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwamba hakuna muajiri yeyote ambaye anawajibika kumkata mshahara mtumishi bila ya ridhaa yake mwenyewe. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa ufafanuzi uliotolewa na mimi nasema tuendelee. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru. Katika mchango wangu nilizungumzia suala la Mradi wa Maktaba katika Skuli ya Msingi ya Kajificheni, ambapo nilisema ulitolewa na Taasisi ya *Britain Tanzania Society* ingawa sikuitaja, lakini tafsiri rasmi ndio hiyo. Lakini baadaye ulipopatikana mradi huu watendaji wa wizara katika idara hii wakauhamishia katika Skuli ya Kisiwandui na nilitaka maelezo hapa.

Sasa Mhe. Waziri aliniambia wanafuatilia na badala yake wanafanya utaratibu, ili kupata fedha kutoka kwa wahusika hao kuitengeneza maktaba hii katika Skuli ya Kajificheni. Mhe. Mwenyekiti, maelezo haya hayaniridhishi.

Kwanza niseme hii familia ambayo imejitolea kusaidia Familia ya Bwana Rone Fanal binafsi nafahamiana nayo. Mhe. Mwenyekiti, walisikitishwa sana hata walipokuja hapa wenzetu ni wafuatiliaji wa kina wa suala la fedha zao wanapozitoa.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, hawa walipotoa fedha kwa ajili ya mradi huu walikuja mpaka na ramani wakijua Skuli ya Kajificheni iko wapi, walipotaka wakaoneshwe mradi wao wakapelekwa Skuli ya Kisiwandui wakasema hii sio, Mhe. Waziri alisema kwamba atalifuatilia, lakini sina hakika kama taasisi hii itakubali tena kudanganywa, ambapo uongozi wa wizara uliidanganya kwa kuhamisha mradi ambao ulikuwa umepelekwa Skuli ya Kjificheni na kuupeleka Skuli ya Kisiwandui.

Kwa hivyo, nilikuwa nataka *commitment* ya Mhe. Waziri, kwamba fedha hizi zisipotolewa na taasisi hii, wizara itatenga fedha kwa ajili ya kuitengeza maktaba kwa mujibu wa mradi ambao ulikuwa umeandaliwa na Skuli ya Kajificheni na tayari umeshatolewa fedha, lakini watendaji wake Mhe. Waziri wakaamua kuuhamisha na kuupeleka skuli waliyoitaka wao. Mhe. Mwenyekiti, naomba *commitment* ya Mhe. Waziri, ili niruhusu fungu hili liendelee.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Ismail Jussa Ladhu alizungumza hoja hii kwa hisia kubwa na mimi nilimjibu, lakini nilikuwa na hakika kwamba nilivyokuwa nikimjibu Mhe. Mjumbe kwa wakati ule alikuwa hasikii, kwa sababu alikuwa na mazungumzo kidogo nyuma akizungumza na amesikia hili la mwisho kama wizara tutafuatilia. *(Makofi)*

Ni kweli kama alivyosema Mhe. Mjumbe, kwamba mradi huu alipita bibi huyu Skuli ya Kajificheni na akavutika na watoto wetu walivyokuwa wakisoma pale. Lakini naomba nirudi kidogo nyuma, wakati yule bibi alipoona ile hali halisi na kutaka kuingia skuli ile kwa ajili ya kwenda kuona zaidi, basi mlinzi alimzuia pale, akamwambia hapana usinizuie mimi niko katika mradi wa *TAP* na ninamjua Mkurugenzi Vuai, nilitaka nije humu ndani nisaidie. Akamuitia Mwalimu Mkuu pale akazungumza naye na akamwambia kama ana nia ya kusaidia. Yule bibi aliyepita kwanza bibi Ana alikwenda Wizarani kwetu kuzungumza na Mkurugenzi wetu Maalim Vuai, akamueleza kuvutika kwake na Skuli ile ya Kajificheni na akaeleza kama kuna taasisi ambayo inaweza kutoa msaada kwa skuli ile.

Mhe. Spika, alitoa mapendekezo kama muandike mradi, muombe lakini msiombe kwa skuli moja, muombe kwa skuli mbili mpaka tatu. Lakini akasisitiza kwamba skuli hizo ziwe za Wilaya ya Mjini. Wizara ikatizama ni skuli gani na skuli gani ambayo tunaweza kupeleka huu mradi. Moja ya Skuli ambazo tuliweza kuona tunaweza kupeleka huu mradi ni Kisiwandui. Tukawaita wote pamoja na Kajificheni kama mnatakiwa kuandika maradi na kuupeleka.

Mhe. Spika, kwa bahati mbaya, Kajificheni wao walikuwa wana *process* refu kwa sababu hawakuwa na kile chumba cha Maktaba, wakataka waende wakafanyiwe makisio ya utengenezaji wa Maktaba. Wenziwao wao tayari walikuwa wanacho kile chumba kwa hivyo wakaandika kwa mujibu ambavyo tumewaelekeza na ile ya Kisiwandui ikenda kwanza kuliko wale ambao walitunukiwa ule mradi. Ikaja kwa Skuli ya Kisiwandui na wenyewe wale ambao walitoa msaada walikuja wakakagua. Walipojua kama sio ile skuli hasa ambayo ilikugaliwa ni skuli mbadala wakasema kama na skuli ile nyengine wataupeleka huu mradi.
Mhe. Spika, sio kweli kama Mhe. Ismail Jussa alivyoelezwa kama ule mradi sisi Wizara tuliuteka, isipokuwa Wizara kama alivyotufahamisha mama Ana kuwa ule mradi tuufanyie mapana usiwe kwa skuli moja tu. Wenzetu Skuli ya Kajificheni hawa walichelewa kupeleka mapendekezo yao wakawahi Wenziwao wa Kisiwandui. Hilo Mheshimiwa ndilo lilitokea. Nakushukuru.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, mimi nasikitishwa sana na Mhe. Naibu Waziri kwamba kama kawaida ya Mawaziri wetu wanaendelea kukubali kupotoshwa na watendaji wao.

Mhe. Mwenyekiti, kama Mhe. Naibu Waziri hafahamu nimueleze kwamba wadhamini wa mradi huu kama waliridhia kupelekwa katika Skuli ya Kisiwandui walipokuja walihoji na walikuja

mpaka na ramani kwamba hii skuli ipo katika *Stone Town* haipo katika eneo hili. Wenzetu sio kama tulivyosisi wababaishaji Mhe. Mwenyekiti.

Kama mradi ulikuwa unajumuisha kutengeneza, kama alivyosema mwenyewe Mhe. Naibu Waziri huyu bibi alipita akaingia ndani ya Skuli na aliona kama hakuna maktaba, akakubali matengenezo yote. Makisio yaliyofanywa Mhe. Mwenyekiti, yalijumuisha mpaka utengenezaji wa hicho chumba kinachotumika kuwa maktaba kuweka rafu zake au *shelves* zile pamoja na mahitaji mengine yote.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Naibu Waziri asikubali kudanganywa, hili limefanyika ni urafiki, baina ya Mwalimu Mkuu wa Kisiwandui uhusiano wake binafsi na Mkurugenzi Vuai katika hili, asitake kupotosha ama anihakikishie kwamba Maktaba hii itajengwa kupitia Taasisi hii au Wizara itakwenda kutengeneza au fungu hili Mhe. Mwenyekiti, nitalizuia. Naomba sana Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana nataka nimuhakikishie Mhe. Ismail Jussa, hawa wafadhili walitwambia kama na hii Skuli ya Kajificheni ambao huu mradi ulipoanzia watahakikisha kwamba na hapa wanapata. Nakama hatopata Mheshimiwa itakuwa ni dhima ya wizara kuhakikisha kama huu mradi tunawatengezea wanapata. Namuahidi Mhe. Mwakilishi.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nitafatilia tuendelee ahsante sana.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipatia fursa hii. Juzi hapa wakati nachangia Mhe. Mwenyekiti huku macho yakiwa na simanzi lakini moyo ulikuwa unalia kabisa, nilieleza kuhusu walimu wa skuli za msingi ambao wamepatiwa mafunzo ya kuweza kufundisha Sekondari. Katika *program* inayoitwa *Teachers Advancement Program* ambayo ilifanywa katika vituo maalum vya elimu vya Unguja na Pemba. Walimu hawa wamemaliza mafunzo haya na tayari wanao uwezo kusomesha Sekondari na wameshaanza kusomesha Sekondari karibu miaka saba iliyopita nyuma.

Mhe. Mwenyekiti, la kusikitisha sana Mhe. Mwenyekiti, hadi leo hii pamoja na ahadi ambazo bado bajeti iliyopita niliambiwa kwamba keshokutwa tutawalipa, wiki ijayo tutawalipa lakini hadi leo hii walimu hawa hawajalipwa. Nataka Waziri anambie hawa walimu ambao wame-*qualify* mafunzo ya TAP watawalipa lini mishahara yao pamoja na zile *arrears* zao ambazo tangu wamalize kozi zao hadi leo hii hawajalipwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti na ni kweli Mhe. Saleh Nassor Juma aliliuliza suala hili na nilimjibu. Nilimuahidi Mhe. Saleh Nassor, kwa sababu tayari tumekaa na wenzetu wa Utumishi na tumewapelekea *proposal* ya kulipwa walimu hawa. Namuahidi Mheshimiwa kwamba siku si za mbali, walimu hawa watalipwa na watazidishiwa mishahara yao baada ya kumaliziana na Wizara ya Utumishi na *arrears* zao ambazo wanadai kwa muda wote huo ambao walistahiki kulipwa.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu wanasheria wanasema kwamba haki ikichelewa kutolewa ni sawa na kwamba haikutolewa

kabisa. Na kwa kuwa siku kadhaa nimeshapewa ahadi kesho, keshokutwa, wikiijayo, mwezi ujao tutawalipa lakini bado walimu hawa hawajalipwa mafao yao. Je, Mhe. Waziri atakuwa tayari ikiwa ahadi aliyoiweka hakuitekeleza ndani ya mwezi huu wa Ramadhani na anachukua hajui kwamba Mwenyezi Mungu yupo, anamuona na anamsikia. (*Vicheko*)

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Saleh, Mhe. Saleh, nadhani moyo wako sasa utulie kwa kupokea hiyo ahadi.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Atamke tu kwamba Mwenyezi Mungu anamsikia na anamuona akisema sawa basi tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Tuendelee.

Kifungu 0801 Idara ya Elimu ya Msingi na Maandalizi 200,000,000
Kifungu 1201 Idara ya Elimu ya Watu Wazima na Elimu Mbadala
Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu katika fungu hili ni kama ile ya mwanzo kabisa, kama nilivyosema niliwambia Wizara kwamba mafungu yale yaliyopunguzwa juu yakachomekwa kwengine nitayahoji katika kila Idara.

Mhe. Mwenyekiti, katika Idara ya Elimu ya Watu Waziri, fungu 211100 Mishahara ya Fedha Taslim, katika fungu dogo lile lile la 211107 Malipo Baada ya Saa za Kazi *(over time).* Katika *original book* ilikuwa milioni ishini na moja, laki tisa sabini elfu. Marekebisho tuliyoletewa yakapunguza ikawekwa milioni moja, laki tisa, sabini elfu. Milioni ishirini zikafyekwa.

Mhe. Mwenyekiti, milioni 20 hizi zikenda zikaongezewa katika ukurasa wa 17 kwenye kifungu 220500 Vifaa na Huduma za Ofisi kwenye fungu dogo la 220516 mwisho kabisa, Vifaa vya kufundishia (*teaching materials*) ambalo lilikuwa ni shilingi milioni moja laki mbili hamsini na nane elfu, likafanywa milioni ishirini na moja laki mbili hamsini na nane elfu.

Mhe. Mwenyekiti, hili lilifanywa wakati tayari fungu hilo hilo huko juu limeshawekewa pesa za kutosha milioni arubaini na mbili, laki tano thalathini na sita elfu na vifaa vya kuandikia (*stationeries*). Fungu hili ambalo ukilitizama ni ongezeko kubwa sana ukilinganisha na mafungu ya miaka mitatu iliyopita.

Hoja yangu Mhe. Mwenyekiti, kwamba kule mwanzo tuliambiwa kwamba lile lilihamishwa kwa sababu ya mradi wa sera. Naomba nielezwe kwamba fungu hili kwa nini limehamishwa likapelekwa huku wakati tayari kuna vifungu vyengine vilivyonona. Kwa mfano kifungu cha viburudishaji vile vile Mhe. Mwenyekiti, ambacho kutoka mwaka jana na mwaka huu kimetoka milioni ishirini na nane hadi milioni arubaini na nane, lLakini hicho sitaki kukihoji, nataka kuhoji hili.

Mhe. Mwenyekiti, hizi milioni 20 ambazo zimekatwa kutoka malipo ya baada ya saa za kazi *(over time)* yakepelekwa katika vifaa vya kufundishia (*teaching materials*). Kuna uhusiano gani baina ya malipo ya saa za kazi na vifaa vya kufundishia. Mhe. Mwenyekiti, naomba maelezo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amalli: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kama ambavyo nilizungumza kwamba, hili lilitokana na utaratibu wa Wizara ya Fedha ambazo wametuwekea. Labda kwa kuhisi tunataka tufafanue zaidi ndio ikabidi hivi vifungu tuvigawe. Lakini fungu hili tumekusudia kufanya zoezi la watu wetu wa kisomo, kusoma na kuandika na kuhesabu kwa ajili ya kununua karatasi na uchapishaji wa *photocopy* pamoja na wino.
Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, maelezo hayaniridhishi. Na sasa nitamuomba idhini yake Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali akubali fungu hili tulikate miloni 20. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti kama nilivyosema kwanza nashindwa kuiona hiyo *link*, kule mwanzo angalau wali *justify*, lakini hapa nashindwa kuiyona *link* ya malipo baada ya saa za kazi, hata katika marekebisho likahamia katika vifaa vya kufundishia.

Lakini kama maelezo ya fungu hili limekusudiwa ni makaratasi kama alivyosema Mhe. Mwenyekiti katika fungu hilo hilo alilolitaja ambalo limehamishiwa vifaa vya kuandikia stationeries limeongezeka kutoka milioni mbili laki mbili, arubaini na moja elfu, mia saba. Mwaka 2009/2010 likashuka kidogo likawa milioni moja laki saba, arubaini na nne elfu. Mwaka 2010/2011 na mwaka jana likawa milioni saba, na arubaini na nane elfu. Mwaka huu limeombewa arubaini na mbili milioni, laki tatu thalathini na sita elfu.

Mhe. Mwenyekiti, hivi hizi hazijatosha hayo matumizi ambayo anayasema Mhe. Naibu Waziri, hata bado katika vifaa vya kufundishia tuongezewe tena milioni 20. Wakati mwanzo waliweka milioni moja tu pale Mhe. Mwenyekiti. Naomba nimueleze Mhe. Naibu Waziri kwa nini nisiliombe Baraza au Kamati hii ya Matumizi ikazikata milioni hizi 20 ambazo zinaonekana zilikuwa hazina matumizi, zimebandikwa hapa ili kutumika zikaja kunufaisha watendaji tu.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana na kwa heshima na taadhima namuomba Mhe. Ismail Jussa Ladhu, milioni hizi 20 atuachie. Kwa sababu licha ya hizi kazi ambazo Mheshimiwa ambazo nimesema tunataka kuzifanya kwa ajili ya wanakisomo wetu. Lakini pesa hizi pia hazitoshi, kuna pesa ambazo itabidi tuzipate kutoka UNESCO ili ziweze kusaidia zoezi hili Mhe. Mwenyekiti liweze kufanyika.
Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Ismail Jussa Ladhu, hii hatukuondosha kwa ajili ya ubabaishaji, kama ambavyo nimetangulia kusema. Lakini ni kutokana na marekebisho ambayo tuliona turekebisha ili Waheshimiwa wa Baraza la Wawakilishi tuwe na ufafanuzi zaidi wa moja kwa moja badala ya kuzungumza kwa *item* moja tu.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, mimi kutokana na uzoefu ya *trend* hii nashindwa kushawishika. Lakini niseme naupasi mpira kwa Kamati ya kina Mhe. Hija Hassan Hija, nadhani hilo watakwenda kujiridhisha kama kweli zaidi ya nyongeza ambayo tayari imeshafika kutoka milioni 1, 2, 7 mpaka ikafika 42 za *stationeries* na bado wakawa wanahitaji milioni 21 nyengine za kufundishia zilizohamishwa kutoka malipo ya *over time*. Nadhani hili kama ilivyokawaida Kamati zetu zitafanya kazi ya kufatilizia.
Kwa sasa hivi namuona ndugu yangu Mhe. Zahra Ali Hamad yuhoi kwa hivyo naomba tuendelee Mhe. Mwenyekiti, Ahsante.
Kifungu 1201 Idara ya Elimu ya Watu Wazima na Elimu Mbadala 202,000,000
Kifungu 1402 Chuo cha Kiislamu Pemba 30,000,000
Kifungu 1403 Chuo cha Kiislamu Unguja 30,000,000
Kifungu 1404 Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, wakati nikichangia kuhusu elimu ya ufundi, nikasema Wizara imeweka *position* gani hii elimu ya ufundi. Bahati nzuri hii taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia ndio kitovu chetu cha kuchukua maeneo mbali mbali kutoka katika skuli za ufundi kwa mfano Kengeja na hivi vyuo vya Amali vilivyopo. Mbona uzito uliopewa elimu ya ufundi ni mdogo sana, sikupata maelezo yoyote.

Pia nikalinganisha chuo hichi au taasisi hii ina jina kama hili iko Mbeya na Arusha. Je, ina uzito gani ukilinganisha na vyuo taasisi zile. Naomba maelezo kidogo kuhusu uzito uliopewa kuhusu elimu ya ufundi Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumpa maelezo Mhe. Rashid Seif Suleiman kuhusu kama kuna mzigo mzito uliopewa Chuo cha Ufundi basi nitoe hayo maelezo.

Mhe. Mwenyekiti, Chuo cha Ufundi hivi sasa tunakiandaa katika jumla ya maendeleo tunayoyapangia kiwe kinatoa vyeti vya digirii na sio tena pale walipo. Mazungumzo hayo yamezungumzwa kati ya Wizara na Bodi na yanafanyiwa kazi.

Lakini pia Chuo cha Ufundi kina mashirikiano makubwa na vyuo vyengine vilivyokuwepo Tanzania Bara ili kujiweka na wenzetu waliokuwepo Bara wenye vyuo vya ufundi kama chetu. Lakini vile vile kama walivyofanya SUZA Chuo hichi sasa kinajiandaa kutoa masomo au mafunzo ya masomo ya sayansi kama *special program* itakayoweza kuwasaidia hapo baadaye, wanafunzi wetu ambao hivi sasa hatuna walimu wa sayansi, basi hao wanafunzi tutakaowajenga hapo wataingia katika mkumbo wa kutoa wanafunzi kusoma masomo ya sayansi. Kwa hivyo hiyo ndio mizigo na ndio *program* tulizonazo kwa Chuo chetu hichi cha Ufundi cha Karume.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, nimeyasikia maelezo ya Mhe. Waziri, lakini masikitiko yangu makubwa kwamba, kwa sababu elimu ya juu ni suala la Muungano, nilitegemea Mhe. Waziri angelinambia katika mfuko wa Elimu ya Juu kwa Tanzania wao wanapata kiasi gani kwa ajili ya Taasisi hii. Kuna taarifa ambazo zinaeleza kwamba Taasisi hizi za Mbeya na Arusha zinapata fungu lake kutoka mfuko wa Elimu ya Juu ya Jamhuri ya Muungano.

Sasa Kama Waziri katika moja ya maendeleo ya Chuo hichi naona hakuyataja, hana habari au habari hii haina ukweli au ikoje hata ikawa sisi Zanzibar bado hatujapata fungu letu katika huu mfuko wa Elimu ya Juu kwa ajili ya Taasisi hii.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Rashid Seif, iwapo chuo chetu cha ufundi cha elimu ya juu, kwa sababu Elimu ya Juu ni suala la Muungano, basi kama Chuo chetu kinapata chochote kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
Nataka kumuelezea kwamba hatuna tunachokipata na mimi naomba dua tusipate tuendelee hivi hivi tunavyokwenda kujidhatiti wenyewe, kujihudumia wenyewe, kama ilivyokuwa mambo mengine hayaonekani tija yake. Chuo chetu kikianza kudadisi masuala ya kupata chochote cha kuendesha chuo tutaanza sasa kuandamwa.

Kwa hivyo sisi hatupati chochote pamoja na kwamba ni elimu ya juu tunajitegemea wenyewe. Ila inapotokea haja ya kutafuta mikopo basi tunatafuta, lakini ufanisi wake ni mdogo. Kwa hivyo sasa tumeamua tusiwe na haja ya kuombaomba katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuviendesha vyuo vyetu vya Elimu ya Juu. Hilo nililisema mwanzo na sasa hivi nalisema tena kwamba hatupati chochote na hatuna haja wala hatuombi.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, naona Mhe. Waziri katupa kubwa kidogo. Sasa ikiwa tuna haki yetu ikiwa hatupewi ni suala jengine, Mhe. Waziri angetwambia tu kuwa sisi hatupewi. Kuliko kutwambia hatuna haja, basi ikiwa hatupewi sawa. Lakini maneno yangu ya mwisho hii Taasisi inajengwa na Taasisi nyengine ndogo ndogo, kwa hivyo tunaomba sana Wizara badala ya kuwa ile ni Taasisi kubwa ambayo kwa hapa Zanzibar na hizi ndogo ndogo azishughulikie. Baadaye tuachiwe tupumuwe. Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.
Kifungu 1404 Taasisi ya Karume Sayansi na Teknolojia 164,000,000
Kifungu 1405 Chuo cha Uwalimu Benjameni Mkata 30,000,000
Kifungu 1406 Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar
Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia katika eneo hili la Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar SUZA nilieleza kwamba pamoja na maendeleo yanayopatikana ambayo kwa kweli hayaridhishi. Maendeleo yanapatikana taratibu sana. Lakini nilizungumzia kuhusu chuo hiki kuwa ni mwanachama wa TCU. Inaonekana wenzetu wa SUZA wamekuwa au wamejitoa katika baadhi ya maeneo.

Mhe. Waziri alipokuwa akijibu alisema kwamba wao bado ni wanachama wa TCU isipokuwa wamejitoa katika suala zima la udahili wa wanafunzi. Sasa ninalotaka kusema kwamba moja kati ya kazi kubwa au shughuli kubwa inayofanywa na TCU ni eneo hili la udahili wa wanafunzi katika wanachama wake. Sasa wao wamesema wamejitoa katika udahili.

Mhe. Mwenyekiti, nataka anambie kwa nini wamejitoa au ni sababu zipi zilizowafanya wajitoe katika udahili wa wanafunzi ambao wanataka kuomba katika chuo hichi na wao wakiwa ni wanachama wa TCU.

Mhe. Naibu Waziri Elimu na Mafunzo ya Amali: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti kwa idhini yako na namshukuru Mhe. Salimini ni kweli suala hili alilichangia na Mhe. Waziri alimjibu.

Sababu mbili kuu ambazo Chuo chetu cha SUZA zilijitoa kwenye TCU. Kwanza tulijiunga lakini tulikuwa hatujajitayarisha. Kwa sababu unapojiunga katika TCU katika suala hili zima la udahili unaweza kuletewa wanafunzi kutoka TCU kutoka upande wowote wa Tanzania. Wanafunzi ambao wanakuja wanahitaji malazi.

Kwa mara ya kwanza ambapo tulichukua wanafunzi na tukawaweka katika skuli yetu ya Lumumba ili kwa kujishikiza ili mwaka wa pili watafute sehemu nyengine ya kukaa. Ilianza kuwa ni sakata na yale ya Bara na ya wenzetu yaliyokuwa yakiwakuta ilikuwa karibu na sisi yatukute wanafunzi kugoma. Walifikia hatua mpaka ya kuchukua kitanda wakakiweka na chandarua kati kati ya uwanja wakaita waandishi waje waone ni namna gani ambavyo tunawalaza. Tukahisi kwa sababu bado ilikuwa hatujajitayarisha na pahala pazuri pa kuwalaza wanafunzi wetu ambao watakuja kutoka popote Tanzania. Tukaona ni vyema basi tujitoe.

Sababu ya pili Mhe. Mwenyekiti, wewe utakuwa ni shahidi kwa hili Baraza lako tukufu katika awamu iliyopita walisimama baadhi ya Wawakilishi wakasema kutokana na yale mambo ambayo yanafanyika kule ambapo tumewaweka wanafunzi wale. Yalikuwa hayaendani na mila na utamaduni na silka zetu. Wakaona sasa tunazalisha mambo ambayo si silka wala si utamaduni wetu. Wakatamka kwenye Baraza tujitoe, na sisi Wizara kwa kuona uzito wa jambo lenyewe tukaamua tujitoe.

Lakini nimuahidi Mhe. Salmin Awadh pindipo SUZA tutakapojipanga na tukawa na sehemu nzuri za kuweza kuwalaza wanafunzi wetu basi haya mambo mengine yanarekebishika. Kama Baraza lako tukufu litaridhia kama sasa turudi basi tutakuwa tayari kurudi Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Mwenyekiti na ninamshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa ufafanuzi alioutoa, isipokuwa hili la pili hii sababu ya pili ambayo Mhe. Naibu Waziri ameieleza ambayo hakuiacha wazi tukaifahamu, kwa sababu anasema kuna mambo ambayo yalikuwa yanafanyika kinyume na maadili yetu. Sasa nataka kujua ni mambo gani hayo ambayo yalikuwa yanafanyika huko SUZA ambayo yanakwenda kinyume na maadili yetu ya watanzania.

Mhe. Mwenyekiti: Ametaja migomo ambayo inatokea kwenye vyuo vyengine huko pia ikaanzishwa kuja hapa. Sasa jambo hilo si jambo la kawaida kwa hapa kwetu, ndicho alichokisema.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Sasa suala langu la mwisho nataka kumuuliza Mhe. Waziri kwa maana hiyo anataka kutwambia kuwa Chuo chake sasa hivi hakichukui wanafunzi kutoka maeneo mengine wanachukua wanafunzi wa Zanzibar tu.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Mwenyekiti: Muda wetu tuliopanga kumaliza shughuli unakaribia.

Mhe. Waziri Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa kuwa muda ulio mbele yetu hautoshi kumaliza shughuli zilizo mbele yetu, hivyo naliomba Baraza lako tukufu tuendelee kuweka kanuni ya muda kando ili tuweze kumaliza shughuli zilizo mbele yetu. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ninakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Salmin kwa hivi sasa wanafunzi wetu ambao tunao ni wazanzibari wenyewe, isipokuwa tunao wachache kutoka ile TAKILUKI kama ambavyo tulizungumza kwenye bajeti yetu, wale ambao wanasoma lugha Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, basi tumwache kidogo apumue.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, juzi wakati nachangia nilitoa tanbihi kwa serikali kwamba Chuo Kikuu SUZA ni chuo pekee cha serikali hapa nchini, na kwa kuwa mwaka jana tulipotembelea pale chuo walikuwa wanataka kuanzisha *program* zao muhimu sana, kwa ajili ya kuweza kutusaidia haya mabadiliko pamoja na kuimarisha haya mapinduzi ya kilimo Zanzibar kwa kuanzisha program ya *environmental science* pamoja na *faculty of agriculture* Pemba *branch*. Lakini la kusikitisha ni kwamba hadi leo hii wameshindwa SUZA kufungua *program* mbili hizi muhimu kutokana na kwamba wanawekewa *ceiling*, kwa hivyo wanabanwa kwenye bajeti na kushindwa kuanzisha programu hizi, je serikali ina maelezo gani katika hili na lini Wizara ya Elimu kwa kushirikiana na Wizara watawa-*support* hawa SUZA kusudi kuanzisha hizi programu muhimu sana kwa wananchi wetu.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti naomba kumjibu Mhe. Nassor mkereketwa, mwana mapinduzi, muasisi wa ASP, suali lake kuhusu hizo programu zinazozungumzwa za SUZA zitaanzishwa lini na kwa namna gani na kwa mfuko upi. Kwanza nataka nitoe maelezo kwamba SUZA *almost* ni taasisi inayojitegemea na inaweza kupata mikopo, inaweza kupata misaada na kadhalika. Na ndio maana majengo yetu tunayojenga kule Tunguu tulipata fedha za msaada nyingi sana kutoka BADEA. Na hivyo hivyo *Vice Chancellor* wetu hivi sasa amejijengea heshima kubwa sana kutambulikana katika sehemu mbali mbali, ndio lile tulilolizungumza, usiposafiri ukenda ukakutana na wenzako utabakia unatia mbwembwe tu hapa mitaani hupati chochote.

Sasa *Vice chancellor* wetu hilo amelijua mapema anakwenda mbio sana, amezitengeneza *program* ambazo sisi tunaziunga mkono sana lakini kwa bahati mbaya kutokana na ufinyu wa bajeti yetu, zile fedha tulizompangia milioni nne na kidogo ndio zitakuwa ndio zile zile, kwa hivyo yeye mwenyewe ameanza kwenda mbio sana na sisi tunamuunga mkono kutafuta mikopo au misaada. Lakini nataka nilihakikishie Baraza hili *Vice Chancellor* ameandaa programu nzuri sana sidhani kama atakosa hiyo misaada na hiyo mikopo wakati wowote atazianzisha hizo program alizozikusudia.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, lazima tukubali kwamba mabadiliko ya tabia nchi kwa visiwa vidogo kama hivi vya Zanzibar ni tatizo. Kuna baadhi ya visiwa tunaweza tukavipoteza kwa kuendelea kuzama na vishaanza kuonesha dalili visiwa hivi vyengine vinataka kupata tatizo hilo. Kwa mfano katika jimbo la Mhe. Haji Faki Shaali pale sasa serikali kuendelea kuwa bakhili kwa kushindwa ku-*support program* muhimu kama hii ya kuanzisha kutoa wataalamu wa mazingira, basi ni kuhatarisha hata wapiga kura wao Mawaziri ambao kesho kutwa wanataka uwaziri tena, wapiga kura watakuja kuzama kwenye visiwa washindwe kupiga kura.

Sasa mimi nilichokuwa ninakitaka hapa na ubakhili wa serikali Mhe. Mwenyekiti vile vile unarudisha nyuma hata mipango ya serikali yetu madhubuti inayopanga, kwa mfano hii programu ya mapinduzi ya kilimo ingelikuwa pale SUZA tushawa-*support* kuanzisha wataalamu wa kilimo kwa kufungua tawi la kilimo kule Pemba ninaamini mpango huu wa kilimo tungeona mzuri sana. Ningeomba serikali katika hili natoa tanbihi kwa serikali kwamba waache ubakhili, ni lini serikali itaacha ubakhili na ku-*support program* za wataalam hawa kina Profesa Idrisa Rai na Dr. Ahmada pale ili kuona maendeleo ya nchi hii yanapatikana, huu ubakhili hasa utaachwa lini, wakishasema ubakhili tushaacha basi mimi nasema tuendelee Mwenyekiti.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti ninampongeza sana Mheshimiwa wangu mkereketwa Mhe. Saleh kwa mchango wake wa kusema kwamba hata serikali hatuwezi kutoa chochote katika kuzianzisha programu hizi. Nataka nimthibitishie kwamba katika bajeti yetu hii, tumetenga sikumbuki vizuri lakini zaidi ya bilioni 1.6 za majenzi ya eneo la pili yake ambalo litakuwa kubwa zaidi kuliko hili eneo la mwanzo kule Tunguu, kwa kuvikusanya hivyo viprogram tunavyovitafuta na kuviweka humo. Kwa hivyo sio kwamba serikali ya Mapinduzi Zanzibar inatoa mchango ziro hapana, tunachangia *structure* na huku tunatafuta msaada, tukipata msaada inawezekana tukaanza hizo programu zetu mwaka huu, za kilimo za nini. Lakini hatukupata msaada tutajikuna tutapojipatia katika bajeti ya mwakani. Tutahakikisha hizo program zitalipiwa na serikali yetu ya mapinduzi lakini kwa sasa tunatafuta misaada na tamaa ya kuipata tunayo.

Kifungu 1406 Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar 4,200,000,000
Kifungu 1407 Mamlaka ya Mafunzo ya Amali Zanzibar 2,200,000,000
Kifungu 1408

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti wakati nilipokuwa nikitoa mchango wangu juu ya mitaala iliyofundishwa nilikuwa nina wasiwasi juu ya elimu inavyokwenda katika programu zetu mbali mbali. Kwa hivyo ningetaka ufafanuzi juu ya suala hili baina ya mitaala yetu ya *primary, secondary* inavyokwenda katika mipango yetu ya elimu.

Mhe. Spika: Mheshimiwa sijui kama unakusudia eneo hili au jengine maana hii ni mikopo kwa ajili ya elimu ya juu.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Mhe. Mwenyekiti nilipokuwa nikichangia kuhusu elimu ya juu nilisema kuwa wanafunzi wanaosoma mafunzo ya dini na kiarabu Wizara haiwapatii mikopo juu ya kujiendeleza na elimu yao hii lakini bado wanasomeshwa. Sijui kuna sababu zipi za msingi zinazofanya hawa wasipate mikopo.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti kama nimemfahamu vizuri suali lake anasema kwa ufupi kwa nini walimu wanaochukua mafunzo ya dini na kiarabu hawapatiwi mikopo. Kama hivyo ndivyo nasema kwa wale walimu walioko vyuoni wanaosomesha masomo hayo hawa wanapatiwa mikopo, na kama wapo hawajaomba tunahimiza waombe watapatiwa mikopo. Lakini Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa ninasoma hotuba yangu nilisema kwamba au sikusema kwa sababu ya muda nasema mikopo ni mikopo, na mikopo lazima ilipwe. Sasa tukimkopesha kada fulani ambavyo sio *priority* kwa taifa na kwa hivyo kuiajiri itakuwa ni vigumu, sasa tunafikiri mara mbili kutoa mikopo.

Kwa hivyo kama ni wanafunzi wanaotaka kuchukua somo la kiarabu na dini, *priority* yetu iko kwenye sayansi na hesabati. Hata wale wanafunzi wanaotaka kuchukua masomo ya *public administration*, au wanaotaka kuchukua sheria hao pia kwetu sisi si *priority*, kwa sababu hawa kusema kweli *market* yao katika uajiri ni ndogo. Kwa hivyo pamoja na jibu alilolitoa kwa walimu wanaosomesha dini na kiarabu kusema kwamba hawa tutawapa mikopo, lakini kwa wanafunzi nataka niseme kwa upana zaidi kwamba wanafunzi hawamo katika *category* hiyo kwa sababu *market* yao katika kuajiriwa ni ndogo sana.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Sasa Mhe. Mwenyekiti, kama Waziri kakubali kuwa walimu wanaoendelea watapata mikopo sawa, je lakini hawa wanafunzi ambao wanajiunga na vyuo hivi kwa fani hizi. Najua kwamba elimu ni ghali mtu kuweza kujihudumia, lakini pia vyuo vyetu vinakubali kuwafundisha hawa sasa ni haki yao na wao kusoma na kupatiwa mikopo. Lakini serikali imeona walio na haki ni peke yao watu wa sayansi na hesabati hawaoni kuwa hapa wanaidhoofisha hii fani ya dini na kiarabu kufanya hivyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti ninakushukuru na ninamshukuru sana mtoa hoja. Mhe. Mwenyekiti hakuna serikali ambayo haina kipaumbele, serikali zote zinakuwa na kipaumbele na hii sio kama tutafanya maisha. Lakini kutokana na mahitaji ambayo tunayo hivi sasa tuna walimu wengi ambao tumesomesha wa dini na kiarabu bado hatujawaajiri. Lakini kuna kada ambazo tuna mahitaji nazo na hatujawasomesha. Kwa hivyo hivi sasa kwa wakati huu kwa mwaka huu tunasomesha zile kada ambazo tuna mahitaji nazo, walimu wa dini na kiarabu bado tunao. Na kama Waziri alisema wale ambao tayari tumewaajiri kwa sababu hawatahitaji ajira mpya, hata wakikopa wana uwezo wa kurudisha, wale bado tunawapa fursa ya kuweza kuendelea. Kwa hivyo naomba Mheshimiwa Mwakilishi akubaliane na sisi katika hili.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti kwenye bodi ya mikopo tulihoji fedha ambazo serikali yetu ilitoa kwa ajili ya mikopo ya vijana wetu ya elimu ya juu karibu bilioni nane, bilioni 7.7. Kwenye orodha ambayo Mhe. Waziri ametupatia, ametupatia majina na fedha bilioni nne. Kwa hivyo kwanza naomba nijue bilioni 3.7 ziko wapi.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima yako naomba nimjibu Mhe. Hija hoja yake kama ifuatavyo. Anauliza baada ya ile orodha tuliyoiwasilisha kuna pengo la shilingi kama bilioni tatu hazijulikani wala hazikuonesha ziko wapi. Nataka niseme orodha ile ilikuwa inahusu wale ambao wanadaiwa, wamemaliza masomo na wapo katika ajira, sasa hawa ndio tunaowafuata kutulipa pesa zetu. Wale waliopo vyuoni wale majina yao hayamo mule, kwa sababu wale bado hawajamaliza kusoma na hawana ajira. Sasa hizo pesa bilioni tatu zinazotafutwa ndio hizo tunazozitumia kuwalipia hawa wanaoendelea na masomo yao.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti nimemfahamu Mhe. Waziri, nimeshtuka ile orodha inasema 2001 mpaka 2011 sasa kuweka sawa maelezo yake, naomba anipatie orodha ya hao walioko chuoni ili nijiridhishe kwamba kweli hawa sio wale.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti nasema orodha tunayo na hata kesho, kesho kutwa tutampatia.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti ninakushukuru na mimi kupata nafasi kidogo kupata maelezo ya ziada. Lakini Mhe. Mwenyekiti nilikuwa naomba mnielewe kwamba kuzuia vifungu sio ukorofi. Lakini hii inaonesha kwamba tunakaa na wananchi na haya ni maneno tunayoyazungumza hapa ni maneno ya wananchi. Kwa hivyo ukionekana unasimama simama usionekane kama labda mkorofi unamsumbua Waziri, haya ni maneno ya wananchi.

Mhe. Mwenyekiti katika ufafanuzi niliokuwa ninaotaka kwa Mhe. Waziri alipokuwa akitoa hotuba yake alielezea zaidi katika hii bodi ya elimu ya juu, kwa wale wanafunzi ambao wanategemewa kupatiwa mikopo au wafanyakazi ambao wanategemewa kupatiwa mikopo. Lakini alielezea kwamba nadhani wanamalizia katika shahada ya pili. Na niliomba kwamba kuna vijana wetu ambao wanataka kusoma katika ngazi ya PHD na kwa kweli katika eneo Mhe. Mwenyekiti tuna upungufu mkubwa sana. Maana yake ukiangalia hata wahadhiri wetu katika vyuo vyetu vikuu wengi wana *masters* na hawa *masters* vile vile wanahitaji na wao waweze kusomeshwa. Sasa katika ngazi hii bado tuna upungufu. Nimemsikia Mhe. Naibu Waziri alielezea kwamba tunaangalia vipaumbele au tunaangalia mahitaji. Mpaka sasa hivi Mhe. Mwenyekiti nikiangalia hata mashirika ya kimataifa yaliyoko Zanzibar wengi wanaoajiriwa ni wageni, kwa sababu sisi hatuna wataalamu wenye sifa hizi.

Sasa nilikuwa ninamuomba tu Mhe. Waziri anijulishe je katika hawa vijana wanaohitaji na kwa bahati nzuri ni wachache ambao wanahitaji kusoma katika ngazi ya PHD sijui wataweza kuwasaidia vipi. PHD Mhe. Mwenyekiti tulipitisha hapa sera ya walemavu, na katika sera ya walemavu moja ya kitu tulichokiangalia kuwapa kipaumbele na nafuu walemavu kila pale ambapo wanahitaji. Sasa kuna kijana wetu ambaye yeye ni mlemavu wa ngozi, Mhe. Mwenyekiti huyu anataka kuchukua masomo ya sayansi lakini mkopo anashindwa kuupata kwa sababu hajatimiza yale masharti, anatakiwa kwanza alipe ili aanze ile *pre* na halafu aendelee. Lakini basi hakuna huruma kwa hawa walemavu na hasa walemavu wenyewe wa ngozi, Mheshimiwa hili nilikuwa naomba anisaidie, maana yake kwa kuwa kuna kijana mmoja au wawili kwa nini tukaachana na hii *pre at least* waweze kulipiwa kwa sababu wazee wao wamejitahidi mpaka sasa hivi. Nilikuwa naomba maelezo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ninakushukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti na ninamshukuru Mhe. Hamza ni kweli alipokuwa akichangia alilizungumza hili, na Mheshimiwa kwa wale waombaji wa PHD ambao fani zao ni kipaumbele kwa serikali yetu kwa wakati huu, ninamuahidi na ninamuhakikishia hawa tutawapa mikopo. Japo Mhe. Mwenyekiti katika vipaumbele vyetu ambavyo tumeweka basi kipaumbele kimoja ni wale wenzetu walemavu, tunawatizama kwa jicho kubwa, kwa jicho la huruma kwa hivyo Mheshimiwa Mwakilishi kama yupo huyu mtu ambaye anaomba mkopo na yeye hajapata basi tunaomba atuletee ili tumsaidie.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Nilikuwa kidogo namuomba Mhe. Waziri anielewe kwamba huyu ambaye ni mlemavu yeye alitakiwa kwanza kuna lugha wenyewe mnaitwa *pre,* yaani kwanza ajilipie halafu baadae aka-*qualify* kusoma yale masomo ya sayansi. Sasa huyu yeye sie yule anayetaka PHD. Lakini Mhe. Mwenyekiti hichi kitu mimi nilichokuwa nazungumzia chengine kwa wale wanaotaka kuchukua PHD kwa sababu tatizo ni kwamba tumeanza kuajiri walimu kutoka nje na tunapokuwa tunaanzisha vyuo vyetu lazima tuwe na wahadhiri wa kwetu. Sasa hao wahadhiri wa kwetu ina maana kama hatujawasomesha katika hizo ngazi za juu sasa sijui tutafikia hatua gani.

Na kwa bahati nzuri kama nilivyosema tunapitisha bilioni nane hizi, lakini hawa wanaoomba PHD ni kidogo sana. Mimi nadhani Mheshimiwa angelijaribu kutumia busara kwa kuangalia hili lakini kwa yule mlemavu wa ngozi yeye kwa bahati anataka kuanza ule mkopo wa mwanzo ili aanze *pre,* lakini *pre* anatakiwa alipe sasa ule uwezo wa wale wazee wake sasa hivi kulipia *pre*

kwa kweli hali ishakuwa dhofu. Na kwa bahati nzuri kijana huyu alitakiwa kwenda Moshi akasome kuna shirika moja la kimataifa kutokana na ule ulemavu wake wa ngozi na kutokana na jitihada yake walitaka kumchukua wakamsomeshe kule, lakini wazee wake Mhe. Mwenyekiti wameogopa. Wameogopa kwa sababu wakimpeleka Moshi kwenda kusoma basi kurudi huku inakuwa bahati nasibu.

Sasa ndio maana tukataka hii huruma ya serikali, na kwa kuwa ninamjua Mhe. Waziri rafiki yangu ni mkereketwa sana wa elimu, basi hebu amuangalie huyu kijana wetu angalau wamsaidie.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti nimemfahamu Mhe. Hamza na kawaida *pre* sisi huwa hatutoi mkopo, lakini bodi, wizara na kushirikiana na yeye Mwakilishi tutahakikisha kwamba mwanafunzi huyo anasoma.

Kifungu 14 – Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu 8,000,000,000
Kifungu 1409 Baraza la Upimaji na Tathmini ya Elimu

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, kwenye Baraza la Mitihani Mhe. Naibu Waziri alijibu majibu ambayo hata kwenye Kamati aliyajibu kwamba wao kama wizara walipelekewa jina hili. Lakini tutakumbuka kwamba Baraza hili sheria tuliyopitisha ni Sheria ya Baraza la Mitihani la Zanzibar na sio Baraza la Upimaji na Tathmini ya Elimu. Sasa Waziri hana taarifa hiyo lakini ukweli ulivyo Baraza hili tulipitisha sheria hiyo Baraza la Mitihani, kwa hivyo naomba maelezo zaidi pengine hata Mwanasheria Mkuu anaweza kunifahamisha wapi jina hili lilibadilika na je, kuna uhalali gani wa kubadilika jina hili.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikubaliane na Mhe. Hija Hassan kwamba kuna makosa katika uandishi wa hili Baraza la Tathmini kwa mujibu wa sheria ambayo ilipitishwa na Baraza hili. Lakini pia naomba nikumbushe kwamba tulijibu hoja hii iliulizwa nadhani na Mhe. Salmin Awadh Salmin, na tukaijibu kwa urefu wakati tulipokuwa tunazungumza hoja ya bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria. Kwa hivyo, kwa mujibu wa kanuni ya 58 fasili ya 5 nadhani haikuwa na haja ya kuizungumza tena kwa sababu inatukataza kufanya hivyo.

Lakini kwa faida ya Mhe. Hija kwa sababu alilouliza ni la msingi sana, na pengine kwa wale wengine waliokuwa hawakuwepo tulisema kwamba kwa utaratibu wa baada ya sheria au mswada kupitishwa katika Baraza, kwa kawaida wataalamu wetu wa ofisi yetu na wa Baraza wanakaa pamoja kuangalia marekebisho ambayo yamefanywa na baadae ule mswada ndio unapelekwa kwa Katibu wa Baraza kwanza anathibitisha, kwamba kweli yale yote yaliyorekebishwa basi yalikuwa ni sahihi, halafu tena ndio unapelekwa kwa Mhe. Rais kwa ajili ya kutiwa saini.

Sasa kwa mswada huu baada ya kurudi kwa Mhe. Rais kwa kawaida ofisi yetu sisi tunaiandikia Wizara husika kwamba sheria yenu imeshatiwa saini na Mhe. Rais, tunawapa nakla ya sheria ile iliyotiwa saini na kuwapa maelekezo mengine ambayo yanahitajika. Baada ya sheria hii kurudi na kuwaandikia sisi Wizara ya Elimu, Katibu Mkuu wa wizara hiyo ya Elimu alipiga simu akaniuliza kuhusu kubadilika hili jina na mimi nikamwambia basi ngoja tuangalie na wenzetu wa

Baraza la Wawakilishi na wakatuthibitishia kwamba marekebisho hayo yaliyofanyika yalikuwa ni sahihi, lakini baadae wenyewe Ofisi ya Baraza iligundua kwamba kweli walifanya makosa katika lile jina, sio Baraza tu lililorekebishwa jina lakini hata jina la sheria yenyewe basi ilikuwa imebadilika na wametuandikia barua rasmi kutaka tufanye marekebisho.

Naomba nimhakikishie Mhe. Hija kwamba kwa mujibu wa kifugu cha 65 cha sheria Nam. 7 ya mwaka 1984 Mwanasheria Mkuu anao uwezo wa kufanya marekebisho kwa makosa kama hayo na tutafanya hivyo katika muda ambao si mrefu.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, kwanza niombe radhi kama kuna kanuni ambayo nimekiuka kwa sababu ya ubinadamu, lakini lengo lilikuwa ni kusimamia ile haki ya Baraza. Kwa hivyo, naomba radhi lakini namshukuru Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa hivyo jina hilo litabadilika kwa mujibu tulivyoamua katika mswada wa sheria.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii ili nipate ufafanuzi juu ya hoja yangu hii. Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia hotuba ya Mhe. Waziri katika eneo hili la Baraza la Mitihani nilizungumzia juu ya suala zima la watoto wale ambao walifutiwa mitihani yao, na kwamba ilikuwa ni adhabu ambayo imetolewa kwa wakati ule na nikamuomba Mhe. Waziri wakati atapofanya majumuisho basi atupe maelezo juu ya hatua zilizochukuliwa kwa wale wahusika, na kwa sababu muda unaonekana ni mkubwa, kuna ama maofisa au walimu waliohusika na kadhia ile ya kuvujisha mitihani.

Sasa alipofanya majumuisho Mhe. Waziri hatukupata maelezo na nilitaka kujua tu kwamba ni maofisa wangapi ambao wamegundulika kujihusisha na kadhia ile na walimu na hatua zilizochukuliwa. Kama hakuna hatua zilizochukuliwa mpaka sasa ni lini hatua zitachukuliwa kwa sababu bado muda inaonekana unakwenda.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, na pia namshukuru Mhe. Salmin. Mhe. Mwenyekiti, wakati namsaidia Mhe. Waziri wangu kujibu nililijibu suali hili kwa urefu sana, na nilisema kama kuna walimu wetu wakuu ambao tayari tumeondoa ngazi ya walimu wakuu tumewaweka walimu wa kawaida. Lakini kuna maafisa wengine wawili ambao kesi zao ziko polisi na tulielezea pia kwamba kuna barua ambazo tulizitoa za watuhumiwa wote kujieleza, barua zile tayari nusu na robo zishajibiwa.

Mhe. Mwenyekiti, hatua nyengine tutazichukua baada ya utafiti wetu wote au ripoti zote zile ambazo tumewapelekea barua kumaliza kujieleza. Mimi nataka nimhakikishie Mhe. Salmin kwa yoyote yule ambaye amehusika katika kadhia hii kama ambavyo niliwahi kusema katika majibu yangu ya hapa Barazani, na leo nasisitiza kama hatua thabiti zitachukuliwa juu ya watu hawa.

Mhe. Mwenyekiti, suala hili lilikuwa ni suala zito na suala ambalo lilikuwa ni *crisis* ndani ya nchi, si vizuri tukalifanyia vishindo vikubwa ni vizuri tukenda kwa taratibu lakini tukahakikisha yoyote ambaye anahusika anapatikana, na haki inatendeka katika hili. Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, isipokuwa Mhe. Mwenyekiti, wakati wa tukio lile wizara yake ilitoa taarifa katika Baraza lako tukufu juu ya kadhia ile kwa wakati ule. Je, Mhe. Naibu Waziri wakati hatua zitakapochukuliwa atapata nafasi ya kuliarifu Baraza hili ili kujua ni hatua gani zilizochukuliwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, kama alivyozungumza Mhe. Salmin ni kweli kwamba utaratibu huu utapofikia hatma yake basi tutahakikisha tunatoa tamko ili Wawakilishi na wananchi wote wapate taarifa juu ya hili Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi nilipokuwa nikichangia sehemu hii nilionesha wasiwasi wangu juu ya usahihishaji wa mitihani ya darasa la saba na la kumi mwaka jana (2011). Walimu walioshirikishwa katika usahihishaji kwa darasa la saba walikuwa ni 307, ambapo 300 walitoka Unguja na walimu saba walitoka Pemba. Wale wa darasa la kumi walimu 460 walikuwa ndio wote, 445 walitoka Unguja na 15 walitoka Pemba. Kwenye *check up* walikuwa ni watu 45, 43 walitoka Unguja na wawili kamili walitoka Pemba, na maafisa waliohusika walikuwa 33 ambapo 30 kutoka Unguja na watatu kutoka Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, nilitaka Mhe. Waziri anieleze walitumia kigezo gani katika kuchukua walimu hawa mpaka ikawa Pemba kuna saba, kumi na tano, mbili na tatu.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Mohammed Haji alipokuwa akichangia alilizungumza hili kwa uchungu mkubwa na sisi wizara kama wizara suala hili tumeliona Mhe. Mwenyekiti. Lakini kama nilivyolizungumzia mwanzo hapa wakati nafanya majumuisho kumsaidia Mhe. Waziri ni kuwa hili linatokana na uchache wetu wa bajeti tuliyonayo. Mwalimu ukimtoa Pemba akija Unguja analipwa posho mbili, posho ya kujikimu na posho yake ya kazi. Kwa hivyo, ukitizama kihesabu utaona ni wachache ambao wanatoka Pemba, lakini kihesabu ya fedha inakuwa pesa ni kubwa kuliko wale wanaotoka Unguja.

Lakini vile vile hili tumeliona na kama Wizara tunaahidi kwamba tutalirekebisha na vizuri haya masuala yote sasa yatakuwa kwenye Baraza hili la Mitihani la Tathmini, hivyo watajiweka vizuri kuhakikisha walimu wetu wote wanapata fursa hii ya kuweza kusainisha mitihani kwa pamoja. Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na maelezo laini, mazuri ya Mhe. Naibu Waziri bado sijaridhika na maelezo yake. Nataka anihakikishie kutakuwa na uwiano gani baina ya Pemba na Unguja katika kutekeleza kazi hiyo.

Mhe. Mwenyekiti: Majibu aliyotoa Mhe. Naibu Waziri ni kwamba tatizo ni suala la fedha, kuwasafirisha walimu kutoka Pemba kuja Unguja itahitaji fedha nyingi kwa sababu ya fedha ya kuwakimu, haikuwa kwamba Pemba watoke wangapi au vipi lakini tatizo ni la fedha. Nadhani hii tuendelee.

Kifungu1409– Baraza la Upimaji na Tathmini ya Elimu	Sh1,564,000,000
Kifungu 1410 – Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu	Sh 90,000,000

Kifungu 1411 – Taasisi ya Elimu Sh 72,000,000
Kifungu 1601 – Idara ya Mafunzo ya Ualimu

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, katika jumla ya mchango wangu nilizungumzia mambo mawili yanayohusiana ambayo nitayajengea hoja hapa. Moja Mhe. Mwenyekiti, niliendelea kuvihoji vifungu mbali mbali ambavyo nilivisema pale vilivyopunguzwa katika fungu la malipo baada ya saa za kazi na baadae vikahamishiwa kwengine. Sasa Mhe. Mwenyekiti, katika Idara hii ya mafunzo ya ualimu katika *vote* ile ile 211100 mishahara ya fedha taslim hiyo *sub vote* ya malipo baada ya saa za kazi ambayo ni 211107, hii awali ilikuwa ni shilingi 66,260,000/-, imekatwa hapa ikabakishwa shilingi 1,260,000/- na zile shilingi 65 elfu zilizokatwa hapa Mhe. Mwenyekiti, zikahamishiwa katika fungu 220200 kwa sababu ya viburudishaji, ambapo awali ilikuwa shilingi milioni tatu katika fungu la 220201 ilikuwa shilingi milioni tatu ikafanywa shilingi 68, 135,000/-.

Kwanza Mhe. Mwenyekiti, mimi siamini kwamba kunahitajika gharama hizo za viburudishaji kwa Idara hii kiasi hiki, ndio maana nikawaambia hawa mawaziri wawe wanaangalia sana watendaji wao kwamba huu uhamishaji wa vifungu hivi mara nyengine maelezo yake hayawiani. Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi hapa naomba jambo moja tu kwa Mhe. Waziri au Naibu Waziri halafu tukubaliane tuendelee, naomba hiyo na ndio maana nikasema niunganishe kwa sababu katika mchango wangu pia nilizungumzia *teacher's centres* ambazo pia ziko katika idara hii hii.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, katika huu ukataji kataji siku shilingi milioni kumi zilichukuliwa kwengine zikenda zikaongezewa pale kwenye ukurasa wa 23 vote 263100 ruzuku, ambapo na matumizi ya vituo vya walimu, *teachers resource centre* ambayo imewekewa shilingi 20,480,000. Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu nilisema vituo hivi mafungu waliopewa hayakidhi haja. Kwa mfano, Kituo cha *Teacher's Centre* cha Walimu wa Maandalizi kilichoko pale Saateni walimu wanakaa chini hivi hivi mbali ya kwamba vingi havina huduma.

Sasa mimi nilikuwa namuomba Mhe. Naibu Waziri anikubalie moja tu, tukubaliane na ile kupunguza kutoka kwenye fungu la malipo baada ya saa za kazi, lakini baada ya kupeleka katika viburudishaji akaweka shilingi 68 milioni, mimi naomba fungu hili lirejee kama lilivyokuwa mwanzo jumla yake ilikuwa ni shilingi 25 milioni zirejeshwe hizo na shilingi elfu kumi badala ya hizi shilingi 80 milioni na elfu kumi iliyopo hapa, na badala yake hizi shilingi 50 milioni zilizopo hapa anikubalie Mhe. Waziri azihamishie katika ruzuku kwa matumizi ya vituo vya walimu badala ya pale kwenye shilingi milioni ishirini ukurasa wa 23 liongezeke hili ili likafanye tija iliyokusudiwa badala ya kupunguzwa likapelekwa hapa.

Akinikubalia hilo Mhe. Mwenyekiti, wala sina ya kumnyanya sana itakuwa hatuendelei. Kwa hivyo ndani ya Idara moja ninaomba tu ahamishe pale apeleke kwengine kuliko kupeleka pale kwenye viburudishaji naomba hilo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima kubwa nakubaliana na Mhe. Jussa kama alivyolitoa.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwa mtindo ule ule wa tulivyotumwa na wananchi wetu lakini kumsaidia Mhe. Waziri mimi hapa nilikuwa sina tatizo sana isipokuwa

ushauri tu. Mhe. Mwenyekiti, tunahitaji walimu wetu wawe watulivu sana ili wanafunzi wetu wapate elimu inayohitajika. Imeonekana katika hoja za Waheshimiwa wengi pamoja na yangu mimi, kwamba kuna madai mengi walimu wanadai kwa wizara. Sasa mimi naomba Mhe Waziri kwamba katika haya mafungu ambayo tuna wasiwasi nayo kwa zile fedha ambazo zitazokuwa zimeonekana katika fungu ambalo tumehisi kuwa si sahihi ziende kwengine, basi ni vizuri tungelipunguza haya madeni ya walimu.

Kwa sababu kuna walimu walioajiriwa juzi tu kuna mshahara wao wa mwezi wa nne wamelipwa nusu wanaambiwa nyengine watalipwa mpaka lini na bajeti ndio tunamaliza. Sasa vitu kama hivi vidogo vidogo vinawavunja moyo hawa walimu wetu.

Jengine nilizungumza kwamba kuna walimu wanaosomesha walimu, kuna mafunzo wenyewe wataalamu Wizara ya Elimu wanajua wanaita *TAP* na *ZAP*. Sasa hao walimu wanaowasaidia hao walimu kuwajengea uwezo mpaka leo wanadai na bajeti ndio tunapitisha. Kwa kuwa bajeti hii ya Mhe. Waziri ndio inayosema rasimu ya bajeti inayotumia *program*, kwa hivyo *program* ya wanaodai humu haimo, watalipwa lini hawa.

Sasa mimi nadhani ili Mhe. Waziri mafungu yake Mhe. Waziri wa Fedha asije akayachukua akayarejesha Wizara ya Fedha, nilikuwa naomba basi hawa wanaodai hasa hawa walimu wanaowasaidia walimu wengine ambao wanaita mafunzo ya *TAP* na *ZAP* waweze kuwalipa, lakini vile vile na walimu ambao wameajiriwa mwezi wa nne kama sikosei basi angalau ile nusu ya mshahara wao wanaodai walipwe. Huu tu ndio ulikuwa ushauri wangu. Mhe. Waziri kama atakuwa na maelezo ya ziada ya kunibisha nitasimama tena, akinikubalia basi nitaunga mkono twende zetu ahsante.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, dalili ya Mhe. Hamza kuunga mkono bajeti yangu nimeshaipata. Nilipokuwa natoa maelezo ya bajeti hii nilisema walimu wanaodai maposho yao, wenye kasoro zao za viinua mgongo hawa wa *TAP*, *ZAP*, na wengineo katika bajeti yetu ya mwaka huu pesa tunazo na tutahakikisha wanalipwa. Na hili nataka nitoe ahadi kwamba nitasimamia mimi mwenyewe nihakikishe hawa walimu na wengineo wanalipwa. Kwa sababu maelezo yaliyozungumzwa toka juzi na leo kuhusu walimu ni mazito yametu-*touch* sote, na sote sasa tunataka kuhakikisha mimi na Naibu Waziri wangu mikopo ya walimu basi tena, haki za walimu basi tena, mikato ya walimu basi tena, kama hatuna namna ya kuzitafuta pesa nyengine za kufanya sherehe za elimu bila ya malipo, sijui nini basi tusifanye hivyo maana hawa walimu sisi tunasema wanakatwa kwa hiari yao, hawa hawakatwi kwa hiari yao kwa sababu wanalalamika, ingekuwa kwa hiari yao wangenyamaza kimya, lakini madhali wanalalamika hawaipendi hii mikato yao.

Kwa hivyo, kwanza tunathibitisha kwamba pesa za bajeti zipo tukianza tu, Mhe. Hamza tupe ruhusa bajeti yetu ipite ikishapita bajeti yetu pesa tutazitumia kuwalipa hao wenye madeni yao, hilo tumeshaahidi toka mapema. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa bahati nzuri na Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora alisema hiyo kwamba hakuna mshahara wa mtumishi yoyote utaokatwa bila ya ridhaa yake.

Kifungu 1601 – Idara ya Mafunzo ya Ualimu Sh 220,000,000
Kifungu 1701 – Idara ya Elimu Sekondari

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti nakushukuru, kama nilivyosema mwanzo pale kuna wengine huwa tunachangia masuala ya kisera. Nilipokuwa nikichangia katika matokeo ya mitihani ya miaka 2007 mpaka 2011 yaliyotiwa katika jadweli, nikasema imeonesha kwamba wanafunzi waliopata *division four* na *zero* ambao hawa ndio wamefeli ni asilimia 85 kwa mujibu wa takwimu iliyotolewa na Wizara ya Elimu. Sasa ndio nikasema kwamba je, matokeo yale sisi yameturidhisha? Na kuna hatua gani ya kurekebisha matokeo ya wanafunzi wetu ili kuweza kuona kwamba tunafungua sekondari, tunaendesha sekondari lakini *out put* yetu ni nzuri. Sasa naona kidogo hili halikujibiwa kuna marekebisho gani yanayofanyika.

Kwa mfano Mhe. Mwenyekiti, tuna sekondari kumi hizi zilizojengwa na fedha za *World Bank,* lakini hatukuoneshwa matayarisho yoyote ya walimu, matayarisho ya *labour assistance* ambao ndio watu wa sayansi hao. Sasa kidogo tuna wasiwasi kwamba je, mambo hayo yakoje hebu tuelezeni kidogo matokeo yale sisi tumeridhika nayo au tunafanya kitu gani cha kuongeza uwezo wa wanafunzi.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, suali hili tumeshalijibu nilipokuwa nafanya majumuisho, pengine Mhe. Rashid Seif alikuwa hayupo au alikuwepo lakini ndio kauliza ili asikike tena si tatizo. Mhe. Mwenyekiti, *division four* bado amepasi mtu ingawa haturidhiki nayo, nataka niliweke wazi hili. Sisi tunaridhika na *division one, two* kosa kosa *three* lakini sio *four,* na hizi division *zero* ndio kabisa. Sasa kama asilimia aliyoisema ya kuanzia *division zero* mpaka ngapi sijui ni asilimia 80 huko ni kuanguka sisi haturidhiki nako. Juhudi tunaichukua, tunaweka miundombinu thabiti tumeshajenga skuli za kileo zenye maabara, *chemistry*, *phyisics*, *biology*, *mathematics* na skuli nyengine hata na *computer science*. Tunajitahidi kuondoka tulipo tunakwenda mbele zaidi.

Kuna mradi ule wa *USAID* wa kusomesha kompyuta tokea darasa la kwanza, la pili, la tatu mpaka la nne uko katika *pilot stage*. Tunaajiri walimu wapya, juzi tumeletewa ruhusa kuajiri walimu 111 wa sayansi, 54 ni *degree* na wengine ni stashahada. Hapo ndipo twendapo hatujafika bado lakini ndipo twendapo tunaelekea huko.

Katika bajeti tutakayoipitisha leo mna fedha za kununua vifaa vya maabara, kuna malalamiko wanafunzi wetu wanasema wanasoma *theory* hawasomi *practise,* tunataka tutoke huko na *alhamdulillah* tumeshanunua na fedha tunazo tutaendelea kununua. Vikalio Mhe. Ismail Jussa alisema hata ile Skuli ya Chekechea pale Saateni walimu wanakaa chini, limetu-*touch* hilo wala hatulifurahii. Kama nikizungumza na wenzangu tukikubaliana hatua ya mwanzo ya vikalio kupeleka tupeleke Saateni mimi ningefurahi sana, tukaliondosha suala hili *once and for all*. Nataka niseme tunajitahidi tupeni nafasi, *give me the tools I will finish up the job.* Hilo ndilo naweza kusema hakuna hata mmoja atakayeridhika kwamba tunaridhika na hapa tulipo haturidhiki, lakini jitihada tunafanya na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atatusaidia.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mimi Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Waziri kwa kuiona hii *concern*. Najua kwamba suala hili ni zito na halina jibu la moja kwa moja, lakini umuhimu wa suala hili ni kufanya tathmini. Kwa sababu tukiwa tunakwenda tu kwanza

sikubaliani kwamba *division four* si *fail*, tukubaliane hapa kwamba *division one, two, three* ndio wamepasi kwa sababu wanao uwezo wa kwenda mbele, lakini *division four* tukiendelea kui-*defend* kwamba ni kupasi tunaendelea kuangusha elimu. Kwa hivyo, tukubaliane na matokeo yanayotoka na tufanye tathmini ili tuone kitu gani kinachoendelea. Tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu 1701 Idara ya Elimu ya Sekondari Sh .301, 000,000/=
Kifungu 2001 Idara ya Mipango na Sera Pemba

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwa kumsaidia tu Mhe. Waziri wangu na swahibu wangu.

Kama alivyoeleza yeye mwenyewe kwamba katika mipango ya masuala ya elimu, kwa kuangalia kuwa hivi sasa hataki tena kuomba omba kwa wenzetu upande wa pili. Kwa hivyo kahangaika wee! Mwisho kaamua na yeye apumue.

Sasa katika Idara hii ya Mipango na Sera Pemba, ninajua katika ujenzi inawezekana pengine masuala haya ikawa yanashughulikiwa Makao Makuu, lakini ninadhani baadae akija akitoa maelezo ataniweka sawa.

Lakini kama kuna ujenzi ambao pengine unashughulikiwa na Mipango Pemba basi hili ninajaribu kulizungumza, lakini litakuwa kijumla jumla linaweza likagusa mpaka Unguja kwenye suala zima la ujenzi, huu ujenzi wa miradi yetu mikubwa mfano kama sekondari tumeshatoa shukurani sana na hata Mhe. Waziri nilimshukuru katika skuli yangu ya Kwamtipura.

Sasa kitu kinacholalamikiwa Mhe. Mwenyekiti, hapa kwenye suala zima la *tendering*. Suala hili nilikuwa naomba sana Mhe. Waziri hebu liangalie kwa karibu na kwa sababu utaratibu wa *tender* una magumashi mengi. Sasa Mhe. Waziri wewe upo juu ya kiti inakuwa hujui lakini kuna magumashi mengi na ambayo wakati mwengine yanaleta masuali yasiyokuwa na jawabu.

Sasa wenzetu katika suala zima la utawala bora basi tokea suala la *tendering,* linawekwa *open tender* kama kawaida ninajua munafanya inapofanya *evaluation.* Lakini mwisho kabisa katika ule utoaji wa *tender* basi tunaomba utumike kama ule utaratibu wanaofanya wenzetu, inaekwa kwenye bodi pale wana-*display* wanakuja wote wanaangalia na hata yale matokeo yote, kuanzia wa mwanzo, wa pili mpaka yule anayekosa ili kila mmoja anakuja pale anajiona ili kuondoa haya maneno madogo madogo.

Sasa hili ndio maana nikasema Mhe. Mwenyekiti, zaidi ninataka kumsaidia Mhe. Waziri kwa sababu tumeanza kupata malalamiko. Sasa ndio maana tukasema haya malalamiko siku zote hatutaki malalamiko, mimi ninaamini bajeti ya mwakani Mhe. Mwenyekiti, hapa itapita kama uji.

Maana yake hapa haya mengi ambayo tuliyokuwa tunayohoji hapa mwakani hayatojitokeza tena. hilo tu Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa ndio angalizo langu. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri maelezo kidogo kama yapo.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, naomba kujibu hoja za Mhe. Hamza za *tendering*.

Mhe. Hamza siku hizi amekuwa mwanasiasa mshupavu na ni mzuri sana. Alianza vizuri akasema kwamba ni swahibu wangu, mpenzi wangu, mkereketwa mwenzangu na kadhalika. Ninataka nimsaidie lakini kila akipiga buti ananitisha na buti zake zinakuwa kali.

Sasa kama unataka kunisaidia Mhe. Hamza si tukutane tu tutazungumza baadae. Lakini hapa buti pale buti, sasa hizo buti zinakuwa nyingi zinatisha. Pamoja na hayo Mhe. Mwenyekiti, ninakubaliana na ushauri wake kwamba tuwe *open*, na huo ndio utawala bora, ni lazima mambo yawe wazi. Tutakapotangaza *tender* tutatangaza *openly* kwenye vyombo vya habari na magazeti. *(Kicheko/Makofi).*

Tutafanya *selection* kwa kufuata utaratibu na sheria, na tukishachagua yule wa kupata *tender* tutamtangaza na kumzungumza na kubandika maeneo yetu ya kusoma taarifa nje, yeyote anayetaka kusoma kama hakuridhika ile taarifa iliyotoka kwenye redio atakuja pale atasoma.

Nasema ninamshukuru sana Mhe. Hamza, ninakubali ni swahibu wangu na mwezangu na tena mimi na yeye tunatoka mbali labda siku hizi kasahau tu. Tulipokuwa toka *pentagon* tulikuwa pamoja yeye.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, ninaungana mkono na ninakubali mawazo yake na ushauri wake.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, unajua ninapopiga buti hapa, ninataka kuhalalisha kwa sababu nikimfuata mheshimiwa pembeni kwa mambo mazito, mara unakuja kuambiwa kwamba Hawara harithi, sasa hii ndio ile nilikuwa ninaisisitiza.

Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu 2001 Idara ya Mipango na Sera Pemba	Sh.227, 000,000/=
Kifungu 2201 Idara ya Utumishi na Uendeshaji Pemba	Sh.14, 689,253,000/=
Kifungu 2301 Idara ya Elimu Pemba	Sh.30, 000,000/=
Kifungu 2501 Idara ya Elimu ya Watu Wazima na Elimu Mbadala Pemba	Sh.25, 000,000/=
Kifungu 2801 Idara ya Mafunzo ya Ualimu Pemba	Sh.28, 000,000/=
Kifungu 2901 Idara ya Elimu Sekondari Pemba	Sh.38, 000,000/=
Kifungu 2902 Idara ya Teknolojia ya Habari Unguja	shs.120, 000,000/=
Kifungu 3001Idara ya Teknolojia ya Habari Pemba	shs.21, 000,000/=
Jumla ya Fungu	**shs.71, 050,000,000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 23 WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI

Kifungu 0401 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti	shs.25, 633,919,000/=
Kifungu 0703 Shirika la Huduma za Maktaba	shs. 200, 000,000/=
Kifungu 0801 Idara ya Elimu ya Msingi na Maandalizi	shs.4, 958,315,000/=
Kifungu 1201 Idara ya Elimu ya Watu Wazima na Elimu Mbadala	shs.2, 094,098,000/=
Kifungu 1402 Chuo cha Kiislamu Pemba	shs.25, 000,000/=
Kifungu 1406 Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar	shs.6, 057,959,000/=
Jumla ya Fungu	**shs.38, 969,291,000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha makadirio ya fedha za wizara yangu bila ya mabadiliko au pamoja na mabadiliko, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali makadirio hayo.

Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Saa 9.25 jioni Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 24/07/2012 saa 3.00 asubuhi)